

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 8 Julai, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani:-

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

MHE. CHRISTOPHER OLE-SENDEKA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI): Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Nishati na Madini Kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka 2008/2009.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE (K.n.y. MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA NISHATI NA MADINI): Taarifa ya Msemadi wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Katibu ili atuongoze katika shughuli zinazofuata. Napenda kwa heshima na taadhima nitambue uwepo wa Katibu

Mkuu wa Chama cha Mabunge Jumuiya ya Madola Mheshimiwa Dr. William Shija, ambaye yupo hapa leo pamoja na ujumbe wake. Naomba Dr. William Shija, uweze kusimama tunashukuru sana kwa kuwa na mgeni Mtanzania aliyeonyesha mfano na yupo sasa kwenye medani ya Kimataifa. Ahsante sana kwa kazi zako kwa Taifa hili. Tunakukaribisha sana jisikie uko nyumbani hapa Dodoma. Naomba mtambue pia kwamba ile Taarifa ya Kamati ya Rais kuhusu usimamizi wa sekta ya madini tayari tumeipata na imegawiwa.

MBUNGE FULANI: Hatujajawiwa.

SPIKA: Basi itagawiwa sasa hivi kwa sababu iko mezani tayari. Ningedhani kwa utaratibu mzuri ingebidi nimwite Naibu Waziri ili atamke kwamba imewekwa mezani.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani:-

NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI: Taarifa ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini.

SPIKA: Naomba sana iweze kugawiwa itasaidia sana katika mjadala unaofuata.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 167

Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa 2004

MHE. OMAR ALI MZEE aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali katika dhamira yake ya kutekeleza Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya 2004 ni kujenga uwezo wa kukabiliana na majanga kama moto, dharura za ajali pamoja na kudhibiti na kukabiliana na majanga kwa kutumia vyombo vya dola:-

Je, ni mikakati gani umechukuliwa katika kujenga uwezo huo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. PHILLIP S. MARMO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mbunge wa Kiwani, kama ifuatavyo:-

Kutokana na kuongezeka kwa matukio na madhara yanayotokana na maafa nchini, Serikali kuitia Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004 na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje imebuni mikakati mbalimbali, kujenga na kuimarisha uwezo na taasisi zake katika kukabiliana na maafa. Baadhi ya mikakati iliyochukuliwa katika kujenga uwezo wa vyombo vyaa dola ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Kujenga uwezo wa vikosi vyaa Zimamoto na Uokoaji kwa kuvipatia mafunzo, vifaa na magari mapya ya kisasa yenye uwezo wa kukabiliana na majanga ya moto pale yanapotokea.

Kwa mfano kati ya mwaka wa fedha 2004/2005 hadi 2006/2007 jumla ya Halmashauri 20 zilipewa fedha za kununua magari mapya ya Zimamoto. Mkakati wa Serikali wa muda mrefu ni kuhakikisha kwamba kila mkoa na wilaya nchini zinapatiwa gari moja la Zimamoto.

(ii) Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 Bunge lako Tukufu lilijadili na kuitisha Sheria ya Zimamoto na Uokoaji ambayo pia inahusisha Sera ya Menejimenti ya Maafa ya Mwaka 2004 pale inapoainisha ulazima wa kufunga vifaa vyaa tahadhari za moto vinavyoijendesha vyenyewe mara moto unapotokea (*Automatic Suppresion System*) kwenye majengo yenye urefu wa zaidi ya mita 28 kwenda juu sawa na ghorofa 8.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaelekeza mkoaa na wilaya nchini kuunda Kamati za Menejimenti ya Maafa. Kufuatia hatua hiyo tayari Idara ya Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu imeendesha mafunzo juu ya wajibu na majukumu ya Kamati hizo katika mikoa 14. Zoezi la kutoa mafunzo katika mikoa iliyobaki inaendelea.

Jeshi la Polisi limepeewa kamera maalum za kusoma Taasisi ya mwenendo wa magari mbalimbali ili kuweza kudhibiti madereva wanaovunja sheria kwa kuendesha mwendo wa kasi kuliko ilivyoelekeza kanuni za usalama barabarani.

Aidha, Jeshi la Polisi limeongezea uwezo wa kupewa pikipiki na vifaa vingine ili kukabiliana na matukio yanayoweza kusababisha maafa hasa mijini.

Mwisho Serikali ilikuwa inaandaa na kuendesha mafunzo ya majoribio yaani *simulation exercises* kwa ajili ya kuijanda kukabiliana na maafa ya aina mbalimbali. Chini ya mafunzo hayo ya majoribio Tanzania ilishiriki katika zoezi lililojulika kama X Blue Ruvuma lililofanyika mwaka 2006 huko mkoani Mtwara. Zoezi lilijumuisha washiriki kutoka Jumuiya ya Maendeleo ya Afrika (SADC). Zoezi hili lililenga hasa kutoa mafunzo ya namna ya kukabili maafa yanayosababishwa na mafuriko.

MHE. OMAR ALI MZEE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Pamoja na uwezo huo uliopewa je, kwa nini watu wetu wanapoteza maisha pale janga linapotokea.

Pili, je Serikali inawachukulia hatua gani wale wote wanaosababisha majanga makubwa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. PHILLIP S. MARMO): Mheshimiwa Spika, kwanza kimsingi maafa yanapotokea huwa hatuna taarifa ya awali, maafa yanatokea na kwa mujibu wa sera zetu wale walio katika eneo hilo lazima wajitahidi iwezekanavyo kadri taarifa hazijapelekwa kwenye Kamati ya Taifa ya Maafa.

Pili, kama nilivyosema hapo awali ni kwamba tuna Kamati mbalimbali za Maafa katika ngazi zote kuanzia vijiji, kata, wilaya, mkoa na Taifa. Hivi ndivyo sera inavyosema na ndivyo sheria inavyosema tunaomba wananchi wote washirikiane na Kamati za Maafa zilizoko katika maeneo yao.

MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Ningombaa niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Wizara hii imejiandaa kushughulikia maafa barabarani na maafa mengine je, ni lini Wizara hii itakuwa na mkakati maalum wa kushughulikia maafa yanayotokea baharini, maziwani na katika mito?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. PHILLIP S. MARMO): Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na matukio ya ajali hasa za baharini na kwenye maziwa na hasa Ziwa Victoria. Kama nilivyosema awali tumeunda Kamati za Maafa katika kata na vijiji vyote hapa nchini.

Kamati hizo zishughulikie maafa yote ikiwa ni yale maafa ambayo yanatoka kwenye maziwa yetu na kwenye bahari. Kwa vile ndiyo wako karibu kwenye maeneo na wanawenza kushughulikia maafa kwa makini zaidi na pale ambapo uwezo wao kirasilimali fedha na rasilimali watu unapungua basi taarifa inatolewa kwenye ngazi za juu ya mkoa na baadaye Taifa.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri napenda kuuliza swali moja la nyongeza.

Kimsingi watu wana wajibu wao katika kukabiliana na matatizo lakini tatizo mara nyingi inakuwa ni vifaa. Je, haoni Mheshimiwa Waziri sasa wakati umefika wa Serikali kuamua kwa makusudi kutafuta angalau helikopta moja au mbili ambazo zitawenza kuyafikia matukio ya ajali kwa haraka na kuweza kuwasaidia wananchi ili wasipoteze maisha yao bure?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. PHILLIP S. MARMO): Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna umuhimu wa kuwa na vitendea kazi kama helikopta katika kukabiliana na maafa.

Tulipokuwa tunaimarisha Kitengo cha Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu maeneo ambayo yamezingatiwa ni pamoja na kuwa na helikopta. Marafiki zetu wengi wametushauri na wako tayari kutusaidia ikiwa ni pamoja na Serikali ya Urusi.

Hivyo napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwa ujumla kwamba pamoja na vifaa vingine ambavyo tunatarajia vitakuja kutumiwa na Kitengo cha Maafa itakuwa ni pamoja na helikopta. Kwa sasa tunategemea zaidi helikopta za Polisi na za Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Na. 168

Uhaba wa Dawa Zahanati ya Manga

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI (K.n.y. MHE. PINDI H. CHANA) aliuliza:-

Kwa kuwa, Ilani ya Uchaguzi ya CCM inasema kuwa, Serikali itaboresha huduma za afya nchini; na kwa kuwa, kuna zahanati nchini ambazo hazipati dawa zinapohitajika kwa wakati:-

Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuboresha na kutatua tatizo hilo hasa kwenye zahanati ya kijiji cha Manga na Madilu Kata ya Madilu Wilayani Ludewa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli wakati mwingine baadhi ya zahanati nchini zimekuwa zikikosa madawa kwa wakati. Serikali imekuwa ikifanya juhudzi za makusudi ili kuhakikisha kuwa zahanati zote nchini zinatoa huduma kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, katika azma ya Serikali ya kuboresha utoaji huduma, upo mpango kabambe wa Serikali wa uagizaji wa dawa unaoitwa “*Intergrated Logistic System*” (*ILS*). Katika mpango huu kila zahanati zikiwemo zahanati za Manga na Madilu, imetengewa fedha na Serikali kiasi cha sh. Milioni moja na laki tatu (1,300,000) kwa mwezi. Fedha hizo hupelekwa na Serikali kwenye akaunti za Bohari ya Madawa (*Medical Store Department – MSD*) na zahanati husika huagiza dawa kufuatana na Bajeti

ya fedha hizo. *Medical Store Department (MSD)* husafirisha kwenye Hospitali ya Wilaya na Hospitali za Wilaya husambaza kwenye vituo vya kutolea huduma husika.

Mheshimiwa Spika, katika Zahanati ya Manga na Madilu kama zilivyo zahanati nyingine na vituo vya afya Wilayani Ludewa, hupokea mgao wa dawa na vifaa vya tiba mara moja kila robo ya mwaka.

Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008 zahanati hizo zimepokea dawa tarehe 18 Oktoba, 2007 na tarehe 22 Februari 2008. Mnamo tarehe 25 Aprili, 2008 dawa zenye thamani ya shilingi 1,715,300/= zilipelekwa tena na kupokelewa katika Zahanati ya Manga. Katika Zahanati ya Madilu dawa zenye thamani ya shilingi 1,068,600/= zilipelekwa na kupokelewa.

Aidha, dawa na vifaa muhimu vya tiba ambavyo hutolewa kwa mfumo wa “*indent system*” ambapo fedha za kununua madawa kwa ajili ya Halmashauri hupelekwa “*Medical Store Department (MSD)*” na Halmashauri huandaa mahitaji ya kila kituo na kuwasilisha “*Medical Store Department (MSD)*”.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine dawa na vifaa hivi vimeduwa havipatikani kwa wakati muafaka kutoka katika Bohari zetu za madawa (*Medical Store Department*) (MSD). Katika kukabiliana na matatizo hayo Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa imeduwa ikisambaza dawa na vifaa katika zahanati zake zikiwemo Manga na Madilu kwa kutumia akiba iliyopo ili kuziba pengo kabla dawa hazijapokelewa kutoka “*Medical Store Department (MSD)*” baada ya zahanati kuwasilisha maombi kwenye Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM imezingatiwa katika suala la kupanua utoaji Huduma za Afya Nchini. Mpango wa kujenga zahanati kila kijiji na Kituo cha Afya kwa kila kata utaanza kutekelezwa katika bajeti ya mwaka 2008/2009. Napenda kuchukua nafasi kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na viongozi wengine wote kuendelea kuhamasisha wananchi kuhusu ujenzi wa Zahanati na vituo vya afya nchini.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika kata jirani na hiyo ya Madilu kuna Kata inaitwa Mwambao ambao iko kandokando ya Ziwa Nyasa na kuna kituo cha afya kinaitwa Makonde. Serikali ilitoa gari kwa ajili ya kuwashudumia wagonjwa na kupeleka dawa, lakini kule hakuna barabara. Kwa hiyo gari lile mpaka limeharibika kwa sababu lilikuwa linakaa Ludewa mjini.

Je, Serikali iko tayari kuwanunulia wananchi wa Mwambao boti yenye injini ndio isaidie kuwasomba wagonjwa na kupeleka dawa kwenye maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, Prof. Mwalyosi anazungumzia eneo la Mwambao na Makonde na kwamba kuna tatizo la barabara na anafikiria kwamba tukiwa na utaratibu wa kutumia boti tunaweza tukasaidia katika mpango huo.

Nataka tu niseme kwamba jiografia ya Ludewa anaifahamu vizuri na kwamba kama dawa zinapelekwa na haziwezi kufika kwa wananchi kwa maana ya kwamba barabara zetu si nzuri mimi naamini kabisa kutakuwa kuna haja sisi na ye ye kukaa kwa pamoja ili tuitafakari hiyo *alternative* anayoizungumzia ili wananchi wasiendelee kupata matatizo katika maeneo aliyoyazungumza.

Na. 169

Tatizo la Ugonjwa wa Malaria

MHE. RIZIKI OMAR JUMA (K.n.y. MHE. ANIA S. CHAUREMBO) aliuliza:-

Kwa kuwa, bado kuna tatizo la vifo vinavyotokana na ugonjwa wa malaria nchini; na kwa kuwa, Serikali ikishirikiana na Mataifa mbalimbali imewe ka mikakati kadhaa ya kulimaliza tatizo hilo:-

- Je, vifo vinavyotokana na ugonjwa huo vimepungua kwa kiasi gani?
- Je, Serikali ina mikakati gani ya ziada ya kuliondoa tatizo hilo kwa Wilaya zilizoathirika zaidi na ugonjwa huo?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa malaria kwa miaka mingi umeendelea kuchangia kwa vifo vya wananchi wengi wa Tanzania hasa kina mama wajawazito na watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

Kwa mujibu wa Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji wa Huduma za afya (MTUHA), takwimu zinaonyesha kuwa ugonjwa wa malaria unaongoza kwa mahudhurio ya wagonjwa wa malaria wanaolazwa.

Malaria huchangia asilimia 40 ya vifo vya watoto. Kwa mujibu wa takwimu zilizopo zinaonyesha kupungua kwa vifo vya watoto, hii inawezekana kuwa ni sababu nyingi zinazochangia hivyo, lakini inatufanya tusadiki kuwa kupungua kwa malaria kumechangia katika kupunguza idadi ya vifo. Kwa mfano:-

Vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano vimepungua kutoka vifo 191 kwa watoto 1000 mwaka 1990 hadi vifo 133 kwa watoto 1000 mwaka 2005; wakati vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka 115 kwa watoto 1000 mwaka 1990 hadi vifo 68 kwa watoto 1000 mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa mchakato wa kutafiti hali halisi ya maambukizi ya malaria na vifo vinavyotokana na ugonjwa huo kwa mwaka ujao na hapo tutapata mwelekeo (*trend*) ya ugonjwa huo.

(b) Serikali itaendelea na jitihada za kupambana na ugonjwa wa malaria nchini na hasa katika Wilaya zilizoathirika zaidi kwa kutekeleza Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Malaria kama ifuatavyo:-

1. Suala la elimu limepewa kipaumbele ambapo makundi yote wajue afua zote zinazoendelea. Tunasisitiza kwamba mtoto anapopata homa afikishwe kwenye kituo ndani ya masaa manane.
2. Tunahamasisha jamii kuhusu usafi wa mazingira ili kuangamiza maficho na mazalio ya mbu.
3. Kupulizia dawa ya ukoko yenyе viuatilifu ndani ya kuta na dari za nyumba, hususan katika maeneo yanayopata milipuko.
4. Kutumia vyandarua vyenyе viuatilifu.
5. Kusisitiza matumizi ya tiba sahihi ya malaria katika vituo vyote vya kutoleaa huduma ya afya.
6. Kutoa tiba ya tahadhari kwa kina mama wakati wa kipindi cha ujauzito.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la mpango huu ni kupunguza madhara na vifo dhidi ya malaria kwa jamii ikijumuisha makundi hayo mawili ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano na akinamama wajawazito.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, naomba niulize masuala mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika mikakati aliyoitaja Mheshimiwa Waziri inatupa matumaini. Lakini kwa kuwa vituo vingi ambavyo wanafikishwa mama wajawazito na watoto pengine kunakuwa na ukosefu mkubwa wa huduma za haraka haraka za kuwatibu malaria akina mama wajawazito na watoto wachanga. (*Makofî*)

Je, Serikali inaonaje ingeboresha zaidi kuhakikisha kunapatikana madawa katika vituo na zahanati ambazo akinamama wale hufikia mapema kabla hatua haijakuwa kubwa ya matatizo?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa sababu huko nyuma kulikuwa na utaratibu wa mama wajawazito kupewa kinga ya malaria yaani wanapokuwa wajawazito, kwa sababu inaonekana kwamba watoto wengine wanapozaliwa tayari wanakuwa wanayo malaria.

Je, Mheshimiwa Waziri anaonaje kwamba Serikali ingerejesha ule utaratibu wa kuwapa kinga akinamama wajawazito kabla ya kufikia hali mbaya hiyo?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, nikianza na la pili katika afua nilizozitaja ndani ya mkakati wetu nimetaja kwamba tunatoa dawa kwa akinamama wakati wa ujauzito hili ni zoezi ambalo linaendelea na tunalisimamia kikamilifu.

Kuhusu upatikanaji wa dawa hili linashabiiiana na swali ambalo limejibiwa hivi punde na Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI jinsi tulivyojipanga katika kuhakikisha kwamba dawa zinapatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tunaondokana na utaratibu wa kutoa *kits* kwa kila kituo na sasa hivi tumeingia katika *intergrated logistics system* ambapo Mkuu wa hicho Kituo anaagiza madawa kufuatana na mahitaji.

Kipindi cha malaria anaona atapunguza mahitaji ya dawa basi atapunguza mahitaji, lakini nia ni kwamba dawa zifike kwa wakati na ziwepo katika vituo wakati wote.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa baadhi ya watu wenye kutumia dawa za mseto za *ALU* huwa wanapata madhara kama kuvimba mwili na wengine wanaota mapunye hata kuweza kufariki. Je, Serikali inatueleza nini kwa wale ambao wanapata madhara ya dawa hizi watumie dawa gani mbadala?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, tunapoanza kutumia dawa mpya tuna utaratibu wa kufuatilia madhara yanayoweza yakatokana na dawa hizo.

Tunatoa fomu maalum ni rangi ya njano ambazo mtumiaji pamoja na daktari wanajaza na kuileta katika kituo chetu cha *TFDA*. Hivyo tunayakusanya na kuangalia ni watu wangapi walilalamika na kama ipo haja tunaziondoa hizo dawa katika soko.

Sasa kama kuna mtu wa namna hiyo ambaye amepata huko kuvimba mwili tunashauri kwamba watuletee taarifa.

Lakini tujue kwamba *ALU* ni dawa mseto kuna dawa mbili. Upo uwezekano wa kutafuta ni kiini kipi ambacho kimeleta madhara na kuibadilisha katika dawa nyingine. Hapa siwezi kutamka utumie dawa gani kwa sababu ziko nyingi, lakini akimwona daktari anaweza akamshauri viliyvo.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nina swalii moja tu la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwamba dawa ziko nyingi. Mimi naomba mtusaidie kwa sababu kuna *ALU* kuna mseto, kuna *fansider*, kuna *chloroquine*. Nini msimamo wa Serikali katika kupambana na Malaria na ni dawa ipi ambayo itatufaa ili kuondoa usumbufu na kuondoa *side effect* ambazo zinawapata wagonjwa wa Malaria?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, tulipoanzisha dawa ya *ALU* ni kwa sababu dawa hizo nyingine alizozitaja zilionyeshwa usugu kwa vimelea vya Malaria. Kwa hiyo tumeondokana na *chloroquine* na *fansider* na dawa nyingine alizozitaja tunatumia *ALU*. *ALU* ndiyo tunaita *first line treatment*. Kwa hiyo, tuna sisitiza kwamba watu wote watumie *ALU*.

Na. 170

Utafiti wa Chanjo ya Ugonjwa wa Malaria

MHE. GEORGE M. LUBELEJE aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilikuwa na mpango wa kufanya utafiti wa dawa ya chanjo ya ugonjwa wa malaria; na kwa kuwa, malaria ni ugonjwa unaongoza kwa kuua watu wengi hapa nchini:-

Je, Serikali ina maelezo gani kuhusu utafiti huo muhimu wa chanjo ya malaria?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utafiti wa chanjo ya malaria unafanywa na Taasisi zetu mbili ambazo ni Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu Tanga (*NIMR*) na Kituo cha Maendeleo ya Utafiti wa Magonjwa cha Ifakara. Utafiti huu unalenga kupata chanjo ya kuzuia vijidudu vya malaria visiweze kuishi na kuzaliana mwilini na hivyo kusababisha aliyechanjwa asipate ugonjwa malaria.

Mheshimiwa Spika, kituo cha Tanga kinafanya utafiti huo katika Hospitali ya Korogwe ambako Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (*NIMR*) imejenga maabara ya kisasa na kituo cha Ifakara kinafanya utafiti huu katika hospitali ya Bagamoyo ambako pia kuna maabara ya utafiti.

Mheshimiwa Spika, chanjo hizi za majaribio ni za aina mbili tofauti na zinatolewa kwa watoto chini ya mwaka mmoja katika maeneo yanayozunguka vituo vya utafiti na waliochanjwa wanafuatiiliwa kwa karibu. Majaribio haya yako kwenye awamu ya pili, yaani kuangalia usalama wa chanjo na uwezo wa chanjo ku “*stimulate*” viini vya kuzuia kupata na ugonjwa wa malaria kwa watu waliochanjwa.

Ni matarajio yetu kuwa matokeo ya awali ya utafiti huu yatatolewa mwezi Oktoba 2008.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, kwanza kabla sijauliza swal la nyongeza naomba katika kuweka kumbukumbu sawa mimi naitwa Lubeleje sio Mabeleje. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swal la nyingeza. Kwanza kwa kuwa zahanati zetu nyingi hazina Maabara na huwezi kumtambua mgonjwa wa Malaria kwa kumuangalia tu. Lazima uchunguzi ufanyike kwenye maabara unachukua damu unacheki kama kuna *Malaria parasite*.

Sasa je, Mheshimiwa Waziri analambia nini Bunge hili ni lini tutaimarisha Vituo vyetu hasa Zahanati kwa kuimarisha maabara na kuweka darubini kwa ajili ya kuchunguza magonjwa hayo?

Swali la pili, kwa kuwa watoto wachanga hawawezi kumeza vidonge na kwa kuwa *Chloroquine* ilikuwa na *syrup* na sindano hii dawa ya mseto ya *ALU* kuna sindano na *syrup* kwa ajili ya watoto wachanga?

SPIKA: Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri kujibu jina hilo Lubeleje asili yake ni unyamwezi. Sasa inapotamkwa Mabeleje ni wingi wa Lubeleje na kwa lugha yetu ile ya asili hiyo ni heshima zaidi kuliko umoja. (*Kicheko*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniokoa na mimi nilimwita Mabeleje kwa kumpa heshima ya ziada na mimi nilisoma Tabora. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swal la Mheshimiwa Lubeleje kama ifuatavyo:-

Swali lake la kuimarisha maabara ni kwamba limo katika mpango mzima wa MAM. Lakini vilevile nitamke kwamba sasa hivi tuna *introduce rapid test* ambazo hazitahitaji maabara. Hizo *test* zipo nchini na zinafanyiwa majaribio na pia kuwafundisha watu wetu waweze kuzitumia. Dawa ya *ALU* tulioizungumza hivi punde ni dawa ghali sana. Tofauti ni *chloroquine* ambayo mtu unaweza ukahisi na ukampa dawa kwa kuhisi zile ziliwa hazina gharama kubwa.

Lakini dawa ya *ALU* kwa dozi nzima ni karibu dola 10 za Kimarekani. Kwa hiyo hilo tumeliona na tuna *introduce rapid test* ambazo unachukua tone la damu na unaweza ukajua kwamba huyu ana Malaria au hana.

Swali lake la pili ni kwamba napenda kumuarifu Mheshimiwa Lubeleje kwamba *syrup* ya *ALU* ipo.

Na. 171

Kilimo cha Umwagiliaji –Sumbawanga

MHE. LUDOVICK MWANANZILA aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Sumbawanga ni moja kati ya Wilaya zinazotoa chakula kingi nchini hasa katika Jimbo la Kalambo; na kwa kuwa, Jimbo hilo limekuwa halipati huduma za Serikali za Umwagiliaji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika vijiji vya Singiwe na Kasanga.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa ni maarufu sana kwa uzalishaji wa nafaka hususan mahindi kiasi cha kuwekwa katika kundi la *big four* yaani Mikoa ya Rukwa, Ruvuma, Iringa na Mbeya. Serikali inatambua hilo ndiyo maana inaelekeza rasilimali zake hasa pambejeo za kilimo na miradi ya umwagiliaji katika Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, mpango Kabambe wa kilimo cha Umwagiliaji maji Mashariki *National Irrigation Master Plan (NIMP)*, 2002 ulibaini hekta 47,672 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa wa Rukwa.

Serikali inaendelea kuendeleza miradi ya umwagiliaji katika Mkoa wa Rukwa kwa kufuata *NIMP* na kwa kufuata utaratibu wa kuibua miradi kutoka katika Halmashauri za Wilaya pamoja na Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa sasa ni kwamba mipango ya kuendeleza miradi ya umwagiliaji inaanzia katika kijiji husika na kupitishwa katika Mipango ya Maendeleo ya Wilaya (*DADSP*). Miradi inapobainika kuhitaji fedha zaidi ya shilingi milioni 200 inaombewa fedha kutoka katika mfuko wa *DIDF* na inapozidi milioni 500 mradi unaombewa kutoka katika Mfuko wa *NIDF*. Mifuko hii ni sehemu ya Programu ya kuendeleza sekta ya kilimo *ASDP*.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umwagiliaji wa Msanzi alioutaja Mheshimiwa Mbunge uliboreshwaa na Programu ya maendeleo ya Rukwa (*Rukwa Development Program -RUDEP*) kwa msaada wa *NORAD*. Hata hivyo wananchi waliamua kutumia eneo la mradi kujenga Shule ya Msingi; lakini taarifa tuliyonayo ni kwamba hivi sasa wananchi wameibua tena upya skimu hiyo. Serikali itautazama upya mradi huo ili kuona namna ya kuuendeleza.

Aidha mradi huu pamoja na mradi wa Kasanga Wataalam wa Umwagiliaji wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) wamekwishaikagua na kuisaidia Halmashauri ya Wilaya kuandaa maandiko na makisio ili miradi hiyo ifanyiwe maombi ya fedha kutoka katika *basket fund* ya *ASDP* kupitia *DADPS*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa Singiwe, timu ya wahandisi wa umwagiliaji imekwishakamilika usanifu wa mradi na umeombewa fedha za utekelezaji katika mwaka 2008/2009. Miradi mingine katika Mkoa wa Rukwa ni pamoja na Urwira ambao unaendelea kutekelezwa.

MHE. LUDOVICK MWANANZILA: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba mradi wa Singiwe umeshachunguzwa na utanza hivi karibuni.

Lakini kwa kuwa Mkoa wa Rukwa haujawa na rekodi nzuri ya utekelezaji wa miradi hii ya umwagiliaji; mwaka 2003 mradi na Urwira na Katuka ulipewa fedha kwa ajili kutekelezwa. Mradi wa Urwira upo katika Jimbo la Mpanda Mashariki ambalo ni

Jimbo la Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mradi wa Katuka upo katika Jimbo langu la Kalambo. Miradi hii imetelekezwa na haifanyi kazi kama tulivyotarajia.

Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha mradi wa Urwira na Mradi wa Katuka unakamilika na ufanye kazi kuwanufaisha wananchi katika majimbo haya mawili.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, si busara kwa Serikali kuhakikisha kwamba miradi ile ambayo imeanzishwa inakamilishwa kwanza kabla ya kuanza miradi mipya? Kwa sababu miradi hii ya Urwira na Katuka ilianza mwaka 2003 imeachwa haijaweza kufanya kazi inavyotarajiwa.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, mimi sidhani kama Mkoo wa Rukwa una rekodi mbaya kupita Mikoa mingine yote. Utekelezaji katika Mikoa mingi unafanana kutokana na matatizo tuliyonayo na hasa ya fedha. Lakini nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mwananzila nikianza na lile kwamba ni kweli ipo haja na ndivyo tunavyofanya hivi sasa kwamba tukamilishe viporo kwanza kabla hatujaingiza miradi mipya. Hata mwaka huu tutakapokuwa tuna *present* miradi yetu na Bajeti yetu utaona kwamba miradi viporo ambayo haijakamilika ndiyo imepewa kipaumbele. Kwa hiyo, nakubaliana nalo kabisa.

Kuhusu swali la kwanza la Miradi ya Urwira na Katuka, mimi napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mwananzila kwamba tayari tumeshachukua hatua na yeze mwenyewe alikuja akaniona na mimi nikaangalia kwamba maombi yake ni ya msingi.

Sasa mradi wa Katuka wenyе hekta 250 ni kwamba tayari Wataalam wameshafanya utafiti na wapi lijengwe Bwawa. Kwa sababu mradi ule ulipojengwa kilichojoitokeza ni kwamba uharibufu wa mazingira ulikuwa mkubwa zaidi kwa kiangazi maji hakuna. Kwa hiyo tutawajengea Bwawa kwa ajili ya kuongeza maji. Mradi wa Urwira huu mradi unaendelea na si kweli kwamba tumetelekeza. Hivi ninavyozungumza mradi huu wa Urwira umepelekewa shilingi milioni 78.6 kwa ajili ya kuendelea kuutekeleza.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ilikuwa imejipanga kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji na tukaambiya kuna fedha; na pia sasa hivi Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kuna ukata kati ya kuwa na fedha na ukata mimi sijui tusimamie wapi. Lakini katika jibu lake amesema Mkoo wa Rukwa una hekta 42,000 ambazo zinatafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Yapo Mabonde ya Rufiji na Kilombelo, hivi kweli kama taifa hatuoni aibu kuendelea kutafuta chakula badala ya kujiendeleza wenyewe na kilimo cha umwagiliaji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza katika *National Irrigation Master Plan* Mkoo wa Rukwa tumesema tumbaini 47,000 na zaidi kidogo sio 42 na hizo ni zile tu za awali bado kuna uwezekano mkubwa kwa sababu kuna vyanzo vingi vya maji.

Lakini niseme kwamba habari ya ukata wa kuendeleza miradi haijatuia kuendeleza miradi kwa kipaumbele. Hivi tunavyozungumza tayari Serikali imepeleka bilioni 7 katika Halmashauri 30 kwa ajili ya kuendeleza miradi ya umwagiliaji. Kwa hiyo kila inapokuja kwa kipaumbele kutoka kwenye Halmashauri sisi tunatekeleza kwa fedha zinazopatikana.

Na. 172

Kufikisha Umeme Wilayani Ifikapo Mwaka 2010

MHE. VITA RASHID KAWAWA aliuliza:-

Kwa kuwa ni sera ya Serikali ya CCM kwenye ilani yake ya uchaguzi ya mwaka 2005 kufikisha umeme wa uhakika kwenye Wilaya zote ifikapo mwaka 2010; na kwa kuwa zipo Wilaya kama vile Namtumbo ambazo zipo kwenye mpango wa kupatiwa umeme lakini mpaka sasa huduma hiyo haijatolewa:-

Je, wakati tukisubiri umeme wa Grid ya Taifa amba tunaona shaka kuwa utachelewa; je, Serikali inaweza kutupatia jenereta moja kati ya zile zilizokuwa zinatoa huduma kwenye Mikoa ya Lindi na Mtwara?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina nia ya kusambaza umeme kwa wananchi wengi zaidi ili kuongeza kasi ya maendeleo kwa kutumia nishati hii muhimu na hivyo kuchochea maendeleo na ukuaji wa uchumi kwa wananchi waishio vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kusambaza umeme kwenye miji 16 ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya ambayo bado haina umeme. Utekelezaji wa miradi ya kuzipatia umeme Wilaya zote hizo ni kazi kubwa na unahitaji fedha nyingi. Kutokana na uwezo mdogo wa Serikali kifedha kuweza kutekeleza miradi yote kwa pamoja, Serikali imelazimika kuomba misaada kutoka kwa washirika wetu wa maendeleo pamoja na kukopa kutoka kwenye taasisi za fedha za kimataifa kuharakisha upelekaji wa umeme katika miji hiyo. Ni mategemeo ya Serikali kwamba miji ya Makao Makuu ya Wilaya zilizobakia zitapatiwa umeme kipindi kifupi kijacho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali na Kampuni ya *Artumas* kusaini mkataba wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia ya *Mnazi Bay* kwa ajili ya Mikoa ya Lindi na Mtwara, jukumu la kuzalisha umeme kwa ajili ya Mikoa hiyo halitakuwa tena mikononi mwa Shirika la Umeme la *TANESCO*.

Hivyo basi mitambo iliyokuwa ikizalisha umeme kwenye Mikoa ya Mtwara na Lindi imeshapangwa kupelekwa kwenye miji mingine isiyokuwa na huduma ya umeme. Vilevile mitambo ya kuzalisha umeme kwenye vituo vya uzalishaji umeme vya TANESCO katika miji ambayo imepatiwa umeme wa gridi itahamishwa na kupelekwa kwenye miji ambayo haijaunganishwa kwenye gridi ya taifa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utaratibu huo mitambo mitatu ya Mtwara itapelekwa Biharamulo, Ngara na Songea. Mitambo miwili iliyotoka Lindi itahamishiwa Tunduru na Kilwa. Maandalizi kwa ajili ya kazi ya kufungua, kusafirisha na kufunga mitambo hiyo kwenye maeneo niliyoyataja imekwishaanza na itakamilika Agosti 2009.

Sababu za kupeleka jenereta katika maeneo hayo ni pamoja na kuwa na wateja ambao wanapata huduma ya umeme hafifu hivyo ni busara kuboresha upatikanaji wa umeme katika miji hiyo. Vilevile njia ya umeme ya msongo wa KV 132 itokayo Makambako kwenda Songea ikikamilika Mji wa Namtumbo uitaunganishwa kwenye gridi ya taifa. Mji wa Kilwa umepewa kipaumbele kwa kuwa jenereta inayotumika katika mji huo iko katika hali mbaya.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali uliopo wa sasa ni kuupatia Mji wa Namtumbo umeme wa gridi kwa kujenga njia ya umeme itakayounganishwa na njia ya umeme ya Makambako hadi Songea.

MHE. VITA RASHID KAWAWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba pia niishukuru Serikali kwa kuupatia Mji wa Songea jenereta ambayo itaongezea nguvu majenerata yaliyopo. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2008/2009 Serikali imetenga bilioni 3.862 katika mradi wa KV 132 Makambako Songea mpaka Namtumbo; na kwa kuwa mradi huu unakisiwa utaghalimu bilioni 70 kwenda mpaka Jimbo la Namtumbo, Jimbo la Peramiho na Jimbo la Mbinga. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwa mpango huu wa mradi wa bilioni 70, Serikali kutenga bilioni 3.8 haioni itachukua takribani miaka 20 kukamilisha mradi huu?

Swali la pili, kwa kuwa tumekuwa tukiahidiwa mwaka hadi mwaka wananchi wa Namtumbo na kuishi kwa matumaini na wananchi wamejandaa kwa kutandaza nyaya za umeme katika nyumba na ofisi zao, Je, Naibu Waziri atakubaliana nami kuwa katika hali hii ya kusubiri miaka 20 hadi umeme wa *grid* ufile nyumba hizo hazitakuwa zimebomoka na kwa kutekeleza ahadi ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi je, Serikali haioni sasa hivi ni wakati muafaka Namtumbo tukapata umeme wa jenereta?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, Mji wa Namtumbo unatarajiwa upate umeme kutokana na mradi wa KV 132 ambao utatoka Makambako kwenda Songea. Lengo la mradi hii ni kutoa umeme wa grid na hivyo basi upembusi yakinifu wa mradi huo umeshakamilika na Serikali imeongea na Serikali ya Sweden na tayari maombi ya fedha yameshawasilishwa na tayari majadiliano ya awali

yameshafanywa na Serikali ya Sweden imeridhia kufadhili mradi huo isipokuwa tunasubiri taratibu zianze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, hizi bilioni 3.862 ambazo zimetengwa ni mchango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwenye mradi huo. Kwa sababu mradi wenyewe utagharimu zaidi ya shilingi bilioni 70.

Sasa sisi wenyewe tumetenga bilioni 3.862 ambazo kazi zake kusema kweli ni kwa ajili ya kutandaza umeme kwenye Miji hiyo ya Songea, Namtumbo, Ludewa na Mbanga ikisubiri umeme huu mkubwa uje kutoka Makambako. Kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu hautachukua miaka 20 na hivyo natarajia kwamba mradi huo utafika Namtumbo kabla ya nyumba hazijaanguka.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na ambayo hayajatosheleza kiu ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma katika kupatiwa umeme ninaomba niwaulize swali jingine dogo la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la kupeleka umeme lilitokana na umeme kutokutosheleza katika Mji wa Songea na kwa kadili ya majibu ya Mheshimiwa Waziri anapeleka majenerata ya kuongeza nguvu pale Songea. Je, sasa hivi Wizara ipo tayari kupeleka umeme Peramiho kwa kuwa nguvu ya umeme itakuwa imeongezeka kwa kiasi kikubwa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mhagama kwa kufuatilia suala hili la Peramiho na tumeshaongea naye mara mbili tatu ofisini Wizarani kuhusiana na mradi huu. Ni matarajio yetu kwamba kwa sasa hivi umeme wa Peramiho unatokana na wa Halmashauri ya Mji wa Songea.

Tumeongea na Mheshimiwa Mhagama na Wizara inafanya tathimini kwa kushirikiana na TANESCO kwamba umeme ule unaotoka Songea kwa kuwa tathimini ambayo tunatarajia itaboreshwa baada ya kwisha kufanya haitakuwa ya gharama kubwa. Tunatarajia kwamba mradi huu wa kufikisha umeme Peramiho kutoka Songea Mjini na ni matarajio kwamba kwa kuweka jenereta hii ya ziada pale Songea Mjini umeme wa ziada utapatikana ambaa utakidhi pia mahitaji ya kupeleka umeme Peramiho.

Na. 173

Mahitaji ya Umeme wa Grid – Vijiji vya Jimbo la Nyang’hwale

MHE. JAMES P. MUSALIKA aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la wananchi wa kijiji cha Kharumwa, na vile vya Ikangala, Kitongo, Nyarubele, Kakora na Nyamtukuza Jimboni Nyang’hwale ni la kuunganishiwa

umeme wa grid (*TANESCO*) ambao nyaya zake zimepita kwenye vijiji hivyo muda mrefu sana; na kwa kuwa Serikali imeshafanya tathimini ya gharama ya kazi hiyo na pia imekuwa ikiahidi kutekeleza mradi huo kwa mwaka 2007/2008.

Je, Serikali imefikia hatua gani ya utekelezaji wa mradi huo?

NAIBU WAZIRI WA NISHARI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa James Philipo Musalika kwa jinsi anavyofuatilia mambo yanayolenga kuwaletaa maendeleo wapiga kura wake. Mheshimiwa James Musalika alishawahi kuuliza swal namba 56 lililojibiwa tarehe 5 Februari 2007 na swal namba 43 lililojibiwa tarehe 19 Juni 2007 yote yakahusika hitaji la umeme kijiji cha Kharumwa.

Katika swal namba 56 Serikali iliahidi kutuma wataalam kwenda kufanya upembuzi yakinifu ili kupata namba bora ya kutekeleza mradi wa kupeleka umeme katika maeneo aliyyataja Mheshimiwa Mbunge pamoja na gharama zake.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujibu swal namba 43 la Mheshimiwa Mbunge ilielezwa kuwa Aprili 2007 *TANESCO* walitekeleza agizo la Serikali kwa kufanya upembuzi yakinifu.

Tathimini hiyo ilionyesha kuwa vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge wa Kharumwa, Ikangala, Kitongo, Nyarubele, Kakola na Nyamtukuza vinaweza kupatiwa umeme kutoka kituo cha pampu za maji Ihelele au Bulyanhulu.

Mheshimiwa Spika, gharama za kuunganisha umeme kutoka kituo cha pampu za maji Ihelele hadi Kharumwa ni shilingi milioni 90 na hadi Nyamtukuza ni shilingi milioni 35. Tathmini ya kufahamu gharama za upelekaji umeme katika vijiji vya Ikangala, Kitongo, Nyarubele na Kakola inakamilishwa. Kutoa umeme Bulyanhulu ni shilingi milioni 600 na kazi zinajumuisha ujenzi wa njia mpya ya umeme ya msongo wa KV 33 yenye urefu wa kilomita 50.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu wa fedha mradi huo haukutekelezw na uliingizwa kwenye orodha ya miradi ambayo utekelezaji wake ungekuwa chini ya miradi ya umeme vijijini kuititia *Access Expansion Programm (AEP)*.

Baada ya mpango huo kushindikana mradi wa kupeleka umeme kwenye vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge kwa sasa utafadhiliwa na Wakala wa Umeme Vijiji (REA)

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa ajili ya kuunganisha umeme kutoka Ihelele hadi Kharumwa yameshawasilishwa Serikalini kupitia REA. Vijiji ambavyo havijafanyiwa tathmini mara tu ghamama zikishafahamika maombi yatawasilishwa Serikalini kupitia REA.

Kazi za utekelezaji wa mradi zitaanza iwapo kibali cha kuunganisha umeme kwenye kituo cha Ihelele kitatolewa na Wizara ya Maji. Ili mradi huu uweze kutekelezwa Wizara ya Nishati na Madini itawasiliana na Wazara ya Maji na Umwagiliaji ili kuona uwezekano wa kupata kibali cha kuunganisha umeme kutoka kwenye kituo chao cha umeme cha Ihelele.

Mheshimiwa Spika, iwapo fedha za utekelezaji mradi zitapatikana, mradi unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 3 kwa kutoa umeme Ihelele na mwaka mmoja kwa kuunganisha umeme Bulyanhulu.

SPIKA: Nakupongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutamka kwa lafudhi ya Kisukuma ile ya Bulyanhulu. Mheshimiwa Msalika Swali la nyongeza.

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa sasa hivi ni takribani miaka kumi mimi nauliza maswali mbalimbali kwa niaba ya nchi ya Nyang'hwale hususan pale Kalumwa kuhusu maombi yao ya umeme; na kwa kuwa kijiji cha Kalumwa kimezingirwa na nyaya za umeme zinazotoka ibadakule kwenda mgodoni na kutoka mgodini kwenda kwenye chanzo cha maji pale Ihelele; na pia wananchi nao walinisaidia mwaka jana kwa njia wanazozijua wao na wakaiambia Serikali kwa njia ya maandamano kuomba huo huo umeme.

Je, Serikali inanishauri nini mimi na wananchi wangu baada ya njia zote hizi kushindikana tutumie njia gani sasa kuomba huo umeme.

Swali la pili. Je, Waziri wa Nishati na Madini yupo tayari mwezi wa tisa baada ya kumaliza Bunge hili aje pale pale Kalumwa aongee au awaambie wananchi hao yeye mwenyewe kuwaambia wananchi wa pale kuhusu tatizo hili. Inawezekana kwa sababu mimi hawaniamini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Naona Mheshimiwa amebanwa koo na wapiga kura.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba rekodi zote zinaonyesha Mheshimiwa Musalika amekuwa akiuliza swali hili Bungeni kama nilivyokiri, kwa muda mrefu, na Serikali imekuwa ikifanya taratibu za kufanya tathmini na hatua za awali kama tulivyoahidi mwaka jana, wataalamu wa *TANESCO* wamekwenda na wameufanya tathmini mradi huu.

Mheshimiwa Spika, uwepesi wa kufanya mradi huu kusema kweli ni kutoa umeme kutoka pampu za maji za Iherere. Lakini Mradi wa kutoka Iherere, waliougharamia ni Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Kwa hiyo, wao ndio wenye miliki na mradi huu.

Sasa sisi upande wa Wizara ya Nishati na Madini kama nilivyomwahidi, tuko kwenye mazungumzo nao kwa sababu vinginevyo, kuutoa kutoa Bulyanhulu ni milioni 600 na fedha zenyewe ndio kama hivyo. Lakini tayari tumeishawasiliana na Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*), tunawasiliana na Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba mwezi wa Tisa nadhani Waziri wangu ataridhia kwenda naye huko Jimboni na ni matarajio yangu kwamba hata utakapofika huo mwezi wa Tisa, wakati huo tayari tutakuwa tumeishafikia hatua nzuri tu katika utekelezaji wa mradi huo.

Na. 174

Upatikanaji wa Mitaji kwa Wajasiriamali

MHE. BAKARI SHAMIS FAKI aliuliza:-

Kwa kuwa pamoa na mifuko mbalimbali ambayo imeanzishwa, upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo na wa kati bado ni tatizo:-

Je, ni vikundi vingapi vya wajasiriamali vimepatiwa mitaji yenye thamani ya kiasi gani kwa kipindi cha mwaka 2006?

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilipewa jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji mpango wa uwezeshaji kwa wananchi kuondoa umaskini na jumla ya shilingi bilioni 21 ikiwa ni wastani wa shilingi bilioni moja (1) kwa kila mkoa katika kipindi cha 2006/2007. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara yangu kwa kushirikiana na iliyokuwa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwekezaji na Wizara ya Fedha ilifanikiwa kuanzisha mpango wa utoaji mikopo kwa wajasiriamali nchini kupitia Benki na Asasi ndogo ndogo za fedha.

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango huu jumla ya wajasiriamali 44,252, kupitia *SACCOS* na vikundi walipata mikopo kama mtaji kupitia benki za *CRDB* na *NMB*. Kiasi kilichotolewa kwa wajasiriamali hao ilikuwa shilingi 32,686,713,000/=.

Aidha awamu ya pili imeshaanza mwezi Desemba, 2007 hivyo tunategemea wajasiriamli wengi zaidi watapata mitaji kupitia *SACCOS* zao na hasa Wilaya ambazo katika awamu ya kwanza hawakupata kabisa.

MHE. BAKARI SHAMIS FAKI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Moja, kwa kuwa pamoja na juhudzi zinazochukuliwa, bado yapo malalamiko kuhusiana na mikopo hii. Je, Serikali inayo mikakati gani ya kuondokana na malalamiko hayo?

Pili, kwa kuwa kwenye majibu yake ya msingi, Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba ziko baadhi ya Wilaya zilikosa mikopo hii; Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea Wilaya hizo kukosa mikopo hiyo? Ahsante sana!

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna malalamiko. Kuna mkakati gani wa kuyaondoa haya, ni kwamba hivi sasa tunafanya tathmini ili tuweze kupata msingi na uenezi wa malalamiko haya na baadaye kupendekeza au kuchukua hatua zinazostahili.

Wilaya gani zilizokosa, sababu za msingi ziliwu; pamoja na majukumu ya ukopeshaji ambayo benki hizi zilipewa, ni kwamba ilibidi benki hizi vile vile zizingatie taratibu za kibenki. Kwa sababu, kwa mfano kama *NMB* ilikuwa haiwezi kukopesha nje ya kilomita 20 kutoka makao makuu ya benki hiyo.

Sasa, katika awamu ya pili, tumejaribu kusahihisha makosa hayo kwa kuweza kuweka na Taasisi zingine za kifedha ili kuhakikisha kwamba hizo Wilaya ambazo hazikuweza kufikiwa, ambazo hazina matawi ya benki ya *NMB* ili ziweze kufikiwa. Vile vile kama *CRDB*, utakuta mara nyingi iko katika Mikoa tu.

Sasa vile vile ndiyo maana tumeongeza Taasisi za kifedha ili kuweza kuhakikisha kwamba Wilaya zote zinaenea. Lakini, hata hivyo, pamoja na kwamba zilikosa katika awamu ya kwanza, katika awamu ya pili, Wilaya hizo tumehakikisha zinapata mgawo sawa kama Wilaya ambazo zilikuwa zimepata katika awamu ya kwanza.

Na. 175

Mpango wa Mfuko wa Uwezeshaji Kutowafikia Walengwa

MHE. JUMA H. KILLIMBAH aliuliza:-

SPIKA: Kwa kuzingatia muda Waheshimiwa, tumalize tu swali la mwisho sasa ambalo linaelekezwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Samahani, sikutoa taarifa kwamba Mheshimiwa Killimbah swali namba 175 ameliondoa kwa sababu amekwishapata majibu na limepitwa na wakati. Kwa hiyo, la mwisho sasa ni lile linaloulizwa na Mheshimiwa Dr. Festus Limbu wa Magu. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Rished Abdallah - uliza swali hilo kwa niaba yake.

Na. 176

Wimbo wa Taifa Kupigwa kwenye shughuli za Wananchi

MHE. RISHED ABDALLAH (K.n.y. MHE. DR. FESTUS B. LIMBU) aliuliza:-

Kwa kuwa, Bunge limepitisha Kanuni kuanza na kufungua mikutano kwa kupigwa wimbo wa Taifa ili kukuza uzalendo:-

Je, kwa nini isitungwe Sheria ili iwe lazima kwa shughuli zote zinazokusanya wananchi kama vile mikutano ya Kitaifa na Kimataifa, miziki ya dansi, taarabu na shughuli zinazofanyika kwenye Balozi n.k. yote ianze rasmi kwa kupigwa wimbo wa Taifa?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili Serikali au nchi yoyote hapa duniani iweze kutambulika ni lazima iwe na alama mbali mbali kama vile Bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa na Nembo ya Taifa. Hapa kwetu Tanzania alama hizi hutumika katika maeneo maalum, shughuli maalum na wakati maalum.

Mheshimiwa Spika, juu ya kwa nini isitungwe sheria ili iwe lazima kwa shughuli zote zinazokusanya wananchi kwa mifano aliyoitoa Mheshimiwa Mbunge. Jambo hili litawezekana tu pale ambapo itaonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo kwa kuzingatia taratibu na Kanuni za kitafiti za nchi ilivyojiwekea yenyewe. Kwa misingi hiyo jambo hili linahitaji utafiti wa kina hasa ikizingatiwa kuwa mikusanyiko ya kitaifa na kimataifa ya wananchi ukiachia mifano michache ya shughuli alizozitaja Mheshimiwa Mbunge ambazo zinafanyika kila wakati na katika maeneo mbalimbali. Aidha, utafiti huo utasaidia kubaini kwamba unaondoa, unapunguza au unaongeza uzalendo na heshima inayostahili kwa alama zetu za Taifa.

SPIKA: Ahsante Waheshimiwa, Maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita kidogo. Sasa ninayo matangazo. Nitaanza na Wageni. Nilipomtambulisha Mheshimiwa Dr. William Shija, Katibu wetu Mkuu wa Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola, sikutamka kwamba yupo pia Mkewe, Bibi Getrude Shija, naomba asimame, ingawa alisimama wakati ule. Naomba pia mtoto wao Anna Shija aweze kusimama tumtambue. Ahsante sana. Wapo pia waliofuatana na Mheshimiwa Dr. Shija katika Msafara huo. Mmoja nadhani kutoka Uingereza, Msaidizi wake. Huyo hapo. Sikupewa jina kwa bahati mbaya sielewi kama ni Mtanzania au ni mgeni. Ian Maccintosh, ndiyo yule! Alah! Ahsante sana! *Welcome Mr. Ian Maccintosh. Such names are usually associated with other colours, but, thanks very much, thank you!*

Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ana wageni wanaokuja kumsadia kwa shughuli leo. Yupo Bwana Arthur Mwakapugi, Katibu Mkuu wa Wizara, yuko Bwana Bashir Mlindoko, Kamishina wa Nishati, Dr. Peter Dalali Kafumu, Kamishna wa Madini, yule pale, ahsante. Kutoka Shirika la Umeme, *TANESCO* yupo Mheshimiwa Balozi Fulgence Kazaura, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Bwana William Mhando, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa *TANESCO*.

Kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli, yupo Generali Mstaafu Robert Mboma, Mwenyekiti wa Bodi ya *TPDC*, yule pale, karibu sana *General*. Yupo Bwana Yona Kiragane, Mkurugenzi Mtendaji wa *TPDC*. Kutoka Wakala wa Umeme Vijijini (*REA*) hiyo inayotamkwa mara kwa mara hapa, yuko Bwana Singi Madata, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya *REA* na DR. Lutengano Mwakahesya, Mkurugenzi Mkuu.

Kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (*EWURA*) yuko Bwana Simon Sayore, Mwenyekiti wa Bodi na Bwana Haruna Masebo, Mkurugenzi Mkuu. Karibu sana. Kutoka *STAMICO*, yuko Bwana Ramadhan O. Khatib, Mwenyekiti wa Bodi na Bwana Grey Mwakalukwa, Mkurugenzi Mkuu *STAMICO*. Kwa kweli, Mheshimiwa Waziri ameleta timu kamili kabisa. Tunampongeza pia kwa hilo.

Kwa heshima, naomba nitambue uwepo wa Wajumbe wa Kamati ya Rais ya Kushauri Serikali kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini. Na niwakumbushe tu Waheshimiwa kwamba, Taarifa hii inatakiwa upate randama tatu (*volume 3*). Kama unayo moja tu au mbili bas, ziko mbili? Juzuun namba mbili na namba tatu? Wanasesma

kwamba juuu namba moja kumbe haihusiki. Basi angalau upate hizo mbili ndio zinahusika.

Sasa, Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini kama mnayofahamu Waheshimiwa, inaongozwa na Mheshimiwa Jaji Mark Bomani ambaye ndiye Mwenyekiti. Yule pale Mheshimiwa Jaji Mark Bomani. Haihitaji maneno mengi sana kumtambulisha Mheshimiwa Jaji Mark Bomani kwa sababu alikuwa ndiye Mwanasheria Mkoo wa kwanza wa nchi yetu Mtanzania. Na katika taaluma hiyo amebobea kiasi kwamba ndiye aliyeaminwa kwenda kusaidia utunzi wa Katiba ya Namibia, na pia ndiye aliyekuwa Msaidizi Mkoo wa Baba wa Taifa katika Usuluhihi wa Mgogoro wa Burundi. Tunafurahi sana kumpata Mheshimiwa Bomani Mtanzania ambaye kwa kweli amechomoza katika sifa nyingi. Karibu sana Mheshimiwa Jaji Bomani. (*Makofî*)

Pamoja naye, hawa ni wenzetu, ni Wabunge wenzetu, sijui niwaieteje maana wameorodheshwa hapa baadhi yao! Basi, wasimame maana nayo nisifanye ubaguzi. Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Zitto Kabwe naona hayupo, Mheshimiwa Ezekiel Maige sasa ni Naibu Waziri naye hayupo, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe naye hayupo, anafuatia Mheshimiwa Idd Simba, yule pale. Ahsante sana. Mheshimiwa Idd Simba naye ana historia ndefu ya kutumikia nchi yetu, tunashukuru sana kumwona hapa. Bwana Peter Machunde, Bwana Mugisha Kamugisha, Bibi Maria Kejo, Bwana Edward Kihunra na Bibi Salome Makange. Karibuni sana na tunashukuru kwa kazi yenu nzito ambayo tunadhani itasaidia nchi yetu kuweza kuwa na mazingira ambayo yatakuwa na faida kwa nchi na maslahi ya nchi zaidi kuliko ilivyokuwa zamani katika Sekta ya Madini. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine sasa: Wageni wa Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Dr. Harrison Mwakyembe na Dr. Guido Sigonda, kwanza ni mama Margereth Ndomondo Sigonda ambaye ni Mke wa Mheshimiwa Dr. Sigonda, lakini pia ndiye Mkurugenzi Mkoo wa Mamlaka ya Chakula, Dawa na Vipodozi. Pamoja naye wapo vijana Godfrey, Erika, Getrude, Erina, Lutengano na Said Kikome. Ahsante sana, karibuni sana. (*Makofî*)

Miongoni mwa wageni waliopo hapo juu ni Wakala wa Jiolojia, Prof. Abdulkarim Mruma, *GST*. Yule pale. Kutoka Chuo cha Madini, Mkoo wa Chuo cha Madini, Bwana Candidus Lupindu. Ahsante, karibuni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Emmanuel Luhahula ni Augustin Kabelela, Katibu wake, katibu wa ofisi kule Jimboni na Emmanuel Maziku, dereva wake. Ni vizuri nao waone mambo haya.

Wageni wa Mheshimiwa Mohamed Chomboh ni uongozi wa CCM Wadi ya Magomeni, Zanzibar wakiongozwa na Mwenyekiti wao Bibi Hamisa. Wale pale, karibuni sana Waheshimiwa kutoka Zanzibar. Tunafurahi mara kwa mara kuwaona kwa sababu kwanza ni mbali, lakini ni sehemu muhimu sana ya Jamhuri ya Muungano.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni vikao:-

Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, anaomba wajumbe wote wa Kamati ya Huduma za Jamii mkutane ukumbi namba 428 leo saa 5.00 asubuhi.

Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, anaomba wajumbe wote mkutane saa 7.00 mchana leo ukumbi namba 231. Kwa hiyo, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, saa 7.00 mchana, ukumbi namba 321.

Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mwenyekiti wa *CPA* Tanzania, ameniomba niwatangazie wajumbe wote wa *CPA* Tawi la Tanzania, kutakuwa na mkutano saa 7.30 mchana, kuwa na mazungumzo na Mheshimiwa Katibu Mkuu wetu, Dr. William Shija.

Kwa hiyo, saa 7.30 *CPA* wajumbe wa Tawi letu hili la Tanzania, mkutano katika ukumbi wa Pius Msekwa leo. Na kabla ya hapo, wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji ya *CPA* Tawi la Tanzania, mnaombwa kukutana na Mheshimiwa Dr. William Shija saa 5.00 asubuhi katika ukumbi namba 219.

Kwa hiyo, saa 5.00 kwanza, Katibu Mkuu Dr. Shija atakutana na Kamati ya Utendaji ya *CPA* na saa 7.30, wajumbe wote wa *CPA* Tawi la Tanzania.

Mnakaribishwa nyote kwenye maonyesho ya *TANESCO*, *TPDC* na Wakala wa Jiolojia yaliyopo kwenye uwanja wa tafrija nyuma ya jengo la utawala. Pale kuna maonyesho, itasaidia sana kuweza kuona shughuli mbali mbali za *TANESCO*, *TPDC* na Wakala wa Jiolojia (*Geological Survey of Tanzania*).

Waheshimiwa Wabunge, ninafurahi kutangaza ifuatavyo kwamba katika mapumziko ya mwisho wa wiki, timu mbali mbali za Bunge za michezo zilicheza na matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:-

Kwenye michezo wa mpira wa miguu wa kirafiki baina ya Timu ya Bunge, Wabunge na Kampuni ya Bia *TBL*, matokeo kama ambavyo mngetarajia, tuliwafunga *Breweries* mawili kwa moja. Hili ni Bunge la Viwango, linaongozwa na Spika, makini.

Kwa hiyo, katika fani zote; Mawaziri wanavyojibu maswali, uchangiaji wa mijadala uliochangamka, lakini hatuko nyuma hata kwenye michezo. Tunataka nini zaidi. Mambo hayakuishia hapo, katika michezo wa kuvuta kamba, Bunge dhidi ya Tanzania *Breweries*, Bunge Timu yetu ya Wabunge ilishinda raundi zote mbili. Hakika Bunge hili linafurahisha sana. (*Makofi*)

Napenda kuwapongeza sana wenzetu waliotupa heshima hii. Najua wanafanya mazoezi kwa bidii na ofisi yangu inawawezesha, wanapata vitu vingi tu na ndio maana wanacheza vizuri. Na napenda mfahamu kwamba Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wetu wa Nishati na Madini ni mmoja wa wachezaji hatari sana, anaogopwa sana na magoli kipa wengi hapa nchini. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofî*)

Niwakumbushe tu kwenye tangazo la *CPA* kwamba wanachama yaani wajumbe wa *CPA Branch* ni sisi Wabunge wote. Kwa hiyo, kamati ya utendaji ndio wale wachache. Lakini saa 7.30 ni sisi Wabunge wote ukumbi wa Pius Msekwa tuongee na mwenzetu Dr. William Shija, atufahamishe mambo yanavyokwenda katika *CPA*. Ahsante sana. Bado matangazo tena!

Waheshimiwa Wabunge, tumekawia kidogo kuweza kupata uamuzi kuhusu suala la Mheshimiwa Nazir Karamagi. Katika Mkutano uliopita mtakumbuka alisimama Mheshimiwa Anna Abdallah, akamwomba Mheshimiwa Karamagi athibitishe ikiwa usemi wake kwamba suala la Mkataba wa *TICTS* lilijadiliwa na Baraza la Mawaziri, kama ni kweli.

Mheshimiwa Karamagi aliniletea barua ambazo hazikutosheleza sana. Kwa hiyo, nikaagiza ofisi ifanye mawasiliano na Ikulu. Na jibu tulilopata linasema kwamba, Mkataba wa *TICTS*, nikanukuu: “Ulifuata taratibu zote za Kiserikali” Mwisho wa kunukuu.

Sasa kutokana na hilo, ni dhahiri kabisa kwamba utaratibu wa kubinafsisha wa Kiserikali huhusisha Baraza la Mawaziri. Na kwa maana hiyo basi, natoa uamuzi kwamba Mheshimiwa Karamagi, hakusema uongo, alisema kweli. (*Makofî*)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali ywa Mwaka 2008/2009 – Wizara ya Nishati ya Madini

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2007/08. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2008/09.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu makadirio ya matumizi ya fedha za Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2008/09.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kutoa shukurani kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa kunitua kuwa Waziri wa Nishati na Madini mwezi Februari, 2008, uteuzi ambao umenipa fursa kwa mara ya kwanza kuwasilisha Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia, nawashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo (Mb) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe (Mb), kwa mchango wao mkubwa wakati wa uchambuzi wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2008/09. Nakushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, Naibu Spika pamoja na wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa umahiri mkubwa. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushauri wanaonipa mimi na wenzangu katika kusimamia na kuongoza sekta za nishati na madini. Nina imani kuwa ushirikiano huo utaendelea ili tuweze kufikia malengo ya Taifa hasa katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, pia, naomba kutumia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Hiyo ni heshima kubwa kwa Taifa letu. Pia, nampongeza Mhe. Rais kwa juhudzi zake katika kuvutia wawekezaji na ukuzaji mahusiano na nchi nyingine ikiwa ni pamoja na kufanikisha ziara ya Mhe. George W. Bush, Rais wa Marekani na kufanikisha kufanyika kwa mikutano wa Leon Sullivan jijini Arusha mwezi Juni, 2008. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kufanikisha kusuluuhisha mgogoro wa kisiasa uliotokana na vurugu za uchaguzi nchini Kenya akiwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, vilevile, nampongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, nakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kuteuliwa kwako kuwa Makamu wa Rais wa Chama cha Wabunge wa Nchi za Jumuiya ya Madola (*CPA*). Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani (Mb), kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (*TAMISEMI*); Mheshimiwa Profesa Peter Msolla (Mb), Waziri wa Sayansi, Mawasiliano na Teknolojia; Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa (Mb), Waziri wa Miundombinu; Mheshimiwa Stephen Wassira (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika; Mheshimiwa Aggrey Mwanri (Mb), Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje (Mb), Naibu Waziri wa Miundombinu na Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga (Mb), Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Dkt. James Wanyancha, (Mb) Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, (Mb), Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa uteuzi wao kufuatia mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri yaliyofanywa na Mhe. Rais mwezi Mei, 2008.

Napenda kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioleuliwa na Mheshimiwa Rais mwezi Februari, 2008 kushika nyadhifa hizo akiwemo Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima, Mbunge wa Mkuranga, aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Benedict Ngalamu Ole-Nangoro

(Mb), kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto. Pia, nawapongeza Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyr (Mb), na Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude P. Rwakatare (Mb), kwa kuteuliwa kwao kuwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2007 Bunge lako lilimpoteza Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia (Mb), aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, aliyefariki dunia kufuatia ajali ya gari. Aidha, mwezi Desemba, 2007 Bunge lako lilimpoteza Mheshimiwa Benedict Kiroya Losurutia aliyekuwa Mbunge wa Kiteto. Pia, nampa pole Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima, Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kufiwa na mke wake. Natoa pole kwako, familia zao na wote walioguswa na misiba hiyo. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amin!

Mheshimiwa Spika, tarehe 28 Machi, 2008, kulitokea maafa yaliyosababishwa na mafuriko katika baadhi ya machimbo ya madini ya *tanzanite* Merelani, Wilayani Simanjiro ambapo wachimbaji wadogo 78 walipoteza maisha. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilifanikiwa kuopoa miili ya watu wote 78 walipoteza maisha. Natoa pole kwa Mhe. Christopher Ole Sendeka, Mbunge wa Simanjiro, ndugu, jamaa na Taifa kwa ujumla. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amin.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Sengerema na viongozi wa Wilaya ya Sengerema kwa ujumla kwa ushirikiano wao wanaonipa na juhudni zao katika kazi mbalimbali ambazo zinachangia maendeleo ya Jimbo na wilaya yetu kwa ujumla. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naishukuru familia yangu, wazazi na ndugu zangu kwa jinsi wanavyoendelea kuniimarissha katika utekelezaji wa majukumu yangu, hususan, mke wangu Blandina ambaye anaendelea kuisimamia familia yetu pamoja na kumlea binti yetu mwenye umri wa mwezi mmoja na nusu sasa. Nakushukuru sana mke wangu Blandina, kwa kweli ningependa wawepo hapa lakini kwa mazingira hayo, namwomba radhi tu kwamba hayupo na sisi leo lakini nashukuru sana Mke wangu kwa jinsi anavyonilea (*Makofi*)

SPIKA: Nilitaka nikuulize Mheshimiwa Waziri leo yupo wapi, kwa sababu siyo kawaida yako wewe kuwa hapo bila Mama.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2007/08. Mpango na Bajeti kwa mwaka 2007/08, ulitekelezwa kwa kuzingatia:- Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2005; malengo ya MKUKUTA; Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti 2007/08 – 2009/10; ushauri na maelekezo ya Mhe. Rais alipotembelea Wizara ya Nishati na Madini Januari, 2006; na ushauri uliotolewa na iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2007/08 zilikuwa ni:- kukamilisha uanzishwaji wa Wakala wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Agency - REA*) pamoja na Mfuko wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Fund - REF*); Kukamilisha mkakati wa Kurekebisha Sekta ya Umeme; Kuimarisha Mfumo wa Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme; Kuanzisha miradi ya hifadhi ya mafuta na kuiwezesha *TPDC* kushiriki katika biashara ya mafuta; kuratibu utekelezaji wa miradi ya gesi asilia; kukamilisha maandalizi ya sheria ya mafuta na sheria ya gesi asilia, kuhamasisha matumizi bora na uendelezaji wa nishati jadidifu na mbadala; kuendelea kukuza uwekezaji katika sekta za nishati na madini kwa kuweka mazingira shindani ya kuvutia wawekezaji; kuendelea kuhamasisha ujasiriamali kwenye miradi ya kuongeza thamani madini kama ukataji na usanifu wa madini na utengenezaji wa bidhaa za madini ya vito; kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata mikopo na teknolojia mwafaka katika utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini; kuongeza maduhuli ya Serikali yatokanayo na madini; na kuimarisha masuala ya usalama, afya na utunzaji wa mazingira katika shughuli za utafutaji na uchimbaji madini.

Mheshimiwa Spika, mafanikio katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2007/08, Wizara ilipata mafanikio yafuatayo:- kupitishwa kwa Sheria ya Umeme na Sheria ya Mafuta mwezi Aprili, 2008; kuanza kazi rasmi kwa Wakala wa Nishati Vijijini mwezi Oktoba, 2007; kukamilika kwa kazi ya kukarabati jenereta yenye uwezo wa KVA 320 mjini Mbanga mwezi Septemba, 2007; kununuliwa kwa jenereta mbili zenye uwezo wa KVA 1,250 kila moja kwa ajili ya mji wa Mbanga na mbili zenye uwezo wa KVA 600 kila moja kwa ajili ya mji wa Ludewa; kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme chenye uwezo wa MW 100 katika eneo la TANESCO-Ubungo Dar es Salaam; kugundulika kwa gesi asilia katika kisima cha Kiliwani Kaskazini Namba 1 Kilwa; kupanuka kwa matumizi ya gesi asilia ambapo viwanda vinne (4) vilivyopo Dar es Salaam vilipatiwa huduma hiyo, viwanda hivyo ni Serengeti *Breweries*, Simba Plastic, Namera *Textile* na Simba *Steel*; kujadiliwa na kukamilika kwa mikataba mitatu (3) mipyä ya utafutaji wa mafuta; kuanzishwa kwa Kitengo cha Ukaguzi wa Shughuli za Uzalishaji na Biashara ya Madini ya Dhahabu katika Migodi Mikubwa (*Gold Audit Programme - GAP*) mwezi Agosti, 2007; Kuunganishwa kwa Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini (*Mining Cadastre Information Management System – MCIMS*) katika ofisi 22 za madini mikoani na Makao Makuu ya Wizara; kufunguliwa kwa ofisi ya afisa madini mkazi mkoani Kigoma mwezi Septemba, 2007; kupitishwa kwa muundo mipyä wa Wizara mwezi Agosti, 2007; na kujitokeza kwa watumishi 117 wa Wizara kupima afya zao kuhusu UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, changamoto, pamoja na mafanikio yaliyotajwa hapo juu, kumekuwa na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na:- kuhimili kasi kubwa ya upandaji wa bei ya mafuta katika soko la dunia; kasi ndogo ya kufikisha umeme vijijini kwa Watanzania walio wengi; kutokuwepo rasilimali fedha inayokidhi mahitaji halisi ya kuwezesha ukarabati na upanuzi wa mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme; kukabiliana na ongezeko kubwa la gharama za utekelezaji wa miradi; kupunguza hujuma (*vandalism*) zinazofanywa kwenye miundombinu ya umeme; mitaji isiyokidhi uwekezaji katika miradi ya gesi asilia ya Songo Songo na *Mnazi Bay*; kuanzisha hifadhi ya Taifa ya

mafuta ya Petroli; upungufu wa watumishi wa taaluma mbalimbali; na kupata rasilimali za kutosha kwa ajili ya kuharakisha upatikanaji wa huduma bora za nishati vijijini.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Nishati, Ukuaji wa Sekta na Mchango wake katika Pato la Taifa katika mwaka 2007, shughuli za kiuchumi za umeme na gesi asilia zilikua kwa asilimia 10.9 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 1.9 mwaka 2006, kwa bei za mwaka 2001. Miiongi mwa sababu za ukuaji huo ni pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji umeme kutoka katika mitambo ya dharura; kuwepo kwa maji ya kutosha kwenye mabwawa ya kuzalisha umeme; kukua kwa matumizi ya umeme viwandani kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji katika viwanda vya chuma na saruji. Aidha, mchango wa kiuchumi wa umeme na gesi asilia katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.1 mwaka 2007 ikilinganishwa na asilimia 2.0 mwaka 2006, kwa bei za mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007, umeme uliozalishwa ulikuwa *megawatt-hour* (MWh) 4,204,620 ikilinganishwa na MWh 3,592,470 mwaka 2006, sawa na ongezeko la asilimia 17. Ongezeko hilo lilitokana na kuwepo kwa maji ya kutosha, hususan, katika mabwawa ya Mtera na Kidatu yanayotumika kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, Kupeleka Umeme Vijijini, katika mwaka 2007/08, miradi ya usambazaji umeme vijijini ilitekelezwa kwa kasi ndogo kutokana na upungufu wa fedha baada ya Serikali kuelekeza rasilimali nyingi katika kukabiliana na matatizo mbalimbali yaliyosababishwa na ukame. Pia, miradi mingi ya kupeleka umeme vijijini inahitaji fedha nyingi ikilinganishwa na mapato madogo ya TANESCO yatokanayo na malipo ya huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Nishati Vijijini, Wakala wa Nishati Vijijini ulianza kazi rasmi mwezi Oktoba, 2007 na umeajiri jumla ya watumishi 21 kati ya 30 wanaohitajika. Wakala unakusudia kuwa na wafanyakazi makini wachache ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuelekeza rasilimali katika kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, majukumu makuu ya Wakala ni:- kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji katika upatikanaji wa huduma za nishati bora vijijini, kwa kutoa ruzuku kwa wawekezaji kutoka sekta binafsi na ya umma; na kuwasaidia wawekezaji kuandaa miradi ya nishati itakayowasilishwa kwenye Bodi ya Nishati Vijijini kwa ajili ya uamuvi wa miradi hiyo kupatiwa ruzuku. Mfumo wa utendaji wa Wakala unahamasisha ubia wa sekta ya umma na binafsi (*Public-Private Partnership – PPP*) ili kuiwezesha sekta binafsi kushiriki vilivyo katika kuchangia kutoa huduma za nishati kwa wananchi vijijini. Uwezeshaji wa miradi utazingatia uwiano wa kijiografia na vigezo vingine vilivyoainishwa katika Sheria ya Nishati Vijijini ya mwaka 2005 na kama ilivyoelezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005, Ibara ya 43 (c).

Mheshimiwa Spika, pamoja na uchanga wake, Wakala tayari umeanza kujenga mtandao (*network*) wa wadau mikoani na wilayani ikiwa ni pamoja na wamiliki na waendelezaji wa vyanzo mbalimbali vya nishati vijijini. Hata hivyo, changamoto zilizojitokeza ni pamoja na:- kutopata rasilimali za kutosha kwa ajili ya kuharakisha upatikanaji wa nishati bora vijijini; kuwaelimisha wadau majukumu ya Wakala; na

uwezo mdogo wa kifedha vijijini hivyo kusababisha uwekezaji katika miradi ya nishati kushindwa kuwa kivutio kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Upelekaji Umeme Makao Makuu ya Wilaya, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 ilielekeza kuongeza kasi ya kupeleka umeme vijijini kupitia mfuko wa Nishati Vijijini. Katika mwaka 2007/08, Wakala wa Nishati Vijijini kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini (*REF*) umetoa ruzuku kwa ajili ya kupeleka umeme katika makao makuu ya wilaya tano (5) za Kilolo, Kilindi, Mkinga, Bahi na Uyui. Pia, baadhi ya maeneo ambayo yalipatiwa fedha kutoka katika Mfuko huo ni Mto wa Mbu, Matema Beach na Shule ya Sekondari ya *Chief Oswald Mang'ombe* iliyopo Musoma. Aidha, Mfuko pia ulitoa fedha kwa ajili ya kulipa fidia ya mali za wananchi zilizoathirika wakati wa kutathmini njia ya usambazaji umeme kwenye mradi wa njia ya bomba la gesi ya kutoka Songo Songo hadi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miji ya Mbinga na Ludewa, jenereta mpya zimenunuliwa na ufungaji unaendelea. Aidha, mifumo ya usambazaji umeme katika miji hiyo imekamilika. Mipango ya muda mrefu ni kuipatia miji hii pamoja na Songea na Namtumbo umeme wa gridi ya Taifa. Serikali ya Uswizi (Sweden) wamethibitisha ufadhlili wa mradi wa Makambako hadi Songea pamoja na miji ya Mbinga, Ludewa, Namtumbo, na vijiji vilivyoko katika laini zitakazojengwa. Mradi pia utahusu upanuzi wa mifumo ya usambazaji umeme katika miji ya Makambako, Njombe na Songea. Gharama ya mradi ni US\$70.4 milioni. Asilimia 90 zitatolewa kama msaada na asilimia 10 kama mkopo wa masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, ufanuzi huu unamsaidia sana Mheshimiwa Vita Kawawa kwa swali alilouliza.

Mheshimiwa Spika, Sheria Mpya za Umeme, Mafuta ya Petroli na Gesi Asilia, Muswada wa Sheria ya Umeme ulipitishwa na Bunge mwezi Aprili, 2008, na kuridhiwa na Mheshimiwa Rais tarehe 6 Juni, 2008. Sheria mpya itaimarisha udhibiti wa uzalishaji, usafirishaji, usambazaji pamoja na matumizi bora ya umeme, itawezesha biashara ya umeme na nchi jirani, na pia itaweka mipango ya kusambaza umeme vijijini. Aidha, Sheria hii imetambua umuhimu wa kuiimarisha TANESCO katika kipindi cha mpito ili iweze kuhimili ushindani kutoka sekta binafsi muda utakapowadia. Sheria mpya vilevile imefafanua jukumu la wawekezaji katika sekta ya umeme kutoa huduma kwenye maeneo ya vyanzo vya nishati, pamoja na maeneo yote ambayo yanapitiwa na njia kuu za kusafirisha umeme.

Mheshimiwa Spika, pamoja na masuala mengine, Sheria hiyo imefafanua majukumu na mamlaka ya Waziri mwenye dhamana ya nishati ikiwa ni pamoja na kusimamia sekta ya umeme katika utekelezaji sera na uandaaji wa mipango na mikakati ya kuhamasisha soko lenye ushindani kwa lengo la kuvutia wawekezaji binafsi na kulinda maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Mafuta ya Petroli ulipitishwa na Bunge mwezi Aprili, 2008, na kuridhiwa na Mheshimiwa Rais tarehe 6 Juni, 2008.

Aidha, Rasimu ya Sheria ya Gesi Asilia imeandaliwa na Wizara ipo katika hatua za kupata ridhaa ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa mchakato wa kutungwa Sheria Mpya za Umeme na Mafuta ya Petroli, Wizara inaratibu utayarishaji wa kanuni na taratibu husika kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa sheria hizo. Wizara itashirikiana na wadau muhimu kuhakikisha kuwa kanuni hizo zinakamilika ifikapo mwezi Oktoba, 2008.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Uendeshaji wa TANESCO, mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji wa TANESCO na muundo wake yanaendelea kufanyika yakilenga katika uboreshaji wa huduma, ufanisi na kujidesha kibashara. Pamoja na kufikia kiwango cha ukusanyaji wa mapato kwa asilimia 96 katika mwaka 2006 na 2007, TANESCO imeendelea kuathiriwa na upungufu wa fedha uliosababishwa na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji hususan, katika uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, Mifumo ya Usafirishaji na Usambazaji Umeme, tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara kwenye gridi ya Taifa limeanza kupungua kutokana na ukarabati uliofanywa katika miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme katika gridi ya Taifa. Ukarabati uliendelea kufanyika katika baadhi ya maeneo na nguvu zaidi zilielekezwa katika maeneo yaliyokuwa na uchakavu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Umeme Sumbawanga, tatizo la kukatikakatika kwa umeme Sumbawanga linatarajiwu kwisha mwishoni mwa mwaka 2008 kufuatia ahadi iliyotolewa na Waziri wa Nishati na Maendeleo ya Maji wa Zambia katika kikao kati yake na Waziri wa Nishati na Madini wa Tanzania kilichofanyika tarehe 30/06/2008 mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Umeme Kigoma, mkakati wa muda mfupi wa kuongeza upatikanaji wa umeme wa Kigoma ni ununuzi wa mitambo mitano yenye uwezo wa kuzalisha jumla ya MW 6. Fedha za ununuzi huo takribani shilingi bilioni 13.8 zimetengwa na ufungaji wa mitambo unatarajiwu kukamilika mwishoni mwa mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Japani ilikuwa na mpango wa kujenga kituo cha kupozea umeme cha New Oysterbay ili kuboresha upatikanaji wa umeme katika jiji la Dar es Salaam. Hata hivyo, mradi haukuweza kuanza katika muda uliopangwa kutokana na upeo wa mradi kubadilika na kuchelewa kupata umiliki wa kiwanja. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kumwajiri mshauri na kukamilisha kazi za awali za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa kuendeleza na kupanua wigo wa upatikanaji wa nishati Nchini (*Tanzania Energy Development and Access Expansion Project – TEDAP*), makubaliano ya utekelezaji wa mradi wa kuendeleza na kupanua wigo wa upatikanaji wa nishati nchini (*Tanzania Energy Development and Access Expansion Project –TEDAP*) yalifikiwa kati ya Serikali na Benki ya Dunia mwezi Januari, 2008. Utekelezaji wa mradi ulianza mwezi Aprili, 2008. Lengo la mradi huu ni kuboresha mifumo ya usafirishaji na

usambazaji umeme katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro (Dola za Marekani milioni 85.8); na kuendeleza mifumo ya umeme nje ya gridi (*off-grid electrification*) kwa kutumia nishati jadidifu kwa ajili ya matumizi majumbani, katika taasisi na kwenye shughuli za uzalishaji mali (Dola za Marekani milioni 22.5). Mradi pia umelenga katika kujenga uwezo wa kitaalamu wa Wakala wa Nishaji Vijijini, *TANESCO* na Wizara, ambapo kiasi cha Dola za Marekani milioni 3.2 zitatumika.

Mheshimiwa Spika, Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme PSMP (*Power System Master Plan*), maandalizi ya kutayarisha Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme (*Power System Master Plan – PSMP*) ambao utatumika kuongoza maendeleo endelevu ya sekta yalikamilika katika mwaka 2007/08. Utayarishaji wa *PSMP* umezingatia Sera ya Taifa ya Nishati, hususan, upanuzi wa wigo wa vyanzo vya nishati kwa ajili ya kuzalisha umeme ili kupunguza utegemezi katika umeme utokanao na maji. Aidha, wataalamu wa Wizara na *TANESCO* walishiriki katika hatua na maeneo mbalimbali ya kutayarisha PSMP, kwa mfano, uandaaji wa mipango inayozingatia unafuu wa gharama (*Least-Cost Expansion Plans*) katika uzalishaji na usafirishaji wa umeme. Wizara iko katika hatua za mwisho za kupata ridhaa ya Serikali kwa ajili ya kutumia Mpango Kabambe.

Mheshimiwa Spika, Mipango ya muda wa kati kulingana na *PSMP* inahusisha miradi ya Mchuchuma (MW400), Rusumo (MW60), Ruhudji (MW358) na katika kipindi cha muda mrefu, miradi ya *Stiegler's Gorge* (MW2,400), Rumakali (MW222), Mpanga (MW158) na Masigira (MW144).

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Taifa ya Mafuta kutopteka na mabadiliko mbalimbali yaliyotokea duniani yakiwemo ya kisiasa, kiuchumi, hali ya hewa pamoja na uzoefu kutoka nchi nyingine, Serikali iliridhia kuanzishwa kwa hifadhi ya Taifa ya mafuta nchini kwa ajili ya kutumika inapotokea dharura na kutengemaza mwenendo wa bei za mafuta ya petroli nchini. Uamuhi huu ulifikiwa mwezi Machi, 2008. Ili kufanikisha hilo, Serikali kupitia *TPDC* inaendelea na mchakato wa utekelezaji wa uamuhi huo.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Kiwanda cha kusafisha mafuta na bomba la mafuta la Dar es Salaam – Mwanza, Serikali inaendelea na majadiliano na mwekezaji aliyeonesha nia ya uendelezaji wa miradi ya kujenga kiwanda cha kusafisha mafuta ya petroli. Aidha, Serikali inakamilisha uchunguzi wa kampuni husika ya *Noor - Oil and Industrial Technology (NOIT)* na wabia wake. Endapo uhakiki utaleta matokeo mazuri, Serikali itaridhia *NOIT* kuanza upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Utafutaji na Uzalishaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005 (Ibara ya 43 (h)) inatutaka kuendelea kutafuta mafuta kwa kasi zaidi. Kuanzia mwezi Julai, 2007 hadi Juni 2008, Serikali imesaini mikataba mitatu ya utafutaji mafuta ya petroli na kampuni zifuatazo:- *Dodsal Hydrocarbon & Power* ya India eneo la Ruvu; *Funguo Petroleum* ya Australia, magharibi mwa eneo la Songo Songo; na *Hydrotan* ya Visiwa vya Morisi (*Mauritius*), eneo la Kaskazini ya Mnazi Bay. Hii inafanya idadi ya mikataba yote ya utafutaji mafuta

nchini kufikia 22, makampuni 13. Kampuni hizo zinaendelea na shughuli mbalimbali za utafutaji mafuta na gesi asilia ikiwemo kudurusu takwimu za kijiolojia na kijiofizikia katika maeneo husika, kuchukua takwimu za mitetemo, na kufanya maandalizi ya uchimbaji wa visima veya utafiti.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa utafutaji wa mafuta na gesi asilia uliofanywa na Kampuni ya Ndovu Resources katika Mkoa wa Lindi, umethibitisha kuwepo kwa gesi asilia katika kisima cha Kiliwani Kaskazini Namba 1. Kampuni hiyo inajиandaa kuchimba visima zaidi ili kubaini kiasi cha gesi kilichopo. Kampuni ya Maurel & Prom kutoka Ufaransa inayofanya utafiti katika maeneo ya Mkuranga imekamilisha tathmini ya taarifa za mitetemo na imeainisha maeneo ambayo vitachimbwa visima veya kuhakiki (*appraisal wells*) kiasi cha gesi kilichopo. Aidha, inachimba kisima kingine cha utafutaji (*exploratory well*) katika eneo la Mafia.

Mheshimiwa Spika, Gesi Asilia ya Songo Songo, gesi asilia ya Songo Songo ilianza kutumika kuanzia Julai, 2004 kwa ajili ya kuzalisha umeme Dar es Salaam na kutumika kama nishati viwandani. Kufuatia ongezeko la mahitaji ya gesi kwa ajili ya kuzalisha umeme, umejitokeza ulazima wa kuongeza uwezo wa mtambo wa kusafisha gesi kutoka futi za ujazo milioni 70 kwa siku hadi futi za ujazo milioni 140 kwa siku ili kusafisha gesi zaidi kwa ajili ya mitambo iliyopo na mipya. Kazi ya upanuzi inategemewa kukamilika mwezi Agosti, 2009.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuitia mikataba ya mradi wa Songo Songo na kufanya marekebisho ya mikopo husika ili kupunguza *capacity charge*. Hii ni hatua muhimu kwani marekebisho husika yatapunguza capacity charge kwa Dola za Marekani takriban milioni 1.0 kwa mwezi. Aidha, Serikali inaendelea kuitia mikataba yote ya nishati.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Gesi Asilia ya *Mnazi Bay*, kazi ya kupima na kutathmini kiasi cha fidia ya mali kwa ajili ya bomba la gesi asilia toka *Mnazi Bay* hadi Mtwara imekamilika na tayari bomba limetandazwa. Visima vitatu (*Mnazi Bay 2, 3 na Msimbati 1*) vimechimbwa na vimetoa matokeo ya kuwepo kwa gesi asilia ya kutosha kutekeleza mradi wa umeme wa MW 30 na miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005 (Ibara ya 43 (a) (ii) Mikoa ya Lindi na Mtwara iliwekwa katika mpango wa kupatiwa umeme unaozalishwa na Kampuni ya Artumas kwa kutumia gesi asilia ya *Mnazi Bay*. Miji ya Lindi na Mtwara tayari imeanza kupata umeme unaotokana na mradi huo tangu Desemba, 2006. Aidha, mikataba ya kuiwezesha Artumas kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme katika maeneo mengine ya mikoa hiyo inatarajiwa kukamilishwa mwishoni mwa mwezi Julai, 2008.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi na Udhibiti wa Shughuli za Nishati, katika mwaka 2007/08, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*) iliendelea na kazi ya kutoa leseni kwa watoa huduma wa umeme na mafuta, kuhakiki bei za umeme na

kanuni ya kupanga ushuru kwa kutumia miundombinu ya gesi asilia ya Songas katika soko la nishati, kukagua na kuhakiki uwezo, ubora na usalama wa vituo vya kuzalisha umeme pamoja na vituo na maghala ya kuhifadhia mafuta ili kuleta nidhamu katika biashara ya mafuta. Aidha, *EWURA* ilitoa elimu kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Mamlaka hiyo kwa wadau kupitia warsha na makongamano. Vilevile *EWURA* kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Nchini (*TBS*) ilifanikiwa kuvinasa na kuvifungia vituo 154 kati ya 194 vilivyogunduliwa kutokana na kujihusisha katika kuchakachua mafuta ya petroli.

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge wanavyofahamu, uhusiano kati ya *TANESCO* na *IPTL* umekuwa wa mashaka kufuatia kutokubaliana na kiwango cha *capacity charge* kinachotozwa. Maamuzi yaliyotolewa na Kituo cha *International Centre for Investment Disputes*, mwaka 2001 wakati wa usuluhishi wa shauri lililowasilishwa na *TANESCO* dhidi ya *IPTL*, iliamriwa kuwa *capacity charge* itakokotolewa kwa kutumia mtaji (*equity*) wa asilimia 30 na faida ya asilimia 22.31. Kiwango cha *equity* kilichotumika kilikuwa Dola za Marekani milioni 86.54.

Mheshimiwa Spika, kufuatia uchunguzi uliofanywa na *TANESCO* imegundulika kuwa equity halisi iliyotumika ilikuwa shilingi 50,000. Kwa maana hiyo, malipo ambayo *TANESCO* imekuwa ikiilipa *IPTL* kama *capacity charge* ni zaidi ya kiasi kilichostahili. Huu ndio msingi wa mgogoro wa sasa ambao Serikali/*TANESCO* na *IPTL* wanaendelea kujadili.

Mheshimiwa Spika, Gharama za Uendeshaji na Bei za Umeme, wakati *EWURA* inapotafakari maombi ya kurekebisha bei za umeme hutumia vigezo vyenye mwelekeo wa ufanisi wa gharama katika uwekezaji na ubora wa huduma kwa mteja. Aidha, maelekezo hutolewa kuhusu hatua za kuchukua za kupunguza gharama za uendeshaji bila kumtaka mlaji kulipia.

Mheshimiwa Spika, Gharama za uzalishaji za *TANESCO* zimepanda kutoka shilingi 96/kWh mwaka 2005 hadi shilingi 120/kWh mwaka 2007. Gharama za ujenzi wa njia za umeme zimepanda kutokana na kupanda kwa bei ya chuma na shaba kwenye soko la dunia. Gharama ya ujenzi wa njia ya kV 33 zimepanda kutoka Shilingi milioni 18 kwa kilometra mwaka 2006 hadi Shilingi milioni 35 kufikia Januari, 2008. Bei za nguzo zimepanda kutoka shilingi 96,000 mwaka 2005 hadi shilingi 153,017 kwa mwaka 2007 kwa nguzo za futi 10. *TANESCO* imelazimika kununua nguzo kutoka nje, ikiwemo Afrika Kusini kutokana na bei kuwa nafuu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji wa Nishati Jadidifu na Mbadala, katika mwaka 2007/08, Wizara iliendelea kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu na mbadala kwa kuzindua mradi wa umemenuru unaofadhiliwa na Sida katika mikoa ya Kigoma, Rukwa, Mtwara na Mbeya. Jumla ya mafundi sanifu na wafanyabiashara 72 katika mikoa hiyo walifundishwa namna ya kufunga mifumo ya umemenuru majumbani - *solar home systems* na jinsi ya kuboresha uendeshaji wa biashara zao. Aidha, utekelezaji wa mradi wa majaribio wa Mwanza unaofadhiliwa na *Global Environment Facility*, (*GEF*) iliendelea katika mikoa ya Kagera, Mara na Shinyanga. Ili kuendeleza uzoefu

uliopatikana mkoani Mwanza katika mikoa jirani iliyotajwa, mafunzo yalitolewa kwa mafundi mchundo 170. Mafunzo hayo pia yalitolewa kwa walimu 12 kutoka vituo sita vya VETA ili vituo hivyo vipate uwezo wa kutoa mafunzo ya umemenuru kwa wananchi wengine. Aidha, shughuli za ufungaji wa mifumo ya umemenuru ziliendelea katika vituo 47 vikiwemo vya afya na shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, mradi huo pia ulifanikiwa kukopesha *SACCOS* mbili kwa majaribio, ambapo wanachama 40 kutoka *SACCOS* hizo waliweza kufungiwa mifumo ya umemenuru ili kuhamasisha teknolojia hii. Semina zilifanyika kwa ajili ya maafisa maendeleo ya jamii 130 kutoka mikoa ya Kagera, Shinyanga na Mara kuanzia ngazi ya mkoa hadi kata.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005 inatambua umuhimu wa kutumia nishati mbadala, ikiwemo nishati ya upepo. Tafiti zimefanywa na zinaonesha kuwa Tanzania ina maeneo kadhaa ambayo yana uwezekano wa kuzalisha umeme utokanao na nishati ya upepo. Maeneo hayo ni pamoja na Mkoa wa Singida, Iringa, Kilimanjaro, Manyara na Rukwa. Kwa kuzingatia umuhimu wake, Serikali kwa kushirikiana na *TANESCO* iliendelea kujadiliana na wadau wenye nia ya kuwekeza katika uzalishaji wa umeme utokanao na nishati ya upepo ili kupanua wigo wa vyanzo vya nishati kwa ajili ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kuzalisha Bayofueli Nchini, suala la bayofueli limeendelea kufuatiliwa kwa makini. Kama unavyofahamu bayofueli inaweza kuzalishwa kutokana na mimea mbalimbali ikiwemo miwa, mtama, mibono na michikichi. Serikali iliendelea kushauriana na Serikali ya Uswidi kuhusu uwezekano wa kuchangia katika kutekeleza Mradi wa kuandaa Sera, Sheria na Muundo Kiasasi (*Strengthening the Policy, Legal, Regulatory and Institutional Framework*). Mradi huu una lengo la kuandaa mazingira sahihi ya uendelezaji endelevu wa bayofueli nchini. Hata hivyo, inatarajiwा kwamba kilimo cha mazao ya bayofueli kitazingatia maslahi ya Taifa kuhusu ajira, ardhi, mazingira na upatikanaji wa chakula. Tangu mwaka 2005, kampuni nane (8) zimepata hati ya uwekezaji kutoka Kituo cha Taifa cha Uwekezaji, na zipo taasisi 30 zinazohusika na masuala ya bayofueli nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa rasimu ya Mwongozo wa bayofueli (*Biofuels Guidelines*) ikiwa ni hatua za awali na muda mfupi za kuwaongoza wawekezaji na wadau mbalimbali wakati maandalizi kuhusu masuala ya sera, sheria pamoja na kanuni na miundo kiasasi yakishughulikiwa. Rasimu ya Mwongozo inatarajiwা kukamilika mwishoni mwa mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, Maporomoko madogomadogo ya Maji na Jotoardhi, ubainishaji wa maporomoko madogomadogo ya maji iliendelea katika mikoa ya Iringa na Mbeya ambapo maeneo 30 mapya yenye uwezo wa takriban MW 29 yalifanyiwa tathmini ya awali. Aidha, Wizara imeendelea kutafiti uwezekano wa kuwepo rasilimali ya kutosha ya jotoardhi kwa ajili ya kuzalisha umeme. Sampuli zilizochukuliwa katika eneo la Songwe na Ziwa Ngozi zilifanyiwa utafiti wa kimaabara nchini Ujeruman. Matokeo ya utafiti yaliashiria uwezekano wa kuwepo rasilimali kubwa ya jotoardhi hapa

nchini. Uhakika wa ukubwa wa rasilimali hiyo utathibitishwa baada ya uchimbaji wa visima vya utafiti kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Matumizi Bora na Uendelezaji wa Vyanzo Mbadala vya Nishati, katika juhudi za kuendeleza elimu ya matumizi bora ya nishati mbadala hapa nchini kuitia mradi wa *SADC-ProBEC*, mafunzo ya utengenezaji majiko sanifu yalitolewa kwa mafundi 40 katika wilaya za Songea na Mufindi. Aidha, matanuri 60 ya kukaushia tumbaku yatumiayo teknolojia sanifu yalijengwa kwa ajili ya majaribio mkoani Tabora na matokeo ya awali yanaonesha uokoaji wa kuni kwa asilimia 50 ikilinganishwa na matanuri ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, katika kuhamasisha uendelezaji wa vyanzo mbadala wa kuni na mkaa kwa kupikia, Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ardhi ilifanya utafiti kuhusu gesi itokanayo na matumizi ya vitofali vya makaa ya mawe wakati wa kupika. Matokeo ya awali yameonesha kuwepo umuhimu wa kuboresha teknolojia ya utengenezaji wa vitofali ili kupunguza gesi yenye sumu hususan itokanayo na sulphur kwa lengo la kulinda afya za watumiaji. Ili kutekeleza hilo, majadiliano kati ya Wizara, Kampuni iliyotengeneza vitofali na Tume ya Sayansi na Teknolojia yameanza ili kutafuta namna ya kuboresha teknolojia hiyo.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa vifaa vinavyotumia umeme mwangi katika viwanda (kwa mfano mota, viyoyozi na taa) ulifanyika katika viwanda vikubwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro, Mwanza na Mbeya. Matokeo yanaonesha upotevu mkubwa wa umeme kutokana na uchakavu na kutokidhi kwa viwango vya ubora vya matumizi bora ya nishati. Upotevu huo unaweza kupungua kwa asilimia 30 hadi 40 iwapo vifaa vyenye viwango vya ubora unaotakiwa vitatumiwa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini, Ukuaji na Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 (Ibara za 38 na 39) inabainisha hatua za kuchukua ili kuharakisha ukuaji wa mchango wa sekta ya madini kwenye uchumi wa Taifa. Hatua hizo ni pamoja na: kuendelea kukuza ushirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi; kuweka mazingira bora ya kuvutia wawekezaji; kuimarisha usalama migodini; kuwaendeleza wachimbaji wadogo; kuboresha mahusiano kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa; na kuendeleza utafutaji wa madini nchini. Ilani hiyo pia inaelekeza kuendelea kuboresha Sera ya Madini kwa lengo la kuboresha ushiriki wa Serikali katika umiliki wa migodi, mfumo wa kodi katika sekta ya madini ili sekta ya madini iwe na manufaa zaidi kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo yaliyoainishwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM kama nilivyoleza hapo juu Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuiendeleza sekta ya madini kwa kuimarisha usimamizi wa sekta na kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini kama nitakavyoleza katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ukuaji halisi wa sekta ya madini mwaka 2007 kilikuwa asilimia 10.7 ikilinganishwa na asilimia 15.6 mwaka 2006 kwa bei za mwaka

2001. Upungufu huo ultokana na kupungua kwa uwekezaji mpya kwenye sekta ya madini na pia migodi mingine kama Buhemba kusimamisha shughuli za uzalishaji. Mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa mwaka 2007, ulikuwa asilimia 2.7 ikilinganishwa na asilimia 2.6 mwaka 2006. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini nchini na kuongezeka kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia. Mauzo ya madini yote nje ya nchi kwa mwaka 2007 yalikuwa ni takriban Dola za Marekani milioni 886.5 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 836.8 mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, Kuboresha Sera na Sheria ya Madini, katika Bunge la Bajeti ya Mwaka 2007/08, Wizara ilipanga kukamilisha durusu ya Sera ya Madini ya mwaka 1997 ili kuongeza mchango wa sekta katika Pato la Taifa. Rasimu ya Sera hiyo imeandaliwa kwa kuzingatia changamoto zilizotokana na ukuaji wa sekta ya madini, maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM na mapendekezo ya Kamati mbalimbali zilizoundwa. Kamati hizo ni Kamati ya Kudurusu Sera ya Madini ya mwaka 2005 na Kamati ya Kupitia Mikataba ya Madini ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa mwezi Novemba, 2007 Mheshimiwa Rais aliunda Kamati ya kuishauri Serikali Kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini. Kamati hiyo ilimaliza kazi na kuwasilisha taarifa yake kwa Mheshimiwa Rais mwezi Mei, 2008. Serikali imepokea na kuchambua mapendekezo ya Kamati hiyo na inaandaa mpango mkakati wa kurekebisha Sera ya Madini, Sheria ya Madini na sheria nydingine zinazohusu sekta ya madini ili kuyatekeleza mapendekezo hayo. Matarajio ya Wizara ni kuwa ifikapo mwezi Aprili, 2009 Sera ya Madini ya mwaka 1997 na Sheria ya Madini ya mwaka 1998 vitakuwa vimerekebishwa.

Mheshimiwa Spika, ninaliomba Bunge lako Tukufu lisome hotuba yangu pamoja na Taarifa ya Kamati ya Rais ya kuishauri Serikali kuhusu usimamizi wa Sekta ya Madini kwa vile taarifa hiyo ni sehemu ya hotuba hii kama ulivyoilitangazia Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuipongeza sana Kamati ya Mheshimiwa Rais iliyooongozwa na Mheshimiwa Jaji Mark Bomani kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini, ili kuendeleza utafutaji wa madini nchini kulingana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM mfumo wa utoaji na usimamizi wa leseni za madini umeimarishwa ili usaidie kuharakisha na kuweka wazi shughuli za utoaji na usimamizi wa leseni kwa kuongeza ufanisi katika uchambuzi wa maombi ya leseni za madini. Utoaji wa leseni umeongezeka takriban maradufu kwa wastani wa leseni 500 kwa mwezi kwa mwaka 2007/08 ikilinganishwa na wastani wa leseni 240 kwa mwezi kwa mwaka 2006/07.

Mheshimiwa Spika, Majadiliano na Kampuni za Madini, mwezi Machi, 2008, Serikali ilianza majadiliano na Kampuni ya *De Beers* ambayo ni mbia na Serikali (kupitia kampuni yake tanzu ya *Willcroft* katika mgodi wa almasi wa *Williamson Diamonds Limited (WDL)*, ili kuona namna ya kuboresha uzalishaji wa almasi katika mgodi huo na

kuhakikisha kuwa Serikali inafaidika na mapato yatokanayo na mgodi huo. Majadiliano hayo bado yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo, katika kutekeleza lengo la kuwaendeleza wachimbaji wadogo, kama ilivyoelekezwa na Ilani ya Uchaguzi, Serikali ilitenga maeneo katika sehemu mbalimbali za nchi, ambayo yanajumuisha Kilindi mkoani Tanga, Kilosa na Mvomero mkoani Morogoro ambako ilitenga hekta 269,842; Maganzo, Kishapu na Ibadakuli mkoani Shinyanga, hekta 14,870 na Mererani mkoani Manyara hekta 10,490. Pia, Serikali imefanikiwa kupata eneo la hekta 4,000 huko Winza Wilayani Mpwapwa, ambako mchakato wa taratibu za kisheria kwa ajili ya kulitenga na kuligawa rasmi kwa wachimbaji wadogo unaendelea. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2007/08 Serikali ilitenga maeneo ya Nyarugusu na Rwamgasa Wilayani Geita na maeneo ya Londoni na Sambaru Wilayani Manyoni kwa ajili ya wachimbaji wadogo ambapo leseni za uchimbaji mdogo zinaendelea kutolewa.

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha Uwezo wa Serikali Kusimamia Sekta ya Madini, ili kuimarisha usimamizi wa sekta ya madini, muundo wa Wizara ya Nishati na Madini umeimarishwa kwa kuipanua Idara ya Madini na kuendelea kuajiri wataalamu zaidi wa kusimamia sekta hiyo. Aidha, ofisi ya Afisa Madini Mkazi, Kigoma ilifunguliwa mwezi Septemba, 2007. Lengo ni kuongeza ufanisi katika usimamizi wa shughuli za madini na kuboresha utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa Shughuli za Madini Nchini, katika kuimarisha udhibiti wa shughuli za madini, Wizara ilianzisha kitengo cha ukaguzi wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini ya dhahabu katika migodi mikubwa (*Gold Audit Programme (GAP)*) mwezi Agosti, 2007. Kitengo hicho kilipewa majukumu ya msingi yafuatayo:- kuhakiki uzalishaji na biashara ya madini kwenye migodi mikubwa ya dhahabu kwa kuchukua sampuli za madini yanayozalishwa kwenye migodi hiyo na kuyafanya uchunguzi kwenye maabara ili kujua aina, ubora na wingi wa madini yaliyozalishwa; kuhakiki gharama za uwekezaji na uendeshaji wa migodi mikubwa ya dhahabu; na kufanya ukaguzi wa shughuli za utunzaji na ukarabati wa mazingira kwenye migodi mikubwa na kuhakiki gharama za utunzaji wa mazingira wa migodi hiyo. Kitengo hicho kina wafanyakazi 35 ambao wote ni Watanzania. Kati ya hao, wafanyakazi 25 walikuwa wameajiriwa na kampuni ya *Alex Stewart (Assayers) Government Business Corporation (ASAGBC)* na wafanyakazi waliobaki wameajiriwa na Wizara kutoka kwenye soko la ajira na wengine walipewa uhamisho wa ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, tangu kuundwa kwa *GAP*, kumekuwa na ufanisi katika kazi ya ukaguzi na udhibiti wa shughuli za madini na kujenga uwezo wa watumishi wake kwa kuwapatia uzoefu unaohitajika. Aidha, pamoja na uwepo wa ufanisi katika kazi za ukaguzi, gharama za kufanya ukaguzi zimepungua kuanzia shilingi bilioni 16.4 zilizokuwa zinalipwa kwa kampuni ya *ASAGBC* hadi shilingi bilioni 3.4 zinazotumiwa na Serikali kufanya kazi hiyo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na shughuli zinazofanywa na Kitengo cha *GAP*, Idara ya Madini imeimarisha shughuli zake za ukaguzi wa usalama, afya ya wafanyakazi

na utunzaji wa mazingira katika migodi mikubwa na midogo. Kazi hii hufanywa na wakaguzi wa migodi waliopo katika ofisi za madini za kanda.

Mheshimiwa Spika, Migogoro katika Shughuli za Madini, katika kufikia lengo la kuboresha sekta ya Madini ili iwe na mafanikio yanayotarajiwa, Ilani ya Uchaguzi inaitaka Serikali kuboresha mahusiano kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo. Wizara ilifanya tathmini na kuona kuwa migogoro mingi kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa inatokana na sababu kuu mbili: Kwanza, wachimbaji wasiokuwa na leseni kuendesha shughuli za uchimbaji madini ndani ya maeneo yanayomilikiwa na watafutaji na wachimbaji wakubwa wa madini. Pili, ni malalamiko ya fidia ndogo inayotolewa kwa wananchi wanaohamishwa makazi yao kupisha ujenzi wa migodi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hizo, Wizara imechukua hatua mbalimbali za kutatua migogoro hiyo ikiwa ni pamoja na: kuendeleza majadiliano ambapo wawekezaji wakubwa walikubali kuachia baadhi ya maeneo ya leseni katika maeneo ya Rwanagasa na Nyarugusu wilayani Geita; Makoro, Ngembambili na Kitai wilayani Mbinga; Seza Kofi na Mumbwi wilayani Handeni; na Winza wilayani Mpwapwa. Kuhusu fidia, tatizo hili linahitaji marekebisho ya Sheria ya Madini na Sheria ya Ardhi ili kurekebisha kasoro zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Uongezaji Thamani Madini, katika kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kuhusu kuhakikisha kwamba sehemu ya madini inayosafirishwa nje ya nchi yakiwa yameongezwa thamani kuongezeka kutoka asilimia 0.3 hadi asilimia 3.0 ifikapo mwaka 2010, Wizara inaendelea na mchakato wa kutunga Sheria ya Uongezaji Thamani Madini ikiwemo Usonara. Lengo kuu la Sheria hiyo ni kuhakikisha kuwa shughuli za uongezaji thamani madini ya vito na dhahabu zinakua kwa kasi na kusimamiwa ipasavyo ili kukuza mauzo nje ya nchi na kuongeza mapato na ajira nchini. Aidha, Wizara iliendelea kuimarisha *Arusha Gemstone Carving Centre* ili iweze kutoa mafunzo ya usanifu wa madini ya vito, miamba na usonara.

Mheshimiwa Spika, Kitengo Cha *Tansort*, Kitengo cha Uchambuzi na Uthamini wa Almasi (*Tanzania Government Diamond Sorting Organisation - TANSORT*) kiliendelea na majukumu yake ya kuchambua na kuthamini almasi zinazozalishwa katika mgodi wa Almasi wa Mwadui, uliopo Kishapu, Shinyanga, ili zipate bei nzuri na hivyo kuongeza mapato ya Serikali. Katika mwaka 2007, jumla ya karati za almasi 282,786 zilizalishwa ikilinganishwa na karati 272,204 mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, katika mchakato wa kukihamishia nchini Kitengo cha *TANSORT* kutoka Uingereza na kutokana na Kitengo kuwa na wafanyakazi wawili (2) tu Watanzania, Wizara ilipeleka wafanyakazi wanenye (4) kwenye mafunzo ya fani ya kuchambua na kuthamini almasi nje ya nchi ili kukijengea uwezo. Kwa sasa Wizara ipo kwenye hatua za kupata ofisi Jijini Dar es Salaam itakapowekwa *TANSORT* baada ya kurejeshwa nchini. Aidha, tathmini inafanyika kupata gharama halisi za kuweza kutekeleza uhamisho huo. Lengo la Wizara ni kuwa ifikapo mwaka wa fedha wa 2009/10 wataalamu wa kutosha watakuwa wamepatikana na bajeti itatengwa kutekeleza kikamilifu uamuza wa kukihamishia nchini.

Mheshimiwa Spika, Chuo Cha Madini, katika mwaka 2007/08, Chuo cha Madini kilitoa mafunzo ya ufundi sanifu katika kozi za utafutaji madini, uhandisi migodi na uchenjuaji madini. Mafunzo hayo yaliendeshwa kwa wanafunzi 71 wa mwaka wa kwanza, 67 wa mwaka wa pili na 32 wa mwaka wa tatu ambao ndio wahitimu kwa mwaka 2007/08.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kuwashukuru wenyе migodi nchini kwa kutoa ajira kwa wahitimu wa Chuo cha Madini. Aidha, nawashukuru wenyе migodi na shughuli za utafutaji mkubwa wa madini nchini kwa kutoa fursa kwa wanafunzi wa Chuo cha Madini kufanya mafunzo kwa vitendo katika migodi yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa Chuo cha Madini, Wizara katika mwaka 2007/08, iliendeleza ujenzi wa miundombinu ya Chuo ikijumuisha maktaba, karakana ya uchimbaji madini, nyumba za watumishi wa Chuo, zahanati na maabara mbalimbali. Chuo kina changamoto ya kutoa wahitimu wengi zaidi ili waweze kutosheleza soko la ajira. Pamoja na sababu nyingine changamoto hii inatokana na kutokuwepo kwa miundombinu ya kutosha ambapo idadi ya wahitimu wenyе taaluma ya ufundi sanifu katika sekta ya madini ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, Wakala Wa Jiolojia Tanzania – *GST*, shughuli za upimaji wa ramani za jiolojia zilifanyika katika maeneo ya Sikunge mkoani Tabora ambapo ramani tano (5) za jiolojia zilikamilika. Ramani maalumu kwa ajili ya kuvutia uwekezaji katika sekta ya madini kwa maeneo ya Mpanda-Kigoma, ukanda wa Ziwa Rukwa na ukanda wa Ziwa Victoria zilitengenezwa. Pia, ramani zinazoonesha maeneo yanayokumbwa na matetemeko ya ardhi mara kwa mara na maeneo yenye mionzi (*radiation*) zilichapishwa.

Mheshimiwa Spika, Wakala ulikamilisha ujenzi wa kituo kipyя cha kupima matetemeko katika eneo la *GST-Dodoma*. Tathmini ya matukio ya matetemeko ilifanyika katika vituo vya Kibaya, Kondoa, Singida, Dodoma, Manyoni na Mbeya. Pia, uchunguzi ulifanyika wa tukio la mlipuko wa volkano huko Oldonyo Lengai – Arusha. Viongozi wa maeneo yaliyoathirika na mlipuko huo walipewa ushauri juu ya kukabiliana na athari zitokanazo na tukio hilo, ikiwa ni pamoja na mikakati ya kuchukua tahadhari kwa ajili ya kuimarisha usalama.

Mheshimiwa Spika, sampuli za miamba ya dhahabu kutoka Nzuguni - Dodoma, Sambaru na Londoni – Singida, zilikusanywa na kazi ya kutafiti uchenjuaji bora wa sampuli hizo ilikamilika. Pia, uchunguzi wa nishati kutokana na maji moto katika Ziwa Ngozi, wilayani Rungwe ulifanyika na kubaini uwezekano wa kuwepo kwa mashapo katika ziwa hilo. Aidha, *GST* kwa kushirikiana na *STAMICO* na *BGR* ya Ujerumanii lichapisha kitabu cha mwongozo kwa wawekezaji katika madini ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa – *STAMICO*, kwa kutambua umuhimu wa Shirika la Madini la Taifa – *STAMICO* na kwa kuzingatia mapendekezo ya kamati mbalimbali, Wizara iliwasilisha kwenye ngazi za maamuzi pendekezo la

kuliondoa Shirika hilo kutoka orodha ya mashirika ya umma ya kubinafsishwa, na kulipa majukumu mapya ya ushiriki wa Serikali katika sekta ya madini na kuhudumia uchimbaji mdogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa liliendelea na shughuli za utafutaji wa madini ya dhahabu katika ukanda wa Ziwa Victoria kwa ubia na kampuni binafsi. Aidha, Shirika lilifanya utafiti wa awali wa madini ya fluorite katika eneo la Sengeri, Mkoani Mbeya na lilitoa huduma ya uchorongaji miamba katika mikoa ya Tanga, Lindi na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha *Seamic (Southern and Eastern African Mineral Centre)*, Kituo kimeendelea kutoa mafunzo katika sekta ya madini pamoja na kufanya uchunguzi na uchambuzi wa sampuli mbalimbali za madini katika maabara kwa ajili ya nchi wanachama ambazo ni Tanzania, Ethiopia, Angola, Kenya, Uganda, Komoro na Msambiji. Aidha, Kituo kina maabara ya mazingira ambayo ni mahsus kwa ajili ya uchunguzi na uchambuzi wa sampuli za mazingira katika maeneo ya uchimbaji mkubwa na mdogo wa madini.

Mheshimiwa Spika, Ajira na Maendeleo ya Watumishi, mwaka 2007/08, Wizara iliiimarisha uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa kuwapatia mafunzo watumishi, kuajiri watumishi wapya wa kada mbalimbali, kudurusu muundo wa Wizara, kushughulikia maslahi ya watumishi, kukarabati majengo na kununua vitendea kazi, kutoa elimu na vifaa vya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI, na kutoa huduma kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza kampeni ya kupima virusi vya UKIMWI kwa hiari zoezi lililoanzishwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete mwezi Julai, 2007, jumla ya watumishi 117 wa Wizara walijitokeza kupima na kujua hali ya afya zao katika zoezi la awali lililofanyika mwezi Desemba, 2007. Aidha, katika zoezi lingine lililofanyika mwezi Machi, 2008 jumla ya watumishi 82 walijitokeza kurudia kupima kwa lengo la kuhakiki majibu ya awali. Wizara ilifanikiwa kuwahamasisha watumishi walioambukizwa virusi vya UKIMWI kujitokeza na kupata huduma kulingana na Waraka wa Watumishi wa Umma Namba 2 wa Mwaka 2006 unaohusu huduma kwa watumishi wa umma wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Wizara imeendelea kutoa huduma ya mlo kamili pamoja na huduma nyingine kwa watumishi waathirika wa UKIMWI waliojitokeza. Aidha, warsha na semina kuhusu njia za kujikinga na kupunguza kasi ya maambukizi ya UKIMWI zilifanyika kwa waelimishaji rika na watumishi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango wa mafunzo wa mwaka 2007/08, uwezo wa utendaji kazi wa watumishi uliendelea kuimarishwa, ambapo watumishi 73 walipelekwa mafunzoni. Kati yao, watumishi 36 walishiriki mafunzo ya muda mfupi na 37 mafunzo ya muda mrefu. Aidha, Wizara iliajiri watumishi wapya 67 wa fani mbalimbali. Pia, jumla ya watumishi 61 wa kada mbalimbali walipandishwa vyeo.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Muundo wa Wizara yamefanyika ili kuendana na ongezeko la majukumu ya Wizara na kukabiliana na changamoto zilizopo.

Muundo mpya wa Wizara uliidhinishwa na Kamati ya Rais mwezi Agosti, 2007. Muundo huo umewezesha kuwepo ongezeko la vitengo viwili ambavyo ni Kitengo cha Sheria (*Legal Services Unit*), na Kitengo cha Usimamizi wa Mazingira (*Environmental Management Unit*). Aidha, Idara ya Madini itakuwa na sehemu tano ambazo ni:- Ukaguzi Migodi - *Mines Inspection*; Uendelezaji Wachimbaji Wadogo - Small Scale Mining Development; Usimamizi wa Baruti na Milipuko - *Explosive Management*; Biashara ya Madini na Uchumi - *Mineral Economics and Trade*; na Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini - *Licensing and Mineral Rights Management* zitakazosimamiwa na Makamishna Wasaidizi. Pia, ofisi za madini za kanda nane zitasimamiwa na Makamishna Wasaidizi.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2008/09 Sekta ya Nishati, pamoja na hatua nyingi zilizochukuliwa kipindi cha nyuma za kuboresha upatikanaji wa nishati, bado uwezo uliopo wa kupata nishati kwa wingi haujatumika vilivyo. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005 imeelekeza hatua zichukuliwe zenye lengo la kuongeza nishati, na hasa umeme na kuongeza uhakika wa upatikanaji na usambazaji wake ili uwafikie wananchi wengi zaidi. Ili kutekeleza azma hiyo na kuiwezesha sekta ya nishati kuwa endelevu na kuweza kuchangia ipasavyo katika kuendeleza uchumi wa Taifa maeneo ya kipaumbele katika utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa Wizara katika mwaka 2008/09 ni:- kutekeleza miradi chini ya Wakala wa Nishati Vijijini; kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya; kuimarisha mfumo wa uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme nchini; maandalizi ya kuunganisha gridi ya Taifa na nchi jirani; kukamilisha majadiliano na kampuni zilizoshinda zabuni ya kutafuta mafuta katika maeneo mbalimbali nchini; kukamilisha maandalizi ya sheria ya gesi asilia; kukamilisha majadiliano ya uendelezaji wa mradi wa gesi asilia ya *Mnazi Bay*; kuanza maandalizi ya miradi ya hifadhi na uagizaji wa mafuta wa pamoja (*bulk procurement*); kuhamasisha matumizi bora na uendelezaji wa nishati jadidifu na mbadala; kukamilisha mipango endelevu ya uendelezaji wa bayofueli nchini; kuhamasisha matumizi bora ya nishati; na kusimamia kazi ya mshauri wa namna ya kugawana gharama na mapato ya mafuta katika pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, miradi chini ya Wakala wa Nishati Vijijini, katika mwaka 2008/09, miradi itakayotekelawa chini ya Wakala wa Nishati Vijijini ni pamoja na kukamilisha upelekaji wa umeme katika makao makuu ya wilaya za Kilindi, Kilolo, Rufiji, Bahi, Uyui, Mkinga na Simanjiro. Aidha, baadhi ya miradi iliyoainishwa chini ya mradi wa *TEDAP* itatekelezwa kuititia Wakala chini ya usimamizi wa Wizara. Wakala pia utatoa mafunzo ya kuandaa na kuendeleza miradi ya nishati vijijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, miradi Iliyo Chini ya AfDB, katika kufanikisha lengo la Serikali la kusambaza umeme vijijini, Benki ya Maendeleo ya Afrika iliidhinisha takriban Dola za Marekani milioni 50 ili kuwezesha usambazaji wa umeme vijijini katika mikoa ya Arusha, Shinyanga na Mwanza. Ni matarijio ya Serikali kuwa fedha hizo zitasaidia katika kuongeza kasi ya upatikanaji wa huduma ya umeme vijijini katika mikoa husika. Kwa sasa mchakato unaendelea wa kumpata mtaalamu mshauri na matarajio ni kuwa atakuwa ameanza kazi ya kuandaa makabrasha ya zabuni na kushauri kuhusu uteuzi wa wakandarasi mwishoni mwa mwezi Julai, 2008.

Mheshimiwa Spika, tozo la Wakala wa Umeme Vijijini, fedha za utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme vijijini zitatokana na ruzuku ya Serikali, michango ya washirika wa maendeleo wa Serikali, wawekezaji binafsi pamoja na tozo mbalimbali. Waziri wa Nishati na Madini alisaini tangazo la kuanzishwa tozo ya asilimia tatu kwa kila uniti ya umeme unaozalishwa nchini kuanzia tarehe 1 Julai, 2008. Sheria ya Wakala inaruhusu tozo hadi asilimia tano. Tozo itaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kupeleka Umeme Makao Makuu ya Wilaya, Miji Mikuu ya Wilaya za Ngorongoro, Kibondo, Nanyumbu na Nkasi inatafutiwa fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango ya kupeleka umeme huko. Upembizi yakinifu wa kupanua gridi ya Taifa hadi kufikia mikoa ya Kigoma, Kagera na Rukwa umekamilika ambapo Wilaya za Kibondo, Kasulu na Bukombe zimejumuishwa. Mpango wa usambazaji umeme katika makao makuu ya wilaya utaendelea kutekelezwa kulingana na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha na Kuendeleza Mfumo wa Usafirishaji na Usambazaji Umeme, Miradi chini ya *TEDAP*, katika mwaka 2008/09, miradi mbalimbali ya kuboresha miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme itatekelezwa kutokana na misaada na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo. Mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia wa Dola za Marekani milioni 111.5 kuititia mradi wa *TEDAP* unalenga kuboresha miundombinu katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro; kusambaza umeme katika maeneo yaliyo nje ya gridi (*off-grid electricity distribution*); na kujenga uwezo wa Wakala wa Nishati Vijijini na wataalamu katika sekta ya nishati ikiwa pamoja na Wizara na *TANESCO*. Mchakato wa kupata wataalamu washauri wa kutayarisha makabrasha ya zabuni mbalimbali na kusimamia utekelezaji utakamilika mwishoni mwa Agosti, 2008.

Mheshimiwa Spika, Miradi chini ya *MCC* na *JICA*, Serikali kwa upande mwingine imepata kiasi cha Dola za Marekani milioni 206.5, kutoka *Millenium Challenge Corporation* (*MCC*) ya Marekani kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa umeme. Kiasi hicho kitatumika kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya usafirishaji na usambazaji umeme kwa mikoa sita (6) ya Tanga, Dodoma, Morogoro, Iringa, Mbeya na Mwanza kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 89.7. Kiasi cha Dola za Marekani milioni 53.7 kitatumika kujenga kituo cha kuzalisha umeme kwenye mto Malagarasi cha MW 8 kwa ajili ya Kigoma, Uvinza na Kasulu, na pia kujenga *sub-marine cable* kutoka Ras Kilononi, Dar es Salaam hadi kisiwa cha Unguja kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 63.1. Wataalamu washauri kwa ajili ya kusimamia Mradi wanatarajiwa kuanza kazi katikati ya Julai, 2008. Aidha, Shirika la Maendeleo la Japoni (*JICA*) limetoa Dola za Marekani milioni 10 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kuboresha miundombinu ya usambazaji umeme katika maeneo ya Masaki, Mikocheni na *Oysterbay* Jiji Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, gridi ya Kaskazini Magharibi ya njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 itaendelea kuimarishwa sanjari na miradi mipy ya laini ya

msongo wa kV 400 kutoka Iringa kupitia Dodoma, Singida hadi Shinyanga. Aidha, ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 inajengwa kupeleka umeme wa gridi katika migodi ya dhahabu ya Buzwagi na *North Mara* kwa makubaliano maalumu kati ya migodi hiyo na *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha Uzalishaji Umeme, katika kupanua wigo wa aina za vyanzo vya nishati kwa ajili ya kuzalisha umeme, mradi wa kuzalisha umeme wa MW 200 kwa kutumia makaa ya mawe ya Kiwira utaendelea kutekelezwa, ambapo yatafanyika maandalizi ya ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kV 220 kutoka Kiwira hadi Uyole, Mbeya itakayounganishwa kwenye Gridi ya Taifa. Mtambo wa Ubungo wa MW 100 utakaomilikiwa na *TANESCO* unategemewa kuanza uzalishaji umeme mwanzoni mwa Agosti, 2008. Mkataba wa *Alstom Power Rentals* uliokwisha muda wake Machi, 2008 haukuhuishwa na Mkataba wa Aggreko muda wake utaisha Novembra, 2008.

Mheshimiwa Spika, kufuatia utata uliojitokeza kuhusu uhalali wa Mkataba wa *Richmond/Dowans TANESCO/Serikali*, imechukua hatua ya kusitisha Mkataba huo kuanzia tarehe 1 Agosti, 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kuunganisha Gridi ya Taifa na Nchi Jirani, matayarisho yanaendelea ili kuziunganisha gridi za Zambia, Tanzania na Kenya. Mshauri mwelekezi ataendelea kuzishauri Serikali za nchi hizi tatu kwa lengo la kuanza utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia ndani ya Muungano, katika kuendeleza juhudhi za utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara inayohusika na Nishati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kukamilisha kazi ya mtaalamu atakayezishauri Serikali mbili ndani ya Muungano jinsi ya kugawana gharama na mapato endapo mafuta ya petroli au gesi asilia itagundulika upande mmojawapo wa Muungano. Mtaalamu huyo ni kampuni ya *AUPEC* kutoka Uingereza ambayo imeanza kazi mwezi Juni, 2008. Kazi hiyo itakamilika mwezi Novembra, 2008.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia kuanza na kukamilisha majadiliano na kampuni zilizoshinda zabuni ya kutafuta mafuta na gesi asilia katika maeneo mbalimbali nchini. Kampuni hizo ni *Tower Resources* ya London, *Ansco Petroleum (T) Limited*, *Motherland Homes Limited* ya India na *Beach Petroleum Limited* ya Australia zilizoshinda zabuni ya kutafuta mafuta na gesi asilia katika maeneo ya ziwa Eyasi-Manyara, Natron na bonde la Wembere, Ruhuhu, Malagarasi na eneo la kusini mwa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, Maandalizi ya Sheria ya Gesi Asilia, kufuatia kukamilika kwa rasimu ya mapendekezo ya kutunga Sheria ya Gesi Asilia, taratibu za kupata ridhaa ya ngazi za maamuzi zitaendelea ili Rasimu ya Sheria iweze kufikishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano mwezi Novembra, 2008.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Gesi Asilia ya *Mnazi Bay*, baada ya kukamilika na kuanza utekelezaji wa mkataba wa muda wa mpito wa ununuzi wa umeme kati ya

TANESCO na *Artumas*, majadiliano ya mkataba wa muda mrefu yatakamilishwa mwaka 2008/09. Kukamilika kwa majadiliano kutaharakisha usambazaji wa umeme katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Aidha, vipaumbele vya Serikali kuhusu matumizi ya gesi asilia ya ziada inayopatikana *Mnazi Bay* ni kutengeneza mbolea, saruji na kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi na Uagizaji wa Mafuta wa Pamoja, ili kuwa na uhakika wa kuwa na mafuta ya kutosha na ya dharura nchini, Wizara itakamilisha mchakato wa kuanzisha hifadhi ya mafuta. Aidha, *EWURA* itawasilisha mapendekozo kuhusu uagizaji wa mafuta wa pamoja (*bulk procurement*) kwa lengo la kuanza kutekeleza utaratibu huo mwaka 2008/09. *EWURA* imetoa tangazo la kukaribisha washauri wa kusimamia taratibu za *bulk procurement* na walioonekana kuwa na uwezo wameorodheshwa na watapewa makabrasha ya zabuni. Orodha hiyo inatarajiwu kuitishwa kwenye Bodi ya Zabuni ya *EWURA* katikati ya mwezi Julai, 2008.

Mheshimiwa Spika, Nishati Jadidifu na Mbadala, katika mwaka 2008/09, Mradi wa umemenuru utaendelea kutekelezwa kwa kuhamasisha soko la teknolojia hiyo katika mikoa ya Dodoma, Ruvuma, Singida na Tabora. Mafanikio ya mradi wa majoribio ya umemenuru Mkoani Mwanza yataendelea kutekelezwa (*replicated*) katika mikoa ya Mara, Kagera na Shinyanga kwa kutumia uzoefu uliopatikana mkoani Mwanza. Aidha, ukusanyaji wa taarifa za nishati ya upopo, jotoardhi, maporomoko madogomadogo ya maji kwa ajili ya uzalishaji umeme (*small-scale hydropower generation*) utaendelea ili kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika kuzalisha umeme. Pia, Serikali itaendelea kuhamasisha viwanda vyenye kuzalisha taka nyingi kama vya sukari na mba, kwa ajili ya kuzalisha umeme kwa kutumia taka husika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/09, Serikali kwa kushirikiana na *TANESCO* itaendelea kujadiliana na wadau wenye nia ya kuwekeza katika matumizi ya nishati ya upopo. Aidha, Wizara itaanza maandalizi ya kutengeneza Wind Atlas ili kurahisisha jitihada za wawekezaji katika nishati hiyo hapa nchini kwa kuwezesha kuwepo kwa takwimu sahihi za maeneo yanayoweza kuzalisha nishati ya upopo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/09, Serikali itaendelea na uandaaji wa mazingira ya kuwezesha uendelezaji endelevu wa bayofueli nchini na itakamilisha mwongozo wa uendelezaji bayofueli ikiwa ni utaratibu wa mpito kabla sera na sheria mahsus ya bayofueli kukamilika. Aidha, baadhi ya masuala ambayo yatazingatiwa ni mazingira, ardhi kwa mazao ya chakula, ajira, matumizi na wajibu wa wawekezaji kutoka nje katika kuhakikisha kwamba wananchi wananaufaika ipasavyo na faida zitokanazo na bayofueli.

Mheshimiwa Spika, Matumizi Bora ya Nishati, Serikali itaendelea kuhamasisha matumizi bora ya nishati katika sekta mbalimbali za uchumi ili kuokoa nishati, fedha na mazingira. Maandalizi kuhusu masuala ya uhamasishaji wa viwango vya ubora katika matumizi ya nishati na nembo majumbani na viwandani (*energy efficiency standards and labels*) yatafanyika.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuhamasisha wadau kuendeleza vyanzo vya nishati kwa kutumia teknolojia mbalimbali ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa matumizi ya bayogesi, *Liquified Petroleum Gas (LPG)*, gesi asilia, moto poa (*gel-fuel*), vitofali vya tungamotaka na makaa ya mawe (*biomass and coal briquettes*) kama mbadala wa kuni na mkaa. Lengo ni kuchangia katika kupunguza kasi ya ukataji miti na kuhifadhi mazingira. Aidha, Serikali kupitia mradi wa *SADC-ProBEC* kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuhamasisha matumizi endelevu ya kuni katika ukaushaji wa tumbaku na majiko bora ya kuni, hasa vijijini na katika taasisi kubwa kwa ajili ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini, Mipango ya Sekta ya Madini kwa Mwaka 2008/09, mipango ya sekta ya madini kwa mwaka 2008/09, itaendelea kuongozwa, pamoja na miongozo mingine, na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Mipango hiyo ni pamoja na kurekebisha Sera na Sheria ya Madini; kuendeleza majadiliano na kampuni za madini; kuanzisha mfuko maalumu wa kuwaendeleza wachimbaji wadogo; kukamilisha maandalizi ya Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali ya Madini (*Sustainable Management of Mineral Resources Project*) kusimamia utafutaji na uchimbaji wa urani (*uranium*) nchini; uimarishaji wa miundombinu katika ofisi za madini; na kuimarisha shughuli za ukaguzi wa gharama za uwekezaji na uendeshaji wa migodi mikubwa.

Mheshimiwa Spika, Sera na Sheria ya Madini, Wizara itakamilisha marekebisho ya Sera ya Madini ya mwaka 1997 na Sheria ya Madini ya mwaka 1998 kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM, changamoto za ukuaji wa sekta ya madini na mapendekezo ya kamati mbalimbali zilizoundwa na Serikali. Lengo ni kuwa na mabadiliko ya msingi katika uendeshaji wa sekta ikiwa ni pamoja na kupitia upya vivutio vya kodi na kuongeza ushiriki wa Serikali katika uwekezaji ili kuhakikisha manufaa kwa Taifa yanaongezeka. Marekebisho hayo pia, yatajumuisha kuirekebisha na kuipa majukumu mapya *STAMICO*.

Mheshimiwa Spika, Majadiliano na Kampuni za Uchimbaji wa Madini, Serikali itaendeleza majadiliano na Kampuni ya De Beers kupitia kampuni yake tanzu ya *Willcroft* katika mgodi wa almasi wa *Williamson Diamonds Limited (WDL)*. Katika majadiliano hayo Serikali itaangalia upya suala la hisa zake kwenye mgodi huo, ambapo kampuni ya Willcroft ina asilimia 75 ya hisa na Serikali asilimia 25. Aidha, Serikali itaendelea na majadiliano na kampuni ya AngloGold Ashanti kuhusu kuondoa kipengele cha asilimia 15 kwenye mtaji wa uwekezaji ambao haujarejeshwa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko Maalumu wa Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo, Suala la kuendeleza wachimbaji wadogo limepewa kipaumbele na Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kuelekeza kuwa wachimbaji wadogo wasaidiwe kupata mikopo na maarifa mapya katika fani ya uchimbaji madini. Katika kipindi cha fedha cha mwaka 2008/09 Wizara itaaniszha mfuko maalumu wa kuwaendeleza wachimbaji wadogo (*Mineral Revolving Fund*) ili utumike kuwakopesha mitaji wachimbaji wadogo na wafanyabiashara wa madini Watanzania. Aidha, Wizara itaendelea kuwahamasisha

wachimbaji wadogo nchini kuanzisha *SACCOS* ili waweze kukopeshwa mitaji na kuendeleza maeneo yaliyotengwa na kupimwa viwanja vya uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali ya Madini, ili Taifa liendelee kunufaika ipasavyo na rasilimali ya madini nchini, Serikali imekamilisha maandalizi ya awali ya mradi wa miaka mitano wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali ya Madini (*Sustainable Management of Mineral Resources*) utakaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Mradi huu pamoja na mambo mengine utasaidia kujenga uwezo wa Wizara kusimamia Sekta ya Madini, kusaidia kukuza shughuli za uongezaji thamani ya madini nchini na kutoa elimu kwa umma kuhusu shughuli za madini. Mwezi Januari, 2008 Benki hiyo ilitoa Dola za Marekani milioni 1.4 kwa ajili ya maandalizi ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Utafutaji na Uchimbaji wa *Uranium* Nchini, kuanzia mwaka 2007, kumekuwa na ongezeko kubwa la shughuli za utafutaji wa madini ya urani hapa nchini ambapo kampuni kubwa za kigeni zipatazo 20 zinaendelea na shughuli za utafutaji wa madini hayo katika mikoa ya Kusini na Kanda ya Kati. Madini haya ni ya kimkakati (*strategic*) kwa nchi nyingi duniani kwani hutoa nishati ya umeme ya uhakika. Aidha, madini haya yana madhara makubwa kwa binadamu kama uchimbaji wake usipozingatia taratibu maalumu. Serikali itaanza maandalizi ya kutunga sera na sheria zitakazosimamia utafutaji na uchimbaji wa urani nchini.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Ofisi za Madini, katika mwaka 2008/09, Serikali itaendelea na mpango wa kusogeza huduma za usimamizi wa sekta ya madini mikoani kwa kuanza kujenga ofisi tatu za kanda ya Kusini Magharibi - Mbeya, Kanda ya Ziwa - Mwanza na Kanda ya Kati - Singida pamoja na ofisi moja ya Afisa Madini Mkazi katika Wilaya ya Ludewa.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Gharama za Uwekezaji na Uendeshaji wa Migodi Mikubwa, ili kutekeleza azma ya Serikali katika kuimarisha shughuli za ukaguzi wa ghamara za uwekezaji na uendeshaji wa migodi na kuhakikisha kuwa migodi inachangia ipasavyo kwenye ukuaji wa uchumi, Serikali itaendelea kuimarisha Kitengo cha *GAP* ili kipate uwezo wa kukagua na kudhibiti madini yote yanayozalishwa hapa nchini na wachimbaji wakubwa na wadogo. Aidha, Idara ya Madini itaimarishwa kwa kutekeleza muundo wake mpya ili iweze kusimamia na kukagua masuala ya usalama na afya ya wafanyakazi migodini, utunzaji wa mazingira na utoaji wa huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Jiolojia Tanzania - *GST* katika mwaka 2008/09, Wakala utafanya kazi zifuatazo:- kutengeneza ramani katika maeneo ya Urambo – Tabora; kukamilisha ramani zilizopo ndani ya *Mtware Development Corridor*; kukusanya na kuhifadhi takwimu za matetemeko ya ardhi; kukarabati na kujenga miundombinu; kufanya utafiti maalumu wa makaa ya mawe; na kutoa mafunzo kwa wachimbaji madini wadogo wa Sambaru, Londoni na Nzuguni kuhusu namna bora za uchenjuaji wa dhahabu. Kwa kushirikiana na *NDC*, Wakala utafanya tathmini ya kina kubaini wingi na ubora wa madini ya chuma yaliyoko Liganga - Ludewa na makaa ya mawe yaliyoko Mchuchuma – Ludewa na Mbalawala - Mbinga. Aidha, Wakala

utawapeleka mafunzoni baadhi ya wafanyakazi hususan katika fani za jiofizikia, jiomelia na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Chuo Cha Madini, katika mwaka 2008/09, Chuo kinatarajia kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu ya Chuo na kuendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi zaidi ili Taifa liwe na mafundi sanifu wengi wenye kiwango bora cha ujuzi katika sekta ya madini. Kutokana na miundombinu iliyopo, Chuo kitaendelea kusajili wanafunzi 60 wa mwaka wa kwanza. Aidha, Chuo kitaandaa mpango mkakati wa kukiendeleza (*Corporate Strategic Plan*) ambao utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwaka 2009/10.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha *Tansort*, katika mwaka 2008/09, Kitengo cha TANSORT kitaendelea na kazi za kuchambua na kuthamini almasi za mgodi wa Mwadui. Aidha, Wizara imepanga kupeleka wafanyakazi wawili zaidi katika mafunzo ya fani ya kuchambua na kuthamini almasi. Lengo ni kukiongezea Kitengo uwezo wa kuchambua na kuthamini almasi zaidi. Kazi nyingine zilizopangwa ni kukamilisha tathmini na maandalizi ya kununua vifaa vitakavyohitajika ili kukiwezesha Kitengo kufanya kazi zake kwa ubora na ufanisi. Wizara inatarajia kuwa ifikapo mwaka wa fedha 2009/10 Kitengo kitakuwa kimehamia Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa – *STAMICO*, baada ya Serikali kutoa uamuvi wa msingi kuhusu hatima ya *STAMICO* inatarajiwa kwamba Shirika hilo litarekebishwa ili liweze kuwekeza kwenye sekta ya madini kwa niaba ya Serikali (*Government Investment Arm*) hususan, kwenye madini mkakati (*strategic minerals*). Aidha, Shirika hilo litahamasisha uwekezaji kwenye madini ya viwanda (*industrial minerals*) na kusimamia juhudzi za Serikali za kuwaendeleza wachimbaji wadogo nchini ikiwa ni pamoja na kutoa huduma za ugani.

Mheshimiwa Spika, *Southern and Eastern African Mineral Centre – SEAMIC* katika kipindi cha mwaka 2008/09, Kituo kitafanya kazi zifuatazo:- kutoa mafunzo yanayohusu sekta ya madini; kuchambua sampuli za madini; kufanya utafiti wa teknolojia bora za kuendeleza madini ya viwanda; na kutoa huduma za ushauri kwa nchi wanachama na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Ajira na Maendeleo ya Watumishi, katika mwaka 2008/09, Wizara inatarajia kuajiri watumishi 65 watakaogawanywa katika idara mbalimbali. Pia, Wizara imepanga kuwapeleka mafunzoni baadhi ya watumishi wake ili kuwajengea uwezo katika utaalamu mahsusili ili kutekeleza majukumu yao kwa umahiri na ufanisi zaidi. Aidha, mazingira ya kufanya kazi yataendelea kuboreshwa kwa kujenga na kukarabati majengo ya ofisi na kununua vitendeza kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mfumo wa utoaji huduma kwa wadau Wizara itaanza kutekeleza Mkataba wa Huduma kwa Mteja - *Client Service Charter* mwaka 2008/09. Mkataba huo haukuweza kuzinduliwa mwaka 2007/08 kutokana na mabadiliko ya msingi yaliyofanyika katika muundo wa Wizara na maoni yaliyotolewa na

wadau. Mkataba huo utazinduliwa katika mwaka 2008/09, baada ya kuzingatia mabadiliko na maoni ya wadau.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/09, Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano; kuimarisha mawasiliano kati ya Wizara na umma kuhusu huduma na taarifa mbalimbali za kisekta; kusimamia shughuli za manunuzi na utoaji wa zabuni unaozingatia sheria na kanuni; pamoja na kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Mapitio na Upimaji wa Utendaji Kazi wa Wazi (*OPRAS*) kwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/09, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi kwa lengo la kupunguza kasi ya maambukizi ya UKIMWI; kuwahamasisha watumishi kupima afya zao; kuanzisha mfumo wa mawasiliano wa namna ya kupashana habari kuhusu masuala ya UKIMWI; na kutoa huduma kwa watumishi walijitokeza wanaoishi na virusi vya UKIMWI kulingana na Waraka wa Watumishi wa Umma Namba 2 wa mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa Kimataifa, katika mwaka 2007/08, Wizara ya Nishati na Madini ilinufaika kwa misaada na ushirikiano kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo. Kwa niaba ya Serikali napenda kutoa shukurani kwa Serikali za nchi za Denmaki, Hispania, Japani, Kanada, Marekani, Norwe, Uswidi, Uhlanzi na Ujeruman. Vilevile, natoa shukurani kwa Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Rasilimali ya Ulaya, Umoja wa Nchi za Ulaya, pamoja na mashirika ya *ADF, GEF, IAEA, IDA, JICA, MCC, NDF, NORAD, Sida, UNDP, UNIDO* na *WEC*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, shukrani, naomba kutumia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Adam Kigoma Ali Malima, Mbunge wa Mkuranga na Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kwa ushirikiano wake mkubwa anaonipa katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara. Aidha, vile vile namshukuru sana Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Nazir Karamagi, (Mbunge). Aidha, nawashukuru Katibu Mkuu, Bwana Arthur Gwanaloli Mwakapugi, wakuu wote wa idara na vitengo, viongozi wa taasisi zilizopo chini ya Wizara wakiwemo wenyeviti na wajumbe wa Bodi na watendaji wakuu, kamati zinazosimamiwa na Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara ya Nishati na Madini pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati na Madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kutumia fursa hii kuwapongeza Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao za Bajeti, wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti) ya Utumishi wa Umma, Waziri wa Miundombinu, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa hotuba zao na ambazo zimetusaidia sana kuandaa bajeti yetu sisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, majumuisho, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha mapendekezo ya Bajeti ya shilingi 362,922,265,600/= kwa ajili ya matumizi

ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka 2008/09. Mchanganuo wa Bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:-

(a) Bajeti ya Maendeleo ni shilingi 320,067,385,600, kati ya fedha hizo shilingi 96,598,691,000 ni fedha za hapa na shilingi 223,468,694,600 ni fedha za nje; na

(b) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni shilingi 42,854,880,000 ambapo shilingi 3,305,639,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 39,549,241,000 ni matumizi mengineyo (*OC*).

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu napenda nitoe shukrani Mheshimiwa Dr. William Shija, ambaye kwangu mimi ni faraja kubwa kusoma bajeti hii kwa mara ya kwanza akiwa mionganoni mwa wageni wetu waalikwa. Dr. Shija ndiyo Mbunge ambaye mimi amenirithisha mikoba ya kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Sengerema nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kwa kuwasilisha hotuba katika muda wake na kwa ufasaha mzuri sana.

Sasa ni zamu ya Mwenyekiti au mwakilishi wa Kamati ya Nishati na Madini. Anakuja tena Mheshimiwa Christopher Ole- Sendeka, kwa niaba ya Mwenyekiti na Kamati. Karibu sana. (*Makofi*)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE- SENDEKA – (K.n.y. WILLIAM H. SHELUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI): Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2007/08 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2007, naomba kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Nishati na Madini, kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha taarifa hiyo, naomba kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Simanjiro, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutekeleza ahadi yake aliyoitoa Mererani ya kusema kwamba miili ya Watanzania waliopoteza maisha kwenye migodo ya Mererani itatolewa na itazikwa kwa heshima stahiki. Kwa maana hiyo, nina kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais. Kama mnavyojua zoezi hilo lilikuwa zito, kwa hiyo, nina kila sababu pia ya kuwashukuru wale waliowezesha kwa fedha wakiwemo Mheshimiwa Adam Malima, aliyeongoza harambee ya kupata fedha hizo, Mheshimiwa Reginald Mengi, aliyetao milioni 25, Waheshimiwa wengine kama *Standard Charter, NMB, Barricks*, Bunge lako Tukufu ambalo lilichangia zaidi ya milioni 17 na wana Apolo amba walishiriki wenyewe kudumbukia kule shimonii na kuwatoa wale ndugu zetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama mnavyojua kuwa Kamati hii ni mpya ambayo majukumu yake hapo awali yalikuwa yakitekelezwa na Kamati ya Uwekezaji na Biashara. Hivyo basi, kabla ya kupitia na kujadili Bajeti ya Wizara hii, Kamati yangu ilipata fursa ya kujielimisha kuhusu kazi na majukumu mbalimbali yanayotekerezwa na Wizara ya Nishati na Madini pamoja na taasisi zilizo chini yake. Katika hatua hiyo, Kamati yangu ilipata fursa ya kujifunza mambo muhimu yafuatayo:-

- Dira na madhumuni ya Wizara;
- Uongozi na Muundo wa Wizara;
- Majukumu ya Idara na Vitengo vya Wizara;
- Maeleo kuhusu Taasisi zilizo chini ya Wizara na Utekelezaji wa Mpango; na
- Bajeti ya Mwaka 2007/08.

Mheshimiwa Spika, mbali ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini, kwa mwaka wa fedha uliopita, kama inavyooleezwa katika kifungu cha pili hapa chini na kuendelea, Kamati ilipokea maeleo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2008/2009, yakiwemo matarajio ya Matumizi na Mpango wa Maendeleo. Aidha, Kamati ilifahamishwa juu ya kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka huo.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2007/2008, iliyokuwa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, ilitoa maoni na ushauri juu ya utekelezaji katika maeneo mbalimbali. Wakati ikipitia Taarifa ya Wizara, Kamati yangu iliridhika na utekelezaji wa baadhi ya ushauri uliotolewa na Kamati hiyo. Aidha, kwa maeneo ambayo utekelezaji wake haukufanyika kwa ufanisi Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa utekelezaji katika maeneo hayo ufanyinywe kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2007/08, yafuatayo yalipangwa kutekelezwa:-

- Kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya za Mbinga, Simanjiro, Kilolo, Ludewa, Kilindi, Bukombe na Serengeti. Aidha, maeneo mengine ni pamoja na: Kagera, Msonga, Magindu, Itiryo (Tarime), Mbewewe, Malya/Sumve, Ukerewe, Ihanja, Bukene, Mvumi - Mlowa, Mchinga A na B, Berega, Urambo na Mgwash ;

- Kupanua na kukarabati Gridi ya umeme ya Taifa, Miradi ya kuzalisha umeme wa dharura ;

- Kuhamasisha uwekezaji katika sekta za nishati na madini kwa lengo la kuongeza mchango wa sekta hizo katika pato la Taifa ;

- Uhamasishaji na uendelezaji wa vyanzo vya nishati jadilifu na mbadala;

- Kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo vingine vya nishati ikiwa ni pamoja na gesi asilia na makaa ya mawe ;

- Ukamilishaji wa majadiliano ya Programu ya kuendeleza na Kupanua Wigo wa Upatikanaji na Usambazaji Umeme Nchini (*Tanzania Energy Development and Access Projects*) ;

- Kutoa ruzuku kwa Taasisi za Serikali zinazosimamia sekta za umeme na mafuta;

- Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini kwa lengo la kuongeza mchango wa sekta ya madini katika pato la taifa ;

- Utekelezaji wa mkakati wa kusaidia na kuendeleza wachimbaji wadogo wa madini;

- Ujenzi wa miundombinu katika Chuo cha Madini – Dodoma ;

- Kudurusu sera na sheria za sekta za nishati na madini; na

- Kutoa elimu ya UKIMWI kwa watumishi wa Wizara na wachimbaji wadogo wa madini.

Mheshimiwa Spika, mafanikio katika Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2007/2008. Katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2007/2008, Wizara ilipata baadhi ya mafanikio yafuatayo:-

- Kuanzishwa kwa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) mwezi Octoba 2007 ;

- Kupitishwa kwa Sheria ya Umeme na ya Petroli na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Aprili, 2008 ;
 - Kukamilika kwa ujenzi wa mtambo unaomilikiwa na Serikali, wenyewe uwezo wa kuzalisha umeme *MW 100* unaotumia gesi katika eneo la Ubungo;
 - Kuchimbwa kwa visima viwili vya gesi na Kampuni ya Ndovu *Resources/Aminex* kwenye kisiwa cha Kiliwani Kusini mwa Kisiwa cha Songosongo ambavyo vimeonyesha kuwa na gesi nyingi;
 - Kuchimbwa kwa Kisima kimoja Na.10 katika Kisiwa cha Songosongo na Kampuni ya *Pan African Energy* (T) Ltd. Kisima hiki kimeongeza upatikanaji wa gesi asilia inayotoka katika Kisiwa cha Songosongo ;
 - Kuanza kutumika kwa gesi katika viwanda vitatu vya *Serengeti Breweries, Nam Park* na Namera *Textiles*. Hii inafanya idadi ya viwanda ambavyo vinatumia gesi ya Songosongo kwa sasa kufikia 19;
 - Kuandaliwa kwa Rasimu ya Mkataba wa Uendeshaji wa Mradi wa Gesi Asilia ya Mnazi Bay baina ya Serikali na Kampuni ya Artumas;
 - Kukabidhi rasmi kazi na vitendea kazi vya maabara Serikalini mwezi Agosti, 2007 kwa Kampuni ya *Alex Stewart (Assayers) Government Business Corporation (ASAGBC)*. Baadaye Serikali iliamua kuwa kazi ya ukaguzi wa migodi mikubwa na udhibiti wa uwekezaji, itafanywa na Wizara ya Nishati na Madini ; na
 - Kuanza kazi kwa Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni (*Mining Cadastre Information Management System – MCIMS*) na kuunganishwa kwa mfumo huo kwenye Ofisi 22 za madini za kanda.
- Mheshimiwa Spika, changamoto katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2007/2008, licha ya mafanikio yaliyopatikana, katika kipindi cha mwaka 2007/2008 changamoto zifuatazo zilijitokeza:-
- Kuchelewa kutekelezwa kwa miradi ya maendeleo kulikotokana na ucheleweshwaji wa fedha kutoka Hazina katika kipindi cha robo ya kwanza na ya nne;
 - Kuendelea kupanda kwa bei ya mafuta kunakosababisha kupanda kwa gharama za uzalishaji umeme kwenye vituo vinavyotumia mafuta;
 - Kuongezeka kwa mahitaji ya umeme nchini;
 - Kukosekana kwa maandalizi na uvezeshaji wa wachimbaji wadogo wa madini;
 - Ugawaji wa maeneo madogo kwa wachimbaji wadogo ikilinganishwa na maeneo wanayopewa wachimbaji wakubwa; na

- TANESCO kuendelea kubeba mzigo mzito wa kulipa “capacity charge” zinazotokana na wazalishaji binafsi wa umeme.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Kamati yangu inatambua nafasi na umuhimu wa Wizara ya Nishati na Madini katika maendeleo ya rasilimali za nishati na madini hasa katika kutoa huduma bora na kuweka mazingira wezeshi kwa wadau. Hata hivyo, utekelezaji wa malengo ya Wizara pamoja na taasisi zake sio wa kuridhisha kutokana na Serikali kuitengea fedha kidogo. Hivyo basi, ili kuiwezesha Wizara kufikia malengo yaliyowekwa ya kuendeleza na kusimamia rasilimali za madini, mafuta na gesi, Kamati yangu inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*). Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge mwaka 1972, (*The State Mining Corporation (Establishment) Order 1972*) chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1969 (*The Public Corporation Act 1969*). Shirika hili limepewa majukumu ya kusimamia madini. Usimamizi huo, ni pamoja na kufanya utafiti, kuchimba na kuchoronga miamba kwa wachimbaji madini. Hivyo, Shirika hili ni chombo muhimu cha kusimamia rasilimali ya madini hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1992 Shirika hili limekuwa likijiendesha lenyewe bila ruzuku kutoka Serikalini. Miongoni mwa kazi zilizofanywa kwa ufanisi, ni pamoja na uendelezaji wa maeneo ya madini kwa ubia na Kampuni kama vile *Tan Can Mining Company Limited, TANZAM 2000, Geo Can Resources Limited* zote kutoka Canada.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu, Shirika hili katika jitihada zake lenyewe, limeweza kuandaa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano na pia limetengeneza Mkakati wa kusaidia Wachimbaji Wadogo wa Madini. Hii inadhihirisha wazi kwamba Shirika hili linaweza kufanya vizuri zaidi kama litawezeshwa. Kamati inasisitiza kwamba, wakati umefika, kwa Serikali kufikia muafaka katika maamuzi yake ya kuliondoa Shirika hili kwenye orodha ya mashirika yanayobinafsishwa (*despecify*) kama ilivyoshauriwa na Kamati iliyotangulia.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua jitihada zinazoonyeshwa na Shirika hili Kamati inaishauri Serikali itekeleze yafuatayo ili kuweza kulinusuru Shirika hili:-

- Waraka ulioandaliwa wenyе mapendekezo kuhusu kutolibinafsisha (*despecify*) Shirika, ufanyiwe kazi haraka ili Shirika liweze kuwa na utaratibu mzuri wa kufanya kazi zake;

- Sheria inayounda Shirika hili ifanyiwe marekebisho haraka ili kuliwezesha Shirika kutekeleza majukumu yake kulingana na hali halisi ya sasa; (*Makofi*)

- Serikali ilipe haraka sana deni la shilingi Milioni 171 ambalo *STAMICO* inaidai iliyokuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (*PSRC*), kwa takribani miaka 10. Kamati inasisitiza deni hilo lilipwe pamoja na riba ili fedha hizo zisaidie Shirika kulipa madeni linayodaiwa na Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma (*PPF*) na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) kama viinua mgongo kwa wafanyakazi wake;

- Mkakati wa Kusaidia Wachimbaji Wadogo ulioandaliwa na *STAMICO* na kukabidhiwa kwa Wizara ya Nishati na Madini, ufanyiwe kazi haraka ili Wachimbaji hao waweze kufaidika na mpango huo. Katika kutekeleza makakati huo, Kamati inaishauri Serikali iliwezeshe Shirika kifedha ili lifanye tathmini ya kijiolojia ya maeneo yenye madini. Aidha, Shirika liweze kueneza na kuratibu uenezaji wa teknolojia za uchimbaji na uchenjuaji wa madini kwa njia ya mafunzo, matumizi na matengenezo ya vifaa mbalimbali, ukodishaji wa vifaa, mitambo na uendeshaji wa vituo vya uchenjuaji, pamoja na kutoa ushauri wa masoko na bei za madini kwa Wachimbaji Wadogo; (*Makofi*)

- Mfumo wa hisa (*share structure*) uliopo ambao uliwekwa tangu mwaka 1972, umepitwa na wakati. Kamati inashauri Serikali kurekebisha mfumo huo ili Shirika liweze kuwekeza na kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha; na

- Mwaka 2007, Shirika liliomba kibali Serikalini ili kuliwezesha kukopa fedha kutoka Benki ya Taifa ya Biashara (*NBC*) ili kununua mtambo wa kuchoronga miamba, lakini kibali hicho hakijatolewa hadi sasa. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha utoaji wa kibali hicho ili Shirika liweze kutimiza malengo yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Umeme Tanzania – *TANESCO*. Shirika la Umeme Tanzania lilianzishwa mwaka 1964 chini ya Sheria ya Umeme ya mwaka 1931. Shughuli kubwa za Shirika hili ni kuzalisha/kufua, kusafirisha, kusambaza na kuuza umeme Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya malengo ambayo Shirika limejiwekea ili kutekeleza dira na dhima ni kama ifuatavyo:-

- Kuboresha hali ya kifedha ya Shirika kwa kuongeza makusanyo ya fedha kutokana na mauzo ya nishati kwa wateja na kupunguza hasara zitokanazo na upotevu wa nishati ya umeme;

- Kuongeza kasi ya kusambaza nishati ya umeme ili kusaidia kukuza uchumi wa Taifa; na

- Kuongeza uwezo na vyanzo mbadala vya kufua umeme ili kuondokana na mgao wa umeme mara kwa mara katika gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa malengo hayo utategemea namna ambavyo Serikali itazingatia vipaumbele vilivyopo katika maendeleo ya nchi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali izingatie yafuatayo:-

- Gharama za kuendesha Shirika hili ziko juu sana kutokana na hali halisi ya uchumi. Kwa hiyo, Kamati inaishauri Serikali kulitafutia Shirika mtaji ili liweze kujiimarisha kwa kupanua njia kuu za kusafirisha umeme na kufanya matengenezo muhimu ya kusafirishia na kusambaza umeme nchini;

- Kukamilisha kwanza miradi ya umeme iliyokwishaanza kabla ya kuibua miradi mingine mipyä. Aidha, Kamati imebaini kwamba fedha za miradi ya maendeleo zinachelewa kutolewa na Hazina. Tatizo hili halihusu Wizara hii tu, bali Wizara/Ofisi nyingine ikiwemo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), hivyo Kamati inaishauri Serikali kuhakisha kuwa, fedha zinazotengwa kutekeleza miradi ya umeme, zinatolewa kwa wakati unaotakiwa ili miradi husika iweze kutekelezwa kwa wakati;

- Fedha za kutosha zitengwe kwa ajili ya kujenga miradi ya kuzalisha umeme hasa wakati wa dharura ili kuondokana na utaratibu uliopo wa kununua umeme kwa gharama kubwa pindi itokeapo dharura. Vilevile, *TANESCO* iwezeshwe kwa kuwekewa dhamana ya mikopo kutoka Taasisi za fedha ili ijenge uwezo wa kumiliki mitambo ya kuzalisha umeme wa dharura;

- Kwa kuwa yanatokea matatizo mbalimbali ya kuibiwa kwa mafuta ya transfoma, nyaya za umeme na uharibifu wa miundombinu ya umeme, Kamati inapendekeza kuwa *TANESCO* ione uwezekano wa kuingia mikataba na Serikali za Vijiji ili iweze kusaidiwa kulinda mali zake na kuzuia uharibifu huo; na

- Pamoja na Kamati kuendelea kuikumbusha Serikali haja ya kupunguza gharama za kuendesha *TANESCO* kuititia hatua mbalimbali, Kamati inaomba kufahamu Serikali imefikia wapi katika kutekeleza Mpango wa Kuimarisha Hali ya Kifedha ya *TANESCO* (*Financial Recovery Plan 2006 – 2010*). Mtazamo wa Kamati ni kwamba Mpango huu utahusisha kurekebisha bei za umeme ili ziweze kurudisha gharama halisi za uendeshaji wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, tutakumbuka kuwa Mwezi Aprili 2008, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Umeme yenye lengo la kufungua milango kwa sekta binafsi kuzalisha umeme sambamba na *TANESCO*. Msingi wa sheria hii, ni kuleta ushindani kati ya makampuni yanayotaka kuzalisha umeme nchini. Kwa msingi huo, Kamati yangu inaendelea kuisisitiza *TANESCO* kukamilisha Mpango Maalum wa Umeme (*Power System Master Plan - PSMP*) na kuikumbusha Serikali kutekeleza ushauri ilitolewa na Kamati kwa lengo la kuliandaa Shirika hili kuingia katika ushindani huo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati yangu, inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa maafikiano baina ya Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Nishati na Madini kuhusu kupitisha umeme katika Daraja la Mkapa lililo katika Mto Rufiji, yanafikia mwisho wake ili umeme uweze kuvushwa na kufika katika miji ya Ikwiriri, Kibiti, Bungu hadi Mkuranga. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Fund (REF)*). Mfuko wa Nishati Vijijini, ulianzishwa kwa Sheria ya Nishati Vijijini ya Mwaka 2005. Kifungu cha 19 (d) cha Sheria hiyo kinaainisha kuwa, pamoja na bajeti ya Serikali, kutakuwa na tozo ya asilimia hadi tano kutokana na mapato ya uzalishaji wa umeme kama chanzo cha Mapato ya Mfuko huo. Tozo hii inajumuisha wazalishaji wote wa umeme wenye leseni. Kamati imeshangaa kuona kwamba miaka mitatu imepita tangu kupitishwa kwa sheria hiyo, utaratibu wa kuanza kwa tozo hizo bado haujaanza. Kwa sababu hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuwa, utaratibu huo uanze haraka iwezekanavyo ili kuboresha maendeleo ya nishati nchini, hususan vijijini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Agency (REA)*). Wakala wa Nishati vijijini (*REA*), ulianza kazi rasmi Oktoba, 2007. *REA* inaratibu utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini (*REF*). *REA* inawezesha miradi ya nishati vijijini kupitia makundi matatu yafuatayo:- Miradi ya Gridi (*grid connection*), Waendelezaji Miradi (*project champions*) na Miradi itakayoibuliwa na *REA* (*propriety rural electrification projects*).

Mheshimiwa Spika, tathmini ya vyanzo vya nishati vijijini iliyofanyika mwaka 2005 imeainisha rasilimali za nishati zilizopo vijijini kama vile; upепo, maporomoko madogo ya maji yenye uwezo wa kuzalisha MW 39.5, joto ardhi yenye uwezo wa kuzalisha MW 20 – 30, mionzi ya jua na tungamotaka (*biomass*). Kamati imeona kuwa hii ni hatua nzuri, hivyo inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inatumia tathmini ya vyanzo hivyo katika kuboresha upatikanaji wa nishati ya umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini Dodoma kilianzishwa rasmi mwaka 1982. Chuo hiki kinatoa mafunzo ya ufundi sanifu katika sekta ya madini ikiwa ni pamoja na fani ya Uhandisi wa Migodi, Jiolojia, Utafutaji wa Madini, Uhandisi wa Uchenjuaji Madini na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau wa madini kama wachimbaji wadogo wa madini na mafundi sanifu walio kazini. Pia chuo hiki hufanya utafiti wa shughuli za madini na kutoa ushauri katika sekta ya madini kwa wadau wa madini.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatambua umuhimu wa Chuo hiki katika kuendeleza taaluma katika masuala ya madini. Kutokana na umuhimu huo, Kamati imebaini kuwa Chuo hiki kimetelekezwa na kuonekana kama hakipo kabisa kutokana na kutopewa uangalizi wa karibu na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini mapungufu yafuatayo katika Chuo hicho:-

- Kukosekana kwa muundo unaoelewaka;
- Upungufu wa Walimu na Watumishi mbalimbali;
- Kutokuwa na miundombinu ya kutosha;
- Ukosefu wa vitendea kazi;
- Bajeti isiyokidhi mahitaji; na
- Chuo kutokuwa na Mpango Mkakati (*Strategic Plan*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu huo, hasa ikizingatiwa kuwa hivi sasa sekta ya madini inakua na inahitaji uwiano wa Mhandisi kwa Mchimbaji kuwa 1:25, Kamati yangu inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

- Serikali ikamilishe mchakato utakaosaidia kubadili Chuo na kuwa Wakala (*Executive Agency*);
 - Serikali kuandaa Mpango Mkakati utakaotoa mwongozo wa namna Chuo hiki kitakavyotakiwa kutekeleza majukumu yake; na
 - Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuboresha miundombinu na kuongeza mitaala kama vile taaluma kuhusu uchimbaji/utafutaji wa mafuta pamoja na ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) lilianzishwa mwaka 1969 chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma Na.17 ya mwaka 1969. Majukumu ya Shirika ni kutafuta na kusimamia shughuli za mafuta nchini kwa maslahi ya Taifa. Kamati imefarijika kuona sasa Serikali imeridhia kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Mafuta na *TPDC* kuingizwa katika utaratibu wa *Retention* kuanzia mwaka wa Fedha 2008/09. Kwa msingi huo, Kamati inaikumbusha Serikali kuhakikisha kwamba inatenga fedha za kutosha ili kuiwezesha *TPDC* kuwekeza kwenye shughuli za mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TPDC* kupewa asilimia 50 ya mauzo ya gesi asilia, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Waraka ulioandaliwa kwa lengo la kutekeleza azma hiyo ufanyiwe kazi haraka ili Shirika liweze kushiriki kikamilifu katika miradi ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Petroli ya mwaka 2008, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha taratibu zake za kuifanya *TPDC* kuagiza mafuta kwa wingi (*Bulk Procurement*). Utaratibu huo uanze kutumika haraka iwezekanavyo ili kusaidia kupunguza ongezeko la bei ya mafuta inayopanda siku hadi siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali zinazolikabili Shirika hili. Changamoto hizo zimeelezwa katika Kiambatisho Na. 1 kilichowekwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Madini. Kamati inatambua umuhimu wa kuwepo kwa Mfuko wa Maendeleo ya Madini (*Mineral Development Fund*) kama moja ya Mikakati ya kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo wa Madini. Kamati pia imefarijika na hatua zinazochukuliwa na Serikali kama vile kuanza mchakato wa kuanzisha Mfuko huo pamoja na Mfuko wa Madini wa Kuwezeshana (*Mineral revolving Fund*) ambayo yote itakuwa chini ya Wizara ya Nishati na Madini. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha uanzishwaji wa Mifuko hiyo unalenga wahusika na si kutumiwa vinginevyo au kunufaisha wenyе uwezo zaidi ya Wachimbaji Wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuanzishwa kwa Mifuko hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatoa elimu ya kutosha kwa Wachimbaji Wadogo kuhusu Mifuko hiyo pamoja na kuwepo kwa fursa za kiuchumi zitakazowanufaisha katika biashara ya madini hususan kwenye kuongeza thamani ya madini yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kusaidia wachimbaji wadogo, Kamati inashauri kuwa *STAMICO* ihusishwe katika kusaidia Wachimbaji Wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa Ofisi za Madini za Kanda, zinaimarishwa ili ziweze kuwahudumia wachimbaji wadogo kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika madini. Kamati inatambua umuhimu wa uwekezaji wa madini katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo. Uwekezaji huo, huchochea maendeleo hususan katika maeneo yenye migodi. Pamoja na umuhimu huo, Kamati yangu imebaini kuwepo kwa matatizo kadhaa ambayo yanawakumba wananchi walioko katika maeneo hayo kama vile:-

- Migogoro baina wenyе migodi na wananchi;

- Migogoro baina ya wachimbaji wadogo na wakubwa;
- Wananchi kulipwa fidia ndogo au kutolipwa kabisa;
- Migogoro kwenye maeneo mapya yenyе madini yanayoibuliwa na wananchi; na
- Kuongezeka kwa maambukizi ya magonjwa kama vile UKIMWI na kadhalika. Mfano Songsongo ambapo Kamati ilitembelea. Kamati inaishauri Serikali kutafuta suluhu ya matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, Kamati inapenda kuishauri Serikali kurekebisha Sheria ya Madini ili kuzuia wawekezaji wasio Watanzania kuwekeza kwenye uchimbaji wa madini ya vito (*gemstones*) isipokuwa kwa kuingia ubia wa asilimia 50 kwa 50 na Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kwamba wawekezaji hulipa mrabaha Serikalini, hata hivyo kiasi cha mrabaha wanacholipa wawekezaji katika migodi ni kidogo na hakiendani na thamani ya madini wanayopata wachimbaji. Kamati inaishauri Serikali ipitie upya viwango vya mrabaha ili viweze kuchangia kuongeza Pato la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika mafuta na gesi mafuta na gesi ni rasilimali muhimu sana katika kuleta maendeleo ya nchi iwapo itachimbwa na kutumika ipasavyo. Utafutaji gesi katika mwambao wa Pwani, umekuwa ukiendelea kwa muda mrefu kwa makampuni toka nje yakishirikiana na *TPDC*. Kwa sasa gesi imevumbuliwa katika maeneo ya Mnazi Bay, Songsongo na Mkuranga na tayari imeanza kuvunwa katika baadhi ya sehemu za Mnazi Bay na Songsongo. Kamati imefarijika na juhudzi zinazoendelea katika utafutaji na uzalishaji wa gesi katika maeneo hayo.

Aidha, kwa maeneo kama vile Mnazi Bay ambako gesi imevumbuliwa na hivi sasa Rasimu ya Mkataba wa Uendeshaji wa Mradi wa umeme kwa kutumia Gesi Asilia ya Mnazi Bay na Kampuni ya Artumas imeandaliwa. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha Mkataba huo haraka ili umeme uanze kuzalishwa na kusambazwa katika maeneo yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefarijika na juhudzi zinazoendelea katika utafutaji na uzalishaji wa gesi katika Kisiwa cha Songsongo. Kwa kutambua juhudzi hizo, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka mchakato wa kuanzishwa kwa Sheria ya Gesi ili utafutaji na matumizi ya gesi hiyo uweze kudhibitiwa kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati inatambua mchango wa *TPDC* katika sekta ya mafuta na gesi. Hata hivyo, *TPDC* haina uwezo mkubwa wa kuwekeza katika shughuli hizi. Kamati yangu inaishauri Serikali kuiwezesha *TPDC* kifedha ili ipate mtaji wa kuwekeza kwenye miradi ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi. Sambamba na kupatikana kwa fedha hizo Serikali iboreshe sera za gesi na mafuta ambazo zitajenga mazingira mazuri ya uwekezaji katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Kisiwa cha Songsongo, kina kiasi kikubwa cha gesi ambayo ina manufaa makubwa kwa viwanda na watumiaji wa kawaida. Mradi wa Gesi ya Songsongo, miundombinu yake ya kuleta gesi Dar es Salaam ni finyu sana. Kamati inashauri kuwa mradi huo upanuliwe zaidi ili watumiaji wengi waweze kufaidika nao. Aidha, imefahamika kuwa wananchi wa Songsongo hawanufaiki na gesi hiyo. Kamati inashauri kuwa uandaliwe utaratibu utakao wanufaisha wananchi wa eneo hilo. Vilevile, mazingira ya eneo hilo yaboreshwe ili yaendane na tasfiri halisi ya thamani ya gesi inayovunwa kisiwani hapo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wenzangu kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuunda Tume ya kuchunguza Mikataba ya Madini iliyoongozwa na Jaji Mark Bomani. Kamati inatambua na kuthamini juhudhi za Mheshimiwa Rais katika kusimamia rasilimali za nchi, hivyo imeona kuwa hiyo ni hatua nzuri katika kuhakikisha kuwa wananchi na nchi kwa ujumla inanufaika na madini yaliyopo. Ni matarajio ya Kamati kwamba matokeo ya taarifa hiyo yatasaidia kuleta maendeleo hususan katika maeneo ya madini na kukuza Pato la Taifa. Tunashukuru kuwasilishwa kwa Taarifa ya Kamati ya Bomani katika Bunge letu tukufu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo mwanzo kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa na Taasisi/Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii, Kamati yangu inaendelea kusisitiza juu ya umuhimu wa kuziwezesha *STAMICO*, *TANESCO*, *TPDC*, Chuo cha Madini na Wakala wa Geolojia Tanzania (*GST*), ili waweze kutekeleza vema majukumu yao na kutimiza malengo katika kusimamia rasilimali husika zilizopo nchini. Maoni ya Kamati ni kwamba, Serikali ione umuhimu wa chombo kama *STAMICO* kuendelea kuwepo ili kuongeza manufaa ya madini kwa Taifa na hasa kupitia Wachimbaji Wadogo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali iitumie *STAMICO* kuwekeza katika madini kwa kuingia ubia na Wawekezaji wa Madini ili iweze kuangalia kwa ukaribu kiasi cha madini kinachopatikana na hivyo kuwa katika nafasi nzuri ya kufanya tathmini ya mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuishukuru Serikali hususan *TANESCO* kwa kutekeleza moja ya mapendekezo yaliyotolewa na Kamati Teule ya Bunge kuhusu kuvunja mkataba kati ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC*, uliorithiwa na Kampuni ya kuzalisha umeme ya *DOWANS Holdings S.A.* Huu ni uamuvi wa busara na wa kijasiri. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu shughuli zilizopangwa kufanywa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2008/2009, Wizara ya Nishati na Madini imetengewa jumla ya shilingi 362,922,265,600.00. Kati ya fedha hizo shilingi 46,160,519,000 kwa ajili ya mishahara na matumizi ya kawaida, shilingi 39,549,241,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 320,067,385,600 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo, shilingi 96,598,691,000 ni fedha za hapa na shilingi 223,468,694,600 ni fedha za nje. Sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida, mishahara ya watumishi, miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, shukrani. Napenda kukushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Pia nimshukuru Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mbunge, Waziri wa Nishati na Madini na Naibu wake Mheshimiwa Adam K. Malima, Mbunge, kwa ushirikiano wa dhati walioutoa wakati wa kujadili Bajeti hii.

Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini Ndugu Arthur G. Mwakapugi, pamoja na Wataalamu wake akishirikiana na Wataalamu kutoka Taasisi/Mashirika yote yaliyo chini ya Wizara hii kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini na uzoefu wao waliouonyesha wakati wa kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini - Fungu 58, kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 ambayo yamewasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Dk. Harrison G. Mwakyembe, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Faida M. Bakar, Mheshimiwa Yahya K. Issa, Mheshimiwa Halima M. Mamuya, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mheshimiwa Rita Louis Mlaki, Mheshimiwa Mohammed H.J. Mnyaa. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Kilontsi M. Mpologomyi, Mheshimiwa Dk. James A. Msekela, Mheshimiwa Omar Shekha Mussa, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Christopher O. Ole Sendeka, Mheshimiwa Mohammed S. Sinani, Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile namshukuru Kaimu Katibu wa Bunge Dk. Thomas D. Kashillilah na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuwezesha Kamati yetu kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niwashukuru Makatibu wa Kamati Ndugu Lina Kitosi na Ndugu Emmanuel Mpanda, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuhudumia Kamati hii kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Sekta hii ya Nishati na Madini na si mwingine ni mwenyewe Waziri Kivuli, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED HABIB J. MNYAA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na kuniwezesha kusimama hapa leo hii kwa niaba ya Kambi ya Upinzani ili kutoa maoni na ushauri kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu Na 99(7) Toleo la 2007 kuhusu mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, kwa vile nimewasilisha mezani, ninaomba inukuliwe kama ilivyo katika *Hansard* hata kama sitomaliza kuisoma yote.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako napenda kutumia fursa hii kuwapongeza wananchi wa Jimbo langu la Mkanyageni na Chama changu cha CUF walioniwezesha kufika hapa Bungeni. Nawaahidi kuwatumikia kwa kadri Mwenyezi Mungu atakvyonijaalia maana wao ndio walio sababisha kuwepo hapa Bungeni leo na kutoa mawazo yao kwa Taifa letu la Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza viongozi wangu wa Kambi Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Dr.Willibrod Slaa, pamoja na wale wote waliota michango yao kwa kunipa moyo muda wote wa maandalizi ya hotuba hii. Na wa mwisho lakini si kwa umuhimu ni Msaidizi wangu wa Wizara hii Mheshimiwa Sevelina Mwijage. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa mipango katika bajeti ya mwaka 2007/2008. Mambo muhimu yaliyopangwa kutekelezwa katika bajeti ya mwaka 2007/08 ni pamoja na yafuatayo:-

- Ukuwaji wa sekta ya Nishati; na
- Ukuwaji wa sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa miradi iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka 2007/2008. Katika bajeti ya mwaka uliopita Bunge lako Tukufu lilipitisha matumizi ya Wizara hii ya jumla ya shilingi 353.959.143.900/- ambapo shilingi bilioni 41.549.559.000/- kwa matumizi ya kawaida ambayo ilikuwa ni asilimia 11.7 ya bajeti yote na shilingi bilioni 312.409.584.900/- kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo ni asilimia 88.3 ya bajeti yote.

Mheshimiwa Spika, hapa napenda kuweka angalizo kwamba bajeti ya mwaka 2006/07, matumizi ya kawaida yalikuwa ni asilimia 7 na ya maendeleo ilikuwa ni asilimia 93. Kwa maana nyingine bajeti ya 2007/08 tuliongeza matumizi ya kawaida na tukapunguza matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine katika bajeti hiyo ya mwaka jana makadirio ya makusanyo ya mapato yalikuwa shilingi bilioni 57.958.480.800/- na hadi kufikia mwezi wa Machi 31, 2008 makusanyo yalikuwa shilingi bilioni 42.177.017.005/02 sawa na asilimia 72.77 zilikuwa tayari zimekusanya.

Mheshimiwa Spika, fedha za maendeleo zilizopatikana katika bajeti hiyo ya mwaka jana hadi kumalizika kwa robo ya tatu ni shilingi bilioni 4.950.321.000/- kati ya Shilingi 312.409.584.900/- zilizotengwa sawa na asilimia 1.58, lakini katika muhtasari kwa ajili ya Kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kilicho fanyika hapa Dodoma siku ya Jumatatu na Jumanne (tarehe 16 na 17 juni 2008), sura ya nne ukurasa wa.11, aya ya 4.3. Mheshimiwa Waziri alitueleza kiasi hicho ni asilimia 86.95 ya kiasi kilicho kasimiwa kwa kipindi hicho ambacho ni 5.693.000.000/-.

Mheshimiwa Spika, hapa Kambi ya Upinzani na Wabunge wengine waliomakini tumepata wasiwasi na kuijuliza ikiwa kiasi kilicho kasimiwa kwa robo tatu ya mwaka ni bilioni 5.693, je, hiyo robo ya mwisho zilipatikana ngapi zilikuwa ngapi ni Shilingi bilioni 306.716.584.900/-? Au hazikupatikana tena? Vipi hali hii? Kumbukumbu za Bunge ni kuwa tumepitisha bajeti ya maendeleo ya Shilingi bilioni 312.409. Kwa lugha sahihi asilimia 86.5 aliyosema bajeti ya maendeleo imetekeliza siyo sahihi, na ni ya kulidanganya bunge lako tukufu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala hili ukilitizama kwa upande mwingine ni kwamba, katika fedha ya maendeleo iliyombwa katika bajeti ya 2007/08 Shilingi bilioni 115.716.584.900/- zilikuwa fedha za nje sawa na asilimia 37 (bajeti tegemezi) na Shilingi 196.693.000.000/- ni fedha za ndani (ambazo ni asilimia 63) ambazo zimeweza kupatikana na kuingizwa katika miradi ya maendeleo ni bilioni 4,950,321,000/-sawa na asilimia 2.5 tu ya fedha za ndani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hii ni hatari na ni dhahiri basi, kwamba pesa inayokadiriwa na kupitishwa na Bunge lako na ile inayopatikana ni kitendawili. Tunalidhihaki Bunge na bajeti kwa jumla na hali hii isipokemewa na kusimamiwa vyema, maendeleo ni taabu sana kupatikana. Tunalidanganya Bunge tunawadanganya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ya mwaka jana 2007/2008, ukurasa wa saba, katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya mradi mkubwa wa gesi asilia ya Songo Songo, Mheshimiwa Waziri, alilielea Bunge lako Tukufu kuwa, ujenzi wa kituo cha MW6 kinachojengwa katika eneo la Somanga Funga, umekamilika kwa asilimia 90. Umeme utakaozalishwa na kituo hiki utasambazwa katika miji ya Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Singino, Nangurukuru, Utete, Ikwiriri, Kibiti na vijiji ambavyo bomba la gesi asilia linapita.

Mheshimiwa Spika, hadi hivi leo tunapozungumza hapa Bungeni na baada ya mwaka mmoja kupita hizo asilimia 10 zilizokuwa zikamilishwe kwa kipindi cha mwaka mmoja mzima bado hazija kamilika. Ufungaji wa mashine haujakamilika, hiyo miji iliyosemekana kupata umeme hata nguzo hazija simamishwa na zilizosimamishwa hazina nyaya na kadhalika. Ndio maana hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya mwaka huu ukurasa wa 34 bado inazungumzia kukamilisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme cha Somanga Funga.

Kuna habari eti mkandarasi kacheleweshewa fedha ya msamaha wake wa kodi ya mafuta na kuna taarifa kuwa mkandarasi ana urafiki na wakubwa na hagusiki na ndio sababu za ucheleweshaji wa miradi hiyo. Hapa Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri atueleze, ni sababu zipi zilizopelekea kwa muda wa mwaka mzima hizo asilimia 10 zilizobaki ambazo hazijakamilika, ukizingatia kazi ya ujenzi wa kituo hicho ulitarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2007.

Mheshimiwa Spika, itakuwa ni vyema Mheshimiwa Waziri kuchunguza tuhuma hizo za kucheleta vibaya kwa miradi hii na kulitaarifu Bunge lako ipasavyo na kubainisha kuhusu taarifa ya urafiki huo wa kuchelewesha kazi za maendeleo vinginevyo dhana ya rushwa haiwezi kuepukika.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi huu wa Tegeta wa kuzalisha umeme wa MW 45 ambao katika maelezo ya Waziri wa Nishati na Madini aliyyoyatoa katika kamati tarehe 28 Machi, 2007, kwamba mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Uhulanzi chini ya mpango wa *ORET* ambapo Serikali ya Uhulanzi itatoa msaada (*grant*) kugharamia nusu ya gharama na nusu nyingine kama mkopo wa masharti nafuu kwa Serikali ya Tanzania.

Mradi huu ulitarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2007. Mheshimiwa Waziri, alituhakikishia kwamba matayarisho ya uundaji wa mashine na vifaa kutoka kampuni ya *WARTSILA* ya *Finland* yalikuwa yanaendelea ikiwa ni pamoja na kazi ya usanifu na utayarishaji wa michoro. Baadaye yakatolewa maelezo kwamba mradi huu sasa ungekamilika Agosti, 2008, yaani mwezi ujao, ikiwa ni ucheleweshaji wa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, gharama za mradi huu zilielezwa kuwa ni *Euro* 31,000,000/= sawa na shilingi bilioni 55.8. Hadi hivi sasa mradi huu haujakamilika na tayari ni wastani wa ucheleweshaji wa miaka miwili. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atueleze kulikuwa na sababu gani za msingi zilizosababisha kucheleweshwa kwa mradi

huo hadi kufikia muda wa miaka miwili. Hii sio bure, Mheshimiwa Waziri ni vyema alieleze Bunge lako Tukufu kama kuna uzembe au vinginevyo.

Katika bajeti ya mwaka 2006/2007, zilitengwa shilingi bilioni 50.6 (kasma 3001-3136) katika bajeti ya mwaka 2007/2008, zilitengwa bilioni 25.6 (kasma 3001-3136). Kwa maana hiyo, katika kipindi cha miaka miwili mradi huu tayari umeshatumia jumla ya shilingi bilioni 76.2 kama tulivyopitisha katika bajeti. Mheshimiwa Waziri athibitishe kama nazo hazikupatikana, vinginevyo kuna ziada ya shilingi bilioni 20.4 ya gharama halisi za mradi huu ambazo ni shilingi billion 55.8. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, alieleze Bunge lako Tukufu lililoidhinisha matumizi hayo ambayo pamoja na kuzidi gharama halisi, lakini bado hayajaleta matunda ya mradi huu wa Tegeta na tunaarifiwa hadi leo haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote tuliyoyabainisha hapo juu bado mradi huu umetengewa shilingi billioni 30.6 katika bajeti ya mwaka huu. Sijui Mheshimiwa Waziri mara hii atatueleza nini na kutoa ahadi gani kwa Bunge lako Tukufu ili kukamilisha mradi huu unaosubiriwa kwa hamu kuongeza uwezo wa uzalishaji umeme wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka pia Mheshimiwa Waziri alifafanulie Bunge lako Tukufu, ni kwa nini katika muhtasari kwa ajili ya kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa muda wa miaka mitatu sasa, 2006/2007, 2007/2008 na 2008/2009. Maelezo ya utekelezaji wa mradi huu ni kwamba uko katika hatua ya uzabuni na utekelezaji wake utaanza mara baada ya kumpata mkandarasi atakaejenga mradi kinyume na maelezo ya Waziri pamoja na *TANESCO*. Sasa tunajiuliza, nani anasema ukweli? Ni Waziri au waandaaji wa Bajeti ya Wizara? Hapa lipo tatizo na linafaa lipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, *Alstom Power Rentals*. Katika hotuba yangu ya mwaka jana, nilihoji juu ya uhalali wa kampuni ya uzalishaji umeme ya *Alstom Power Rental* inayotumia mafuta ya mazito, *heavy oil HA4*, tulioarifiwa kuwa ilianza kuzalisha umeme wa *MW 40* tarehe 19 Machi, 2007 kwa mkataba wa mwaka mmoja. Mradi huu uligharimu *USD 116* milioni, ingawa kwenye ripoti ya Kamati ya kuchunguza zabuni ya *Richmond* ilibainisha kuwa gharama halisi ya mradi huo ni *USD 130.181* milioni, sawa na shilingi bilioni 162.726.

Mheshimiwa Spika, pia nilihoji miradi ya kukodi ya kutumia mafuta wakati tayari tuna uzoefu wa *IPTL* inayokausha uwezo wa kifedha wa Serikali pamoja na *TANESCO* na kwa bahati nzuri ripoti hiyo ya *Richmond* ilonyesha njia mbadala ya kuzalisha umeme kama huo kwa kutumia gesi asilia kwa bei nafuu. Leo hii imebainika kwamba *TANESCO* wameshindwa kuingiza hata *MWI* katika *Grid* ya Taifa mpaka mkataba wa mradi huo umemalizika kinyume na majibu ya Waziri wa wakati huo aliylieleza Bunge lako Tukufu kama ilivyo katika *HANSARD* ya tarehe 16 Julai, 2007 ukurasa wa 143.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeghamramika kwa kiasi kikubwa kuileta kampuni hiyo hapa nchini na kwa kuwa hatukuweza kufaidika na umeme wa kampuni

hiyo na kwa kuwa kuna taarifa kuwa mitambo hiyo ilikuwa ni mibovu iko haja ya Bunge lako Tukufu kupata maelezo ya kina kutoka kwa Waziri mhusika na ikiwezekana Kamati yako ya kudumu ya Bunge inayohusiana na sekta hii kutafuta ukweli wa suala hili ulioisababishia Serikali hasara kubwa ya kiasi hicho na kuishauri Serikali kuepuka miradi mingine ya zima moto kama hiyo, kuepuka kuwabebesha wananchi gharama za juu za umeme zinazosababishwa kama fidia ya makampuni kama hayo.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza gharama za uendeshaji wa umeme na kupata maendeleo endelevu nchini, Serikali iliona kuna umuhimu wa kubadilisha mitambo ya *IPTL* ya *MW 100* ili itumie gesi asilia badala ya mafuta. Kwa mujibu wa *MKUKUTA*, mradi ulikadirwa kuanza Julai, 2005 na kukamilika 2007 na makadirio ya gharama yalikuwa ni Tsh. bilioni 23.76 kwa wakati huo. Katika bajeti ya mwaka juzi, 2006/2007, mradi ultengewa shilingi bilioni 18.45 katika bajeti ya mwaka 2007/2008, mradi huu ultengewa shilingi bilioni 15.54 (kasma 3001-3198. Hii inaonyesha kwa muda wa miaka miwili jumla ya fedha zilizotumika ni Sh. 34,003,923,800/= ambayo hii ni ziada ya shilingi bilioni 10.24 ukilinganisha na gharama halisi ya mradi huu kwa mujibu *Mkukuta* wa shilingi bilioni 23.76.

Mheshimiwa Spika, hapa Kambi ya upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufanuzi wa kina ndani ya Bunge hili Tukufu juu ya fedha tuliyopitisha katika Bunge na ile iliyotumika kwa miaka yote hiyo na thamani ya kazi iliyokwishafanyika kuhusiana na mpango/mradi huu, ni kwa nini kukawa kuna ziada hii ya fedha zilizotumika na hata bila ya mradi wenye kuanza?

Jambo la kushangaza zaidi ni kuwa, mradi umetengewa tena mwaka huu jumla ya shilingi bilioni 24, hivyo tunamtaka Mheshimiwa Waziri atueleze lengo halisi la kutenga tena kiasi hiki cha fedha kwa mradi huu ambao utekelezaji wake hauonekani na wamiliki wa kampuni hiyo hawaonekani kama wako tayari kukubaliana na wazo hilo la kubadilisha mitambo hii kuwa ya gesi. Kambi ya Upinzani inamtaka ufanuzi wa mradi kama huu usiotekelzeza na haja ya kuingizwa kwenye bajeti kwa miaka mitatu mfululizo bila ya mafanikio na kuharibu programu ya Mkukuta.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha mpango wa maendeleo na bajeti ya matumizi ya kawaida mwaka 2006/2007, mradi wa Kinyerezi ultengewa jumla ya shilingi 200 kwa lengo la kuongeza *MW 200* ili kuzalisha umeme wa bei nafuu kwa kutumia gesi asilia ya Songo Songo. Mradi huu ultarajiwu kuchukua miaka mitatu hadi kukamilika kwake. Hakuna maelezo yoyote yaliotolewa juu ya mradi huu sio katika bajeti ya mwaka 2007/2008, wala mwaka 2008/2009. Hivyo, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atueleze maendeleo ya mradi huu ambao tayari ulikwishatengewa shilingi milioni 200, ukizingatia hadi sasa hakuna maelezo yoyote angalau juu ya upembuzi yakinifu wa mradi huu. Au tulipitisha mradi hewa?

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2006/2007, mradi 21 ya kupeleka umeme vijijini hasa Makao Makuu ya Wilaya ilipangwa katika bajeti tuliyopitisha mwaka huu jumla ya shilingi bilioni 16,226 zilipitishwa na Bunge lako Tukufu. Katika bajeti ya mwaka 2007/2008, mradi 20 ilikuwa ni uendelezaji wa miradi hiyo hiyo ya

mwaka 2006/2007, ukiacha ule wa kupeleka umeme Makambako na Bunge lako lilipitisha jumla ya Tsh. 9,799,729,200/= ambapo shilingi milioni 870 zilikuwa ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, Bunge lako Tukufu tayari lilishapitisha bajeti ya Tsh. 26,025,000,000/= kwa miradi hiyo ya usambazaji umeme vijijini. Katika miradi hiyo ya usambazaji umeme vijijini, jumla ya miradi 13 bado haijakamilika na imo katika bajeti ya mwaka huu, 2008/2009 na imepangiwa jumla ya Tsh. 1,378,533,000/=katika kasma hiyo ya 3001 - 3112.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa iliyotolewa na *TANESCO* kwenye Kamati ya Nishati na Madini Mei, 2008 tulielezwa kwamba gharama halisi ya kukamilisha miradi hii ni shilingi bilioni 22.087. Kutokana na sababu hizo zilizotolewa na *TANESCO* na kwa kuwa nilimwomba Mheshimiwa Waziri kunipatia idadi ya fedha iliyopatikana na kutumika katika kila mradi wa usambazaji umeme vijijini kwa mwaka 2005/2006, 2006/2007 na 2007/2008 lakini kwa bahati mbaya suala hilo hajalifanikisha.

Kwa kuwa miradi hii inaendelea na ni miradi inayowagusa na kupigiwa kelele na Waheshimiwa Wabunge wengi kwa niaba ya Wananchi wao, hivyo basi, naomba kutumia nafasi hii kwa niaba yangu, Kambi ya Upinzani na kwa niaba ya Wabunge wengine wa Chama tawala, Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii atuletee kabla ya majumuisho ya bajeti yake jedwali kamili litakaloonyesha kwa usahihi jina la mradi, makisio ya mradi huo. Fedha iliyooombwa na iliyotumika kwa kila mwaka katika kipindi hicho cha miaka mitatu ili Wabunge tuweze kujiridhisha na kuona kwamba hatupitishi bajeti hewa na idadi wanayohitaji *TANESCO* kukamilisha miradi hii ni sahihi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maendeleo endelevu ya rasilimali, nishati na namna ya kupunguza gharama za uzalishaji, ni muhimu sana kwa Serikali kuwajibika ipasavyo katika kuhakikisha sekta ya nishati inapewa umuhimu wa pekee unaostahili kwa kuitengea bajeti ya kutosha na kuwa na rasilimali watu waliobobea na utendaji makini.

Zaidi ya hayo, mikataba yote inayohusiana na umeme tutakayokatibiana na makampuni ya Kitanzania au ya Kigeni ni lazima ifanywe kwa uangalifu na uwazi mkubwa ili yapatikane mafanikio kwa pande zote, *win-win situation* na ni muhimu sana kuepukana na mikataba ya gharama inayofilisi *TANESCO* au Serikali kama ile ya *IPTL*, *ALSTOM*, *RICHMOND* na kadhalika. Pia iko haja sasa ya kubadili tabia, kuwa na mwamko na ubunifu wa njia zitakazotupunguzia gharama za uzalishaji na upotevu wa umeme usio wa lazima.

Mheshimiwa Spika, inakisiwa kwamba msongo, *grid*, yetu ina upotevu wa umeme takriban asilimia 25. Ni rahisi kurekebisha miundombinu inayosababisha upotevu huu kuliko gharama za kuzalisha kima kama hicho kinachopotea. Hivyo, ni rahisi kupunguza upotevu wa umeme, *energy losses*, unaosababishwa na watumiaji wasiowaangalifu. Kwa mfano, upotevu wa umeme katika maofisi ya Serikali unaosababishwa na kuacha wazi taa pamoja na viyoyozi, vinafanya kazi hata kama ofisini hamna mtu na mara nyingine sio siku za kazi, baadhi ya taa za barabarani kuwaka hata nyakati za mchana na baadhi ya

watumiaji umeme majumbani hawana mwamko wa kutumia balbu maalum zinazotumia umeme kidogo na kutoa mwangaza mkubwa, yaani *energy saving bulbs*.

Mheshimiwa Spika, kuna nchi nyingi ambazo wamepanga mipango madhubuti ya kutumia *energy saving bulbs* kwa ajili ya kupunguza gharama za uzalishaji. Mfano mzuri ni nchi ya Uganda ambao wana mpango wa kusambaza balbu 800,000 ili kuweza kuokoa kiasi cha zaidi ya US\$ 1,000,000 kwa punguzo la *MW 30*. Serikali ya nchi hiyo tayari wameondoa VAT ya asilimia 18 na *import duty* ya asilimia 25 katika bajeti ya mwaka jana kwa kampuni ya *Osram* ya Ujeruman kwa uingizaji wa taa hizo ili kupunguza gharama za manunuzi na kutoa bure kwa wale wasiokuwa na uwezo wa kununua balbu.

Kutokana na tafiti zilizofanywa nchini Kenya, zinaonyesha kuwa nchi hiyo inapoteza kiasi cha shilingi bilioni 10 kwa mwaka kwa kutumia taa ambazo zinatumia umeme mkubwa ambazo fedha hizo zingeweza kuwasomesha Wanafunzi wa Shule zote za Msingi Nchini humo. Laiti kama kila nyumba itatumia *energy saving bulbs*, basi wangeweza kuokoa kiasi cha *MW 131* ambazo ni sawa na punguzo la asilimia 80.

Hii inaonyesha kwa kupitia mpango huu *line* yenye uwezo wa kuwahudumia wateja wapatao 1,000 basi, ingeliweza kutoa huduma kwa watu 5,000. Kutokana na mpango huu pia Nchi ya Ghana wameweza kuokoa kiasi cha fedha US\$ 12 milioni kwa kuweza kupunguza *GW 2*. Nchi ya Australia tayari wameshapitisha sheria ya upigaji marufuku wa uuzaaji wa taa za zamani ambazo hutumia umeme mkubwa na badala yake kuhamasisha utumiaji wa *energy saving bulbs* nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, wakati tukiona nchi mbalimbali duniani zinafanya juhudhi hizo, ni dhahiri kuna nafuu kwa mfano, mtu mwenye kipato cha wastani na anayeishi kwenye nyumba ya kawaida yenye familia ya kiafrika huwa anatumia wastani wa *unit 380* za umeme kwa mwezi, kwa wale wanaotumia balbu ya *watt* 60 lakini familia hiyo hiyo inapotumia balbu ya *watt* 20, *energy saving bulb*, angetumia wastani wa *unit 125*, ikiwa ni punguzo la matumizi la asilimia 67.

Kwa tafiti zilizofanywa, imebainika kwamba kampeni ya kutumia *energy saving bulbs* imeweza kupunguza gharama za uzalishaji wa nishati hii ya umeme. Zaidi ya yote, utumiaji wa taa za zamani unaongeza utumiaji mkubwa wa umeme ambao hupelekea utumiaji mwingi wa gharama za uzalishaji umeme, mafuta/gesi/ maji, ambao husababisha ongezeko la joto duniani. Kwa kuwa Tanzania au Wizara ya Nishati na Madini haijalifikiria suala hili na halimo katika bajeti ya mwaka huu, hivyo basi, kwa utafiti huo tulioufanya, nimewomba Mheshimiwa Waziri kulitafakari suala hili na kuliingiza katika bajeti ya mwaka ujao.

Mheshimiwa Spika, katika jiji la Dar es Salaam na miji mingi ya Tanzania kuna miundombinu ya umeme ambayo haiko katika hali ya kawaida inavyohitajika. Kwa mfano, baadhi ya transfoma zilizowekwa chini ambazo hazina uzio na waya za umeme mkubwa zilizounganishwa na transfoma hizo hazina ngao, *shield*, pia baadhi ya nguzo zimekaza, *inclined* sana kiasi cha kuhatarisha maisha ya wapita njia, kwani wakati wowote zinaweza kuanguka. Vivyo hivyo baadhi ya waya za taa za barabarani ziko wazi. Hii sio

sura nzuri ya miji yetu katika Tanzania ya leo na kitengo cha usalama cha *TANESCO*, yaani *Safety Department*, inafaa kitengewe fedha kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Nishati na Madini angalau kwa kuwasilisha *DRAFT* ya *Power System Master Plan* mnamo tarehe 28 na 29 Aprili, 2008 katika Hoteli ya Kilimanjaro *Kempisk* kwa kupata maoni ya wadau na ni mategemeo yetu kwamba Wizara itasikiliza maoni ya Kamati ya Nishati na Madini ya kuiwasilisha hapa Bungeni kupata maoni ya Wabunge ambao ndio wadau wakubwa wanaowakilisha wananchi. Kwa wale tuliobahatika kuiona, tulishangazwa kuona ongezeko la $3,595MW$ kwa kipindi cha miaka 25 ijayo, lakini *plan* hiyo imeanzia mwaka 2006 hadi 2031 pamoja na kuwasilishwa mwezi Aprili, 2008. Ni nini kilichowafanya wataalam hao wasifanye *simulation* kuanzia mwaka wa kuwasilisha *plan* hiyo? Je, walifikiria ongezeko la idadi ya watu katika kipindi cha miaka 25 ijayo? Tunategemea Mheshimiwa Waziri atalifafanulia Bunge lako Tukufu suala hili.

Mheshimiwa Spika, katika *plan* hiyo, pia inajumuisha ile dhamira ya *interconnector* baina ya Tanzania, Kenya na Zambia ambalo ni jambo zuri kwa maendeleo ya nchi zetu. Hata hivyo, napenda kutahadharisha kwamba, ili Tanzania tuweze kufanikiwa na kupata kuuza umeme kwa majirani zetu, hatuna budi kujitosheleza kwa soko letu la ndani kwanza na kuzalisha zaidi ya kiwango kilichopangwa kwenye *DRAFT Power System Master Plan* hiyo.

Mheshimiwa Spika, sababu kuu ya maoni hayo ya Kambi ya Upinzani ni kwamba, Afrika ya Kusini wamenekuliwa wakisema katika toleo maalum *la ENGINEERING NEWS, Aprili 25 - May 1, 2008 volume 28 no 15*, kwamba kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya nishati ya umeme, wana mpango wa kuongeza $40GW$ ifikapo mwaka 2025. Mipango ya kupata umeme wa mkaa wa mawe kutoka Botswana na Msumbiji, umeme wa gesi asilia kutoka Namibia na Msumbiji na umeme wa maji kutoka Jamhuri ya watu wa Kongo imeshaanza. Kampuni ya umeme ya S.A, *ESKOM* inasema, kutokana na nyimbo ya Carlos Santana, inasema: “*Life is a game of give and take*”, yaani nipe nikupe, lakini kutokana na tatizo la nishati hii, Afrika ya Kusini wanaangalia zaidi kuingiza umeme kutoka nje na sio kutoa.


Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini ni sekta nyeti na ambayo inakua kwa kasi kikubwa kulinganisha na Sekta nyingine katika uchumi. Aidha, ni sekta ambayo kama ikishikwa na kupaliliwa vizuri inaweza kuibadilisha nchi yetu kutoka kuwa ombaomba na kuwa toshelezi. Kambi ya Upinzani inaelewa na inaamini kuwa kazi kubwa imefanywa na Kamati ya Madini ya Mheshimiwa Jaji Bomani. Hivyo basi, inaitaka Serikali kuyafanya kazi mapendekezo yote ambayo yametolewa na Kamati hiyo kuhusiana na Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iwe mwanachama wa *Extractive Industries Transparency Initiative*, yaani *EITI*, ambayo ni asasi ya kimataifa yenye Makao Makuu yake *Oslo* nchini *Norway* ambayo inasisitiza uwazi wa mapato yatokanayo na maliasili ambazo nchi imejaaliwa na Mwenyezi Mungu. Asasi hiyo inasisitiza nchi mwanachama zenye dhamana ya kulinda rasilimali za wananchi kuwa

wazi katika mapato yote yatokanayo na rasilimali zao. Ili kuwa na uwazi huo, asasi hiyo inasisitiza kuwa Serikali zinachapisha kwa wazi mapato yote inayopokea toka kwenye makampuni ya migodi na jinsi mapato hayo yanavyotumika. Aidha, Kampuni za madini zichapishe malipo yote wanayotoa kwa Serikali.

Kambi ya Upinzani inasisitiza na kuitaka Serikali kuwa mwanachama wa asasi hii. Hii itasaidia kwanza wananchi kuwa na imani na Serikali yao kuhusu matumizi ya rasilimali zao ambazo Serikali ni mlezi wake. Hii itapunguza maswali ambayo wananchi wanajiuiliza bila ya Serikali kuwa na majibu stahiki. Sambamba na hilo, ni dhahiri udanganyifu unaofanywa na makampuni ya madini unaweza kupungua kwa kiasi kikubwa, kwani watakuwa wamejifunga minyororo wenywewe.

Mheshimiwa Spika, kauli ya Waziri wa Nishati na Madini aliyoitoa Bungeni katika Mpangilio wa Kiutawala (*chart*).



Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia wakati wa uchangiaji bajeti ya ofisi ya Waziri Mkuu, Serikali imetoa majibu ambayo hadi sasa bado yanawachanganya Watanzania kutokana na utata wake kuhusiana na suala zima la *MEREMETA*.

Katika kipindi cha bajeti ya 2006/2007 tuliuliza maswali mengi kuhusiana na Kampuni ya *MEREMETA* iliyokuwa imeundwa kwa minajili ya kuiongezea nguvu kimapato Kikosi cha Nyumbu cha JWTZ Kati ya majibu yaliyojibowi na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini wa wakati huo kwa mujibu wa *HANSARD* ni kuwa, nanukuu: “*Sasa kwa ufupi, nataka niseme yafuatayo: Kwanza MEREMETA amesema imeanzishwa off-show, hata mwanzo ndiyo iliyokuwa na sasa iko katika process ya winding-up. Kwa hiyo, kinachoendelea sasa ni katika mtiririko huo.*” Mwisho wa kunukuu.


Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika kuhitimisha bajeti yake tarehe 23 Juni, 2006 alisema yafuatayo kuhusiana na *MEREMETA*. Nanukuu: “*Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya nani ni wamiliki wa MEREMETA na Mwananchi? Kwa maelezo niliyokuwanayo ni kwamba MEREMETA ni Kampuni ya Serikali iliyanzishwa kwa lengo la kununua dhahabu kutoka wachimbaji wadogo wadogo. Baadaye Kampuni ilianza mradi wa kuchimba dhahabu katika eneo la Buhemba Mkoani Mara.*” Mwisho wa kunukuu. Lakini wakati Mheshimiwa Waziri wa Nishati akitoa maelezo ya Serikali kuhusiana na ombi la Mheshimiwa Dr. Slaa la kutaka maelezo toka Serikalini kuhusu tuhuma za ubadhirifu katika BOT, alijibu yafuatayo, nanukuu: “*Serikali inapenda kukanusha kauli hizi kwamba Kampuni ya MEREMETA imeuzwa kwa TANGOLD. Kampuni ya MEREMETA haijauzwa kwa mtu yeyote au kwa Kampuni yeyote, iwe kwa bei ya kutupwa au kwa bei ya kuruka. Kama nilivyoeleza hivi punde, MEREMETA imesitisha shughuli zake kwa mujibu wa sheria. Kutokana na hatua hiyo, mali na madeni ya MEREMETA yamehamishiwa kwenye Kampuni mpya ya TANGOLD ambayo inamiliikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja. Mali hizo zinajumuisha pia Mgodi wa dhahabu wa Buhemba.*” Mwisho wa kunukuu.

Kauli hizi za Serikali zinapingana na zina utata. Kwanza tumeelezwa iko katika hatua za mwisho za *winding-up* na Waziri mwingine anasema, Serikali imeinunua. Haya, kama Serikali imeinunua ilikuwa ni ya nani hapo mwanzoni na ni kwanini ilikuwa chini ya JWTZ? Haya ndio masuali ambayo hadi leo hii hayajapata majibu tangu mwanzo na ndio msingi wa manung’unko na malalamiko ya Watanzania, yaani kutokupata majibu ya moja kwa moja kutoka Serikalini.

WANAHISA WA MEREMETA KWA UTAFITI WA KAMBI YA UPINZANI

TRIENNEX
(pty ya Afrika Kusini
yenye hisa 50%

MSAJILI
HAZINA (Tz) - hisa 50%



Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataku kujuu, hii MEREMETA hasa ni ya nani? Hawa *London Law Services* na *London Secretarial Services* ni akina nani hasa? Kampuni ya MEREMETA ina hisa asilimia ngapi? Haya ni mambo yanatufanya tuwe na mashaka makubwa sana. Hivi Serikali inaogopa nini kuweka mambo haya wazi hadharani, angalau kwa kamati husika ya Bunge basi, ili kama kuna sababu ya msingi wawakilishi wa wananchi waweze kufahamu.

Kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuwa MEREMETA ni ya Jeshi na haiwezi kutolewa maelezo Bungeni kwani ni kutoa siri za jeshi, hivyo kuhatarisha usalama wa nchi, ni majibu ya kushangaza. Wanahisa wa MEREMETA ni wageni na hivyo siri za Jeshi ni salama kwa wageni kuliko Wabunge au Bunge lako? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali itoe majibu sahihi na sio kutoa majibu ya kisiasa tu. Kambi ya Upinzani imekwishesha, iwapo kuna jambo la siri kweli, basi liwasilishwe kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge au Kamati ya Uongozi. Lakini kauli kuwa Serikali haiwezi kusema lolote, haiwezi kamwe kukubalika na Bunge hili. Bunge linapaswa kusimamia hata Jeshi kwa mambo yasiyohusu mikakati ya kijeshi. Dhahabu ni biashara na hakuna siri ya kibiashara kwa Bunge. Ni imani yetu kuwa Serikali itatuelewa hivyo na kutoa majibu ya kuridhisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyatoa hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:
Kuhusu Utaratibu.

SPIKA: Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:
Mheshimiwa Spika, Kanuni namba 63(3). Mbunge, aliyejukwaa anazungumza sasa hivi kwenye taarifa yake ukurasa wa nne, ile aya ya kwanza kabisa, anasema ufungaji wa mashine haujakamilika, hivyo miji iliyosemekana kupata umeme, hata nguzo hazijasimamishwa na zilizosimamishwa hakuna waya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunasikilizwa na Watanzania wengi, maneno kama haya ningependa yathibitishwe kama yana ukweli, kwa sababu yanaonekana Mheshimiwa Mbunge, hakusema kweli.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, sikuyaona hayo. Lakini haya ni maoni ya Kambi ya Upinzani. Napenda niamini kwamba walivyotembea wametazama na kuona hivyo. Sasa kwa sababu mjadala unaendelea, sioni haja ya kulitafutia jibu sasa hivi Mheshimiwa Waziri. Nina hakika atalikanusha kama sio kweli. Waziri muhusika na Naibu wake, watalikanusha kwa njia ambayo italiweka wazi zaidi. Kwa hiyo, naomba tuendelee. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, napenda niwakumbushe kwamba, au nitamke tu kwamba tuna wachangiaji walioomba 47 katika makundi yafuatayo:- Ambao hawajachangia kabisa wako 12, waliochangia mara moja wako 31 na waliochangia mara mbili au zaidi wako wanne. Sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 60(5), (6) na (7) ambayo ni lazima niisome kwa kunukuu, inasema: “*Endapo maombi ya kuchangia hoja fulani yatakuwa mengi zaidi ya muda uliotengwa kwa hoja hiyo, Spika atatoa nafasi ya kwanza kwa Wabunge, ambao hawajachangia katika hoja zilizotangulia kujadiliwa katika Mkutano unaoendelea au wamechangia mara chache.*” Kwa hiyo, hicho cha kwanza. Kwa hiyo, ni dhahiri tutaanza na hawa 12 ambao hawajachangia.

Pili, “*Bila kuathiri masharti ya fasili hiyo, Spika, atahakikisha kuwa nafasi za kuchangia zinatolewa kwa uwiano unaofaa baina ya aina zote za Wabunge walioomba kuchangia.*” Kwa hiyo, hilo nalo linatuongoza sisi tunaokaa hapa.

Tatu, “*Masharti yaliyotangulia katika kanuni hii, hayatamuia Spika.*” Naruadia hiyo, “*Hayatamuia Spika kutoa nafasi ya kuchangia kwa Mbunge mwengine yejote, iwapo Spika, ataona kuwa taaluma au uzoefu fulani wa Mbunge huyo utaboresha hoja inayojadiliwa.*”

Nimetangulia kusema haya ili sisi sote tunaokaa hapa, tunapotoa maamuzi haya nani aseme, basi mjue tunaongozwa na Kanuni. Sasa basi, kwa uzoefu tulionao, sasa hivi hadi saa 07.00 wataweza kuchangia wawili tu au wakifupisha labda watatu na jioni inawezekana wakachangia 11. Kesho asubuhi, wanaweza wakachangia tena 11 na jioni napenda niruhusu watatu tu ili tufike saa 11.45. Nitamwita Naibu Waziri, atafuatiwa na Mtoa Hoja, watamaliza saa 01.00 jioni ili tuingie kwenye Kamati ya Matumizi saa 01.00 jioni kesho. Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa katika hali hii kwamba Waheshimiwa Wabunge, watakaochangia kati ya hawa 47, watakuwa ni 28 au 29, niliona hili mlifahamu kabla hatujakwenda mbali.

Lingine, nimeshindwa kujizuia kuwapongeza Idara yetu ya *HANSARD* kwa kazi nzuri sana hii wanayoifanya. Sasa hivi, hotuba za Kamati na pia zile za Kambi ya Upinzani, zinatoka katika hali inayorahisisha hata rejea. Badala ya kubeba yale makaratasi ya zamani mengi hivi, *HANSARD* wanakesha wanafanya kazi hii. Naomba nitambue utendaji kazi mzuri wa *HANSARD* na kwa wakati muafaka kwa niaba yenu nitawatuza kitu fulani. Ahsante sana. (*Makofi*)

Sasa wanaotazamiwa kuchangia ni kama ifuatavyo: Nitawataja wale 12 ambao hawajachangia hata mara moja katika Mkutano huu. Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Antoni Mwandu Diallo, Mheshimiwa Fred Mpandazoe Tungu, Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakari, Mheshimiwa *Professor Fithman Banyikwa*, Mheshimiwa Balozi Getrude Ibengo Mongella, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Ephraim Madeje na Mheshimiwa Hasnain Dewji. Kwa sasa nitaanza na Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, atafuatiwa na Mheshimiwa Joelson Mpina.

Mheshimiwa Sinani hayupo, basi inaturahisishia mambo. Mheshimiwa Mpina naye hayupo? Mheshimiwa Anthony Mwandu Diallo! Loh! Mheshimiwa Fred Mpandazoe Tungu, yeye yupo. Basi tunaanza na Mheshimiwa Fred Mpandazoe Tungu atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Ally Salum.

MHE. FRED MPENDAZOE TUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa William M. Ngeleja kwa jinsi alivyowasilisha kwa umahiri mzuri sana hotuba yake ya Bajeti. Vilevile naomba ku-*declare interest* kwamba yule ni mdogo wangu, nampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hoja, hii naomba niseme yafuatayo:- Kwanza kabisa, ni ukweli usiopingika kwamba nchi yetu ina madini mengi, lakini vilevile sekta hii haijachangia vyta kutosha kwenye pato la Taifa, vilevile ripoti ya Mheshimiwa Jaji Bomani imeeleza hivyo hivyo. Kuna sababu mbalimbali ambazo zimeelezwa ambazo zinasababisha sekta ya Madini isichangie kikamilifu katika pato la Taifa. Lakini mimi nitazungumzia mambo mawili tu.

La kwanza kabisa, ni uwekezaji mdogo wa Serikali katika sekta ya Madini. Hata ripoti ya Mheshimiwa Jaji Bomanji katika ukurasa wa 115 imebaini suala hili kwamba Serikali inawekeza kidogo sana katika sekta ya Madini na kutokana na uwekezaji mdogo, inajikuta kwamba Serikali vilevile ufuutiliaji katika usimamizi wa uwekezaji wa makampuni ya nje katika sekta hii ya Madini na wenyewe unakuwa mdo. Nitoe mfano tu wa mgodi wa Almasi wa *Williamson Diamond Limited* uliopo Wilaya ya Kishapu. Mgodi huu ulianza uzalishaji mwaka 1958, umepitia historia ndefu, lakini itoshe tu kusema mwaka 1994 Serikali ya Tanzania iliwekeana mkataba na kampuni ya *Debeers* na Serikali ya Tanzania ikanunua hisa ya asilimia 25 tu. Mgodi wa Mwadui ni moja ya migodi mikubwa sana duniani, lakini Serikali imekuwa na hisa ya asilimia 25 tu, kiasi kidogo sana na kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba usimamizi wake umekuwa ni mdo sana.

Nitoe mfano kuhusu suala la usimamizi na ambalo linasababisha hasara kubwa sana katika Serikali yetu kupata hasara kutokana na uwekezaji katika Sekta ya Madini. Kampuni ya Mwadui pamoja na kuwa ni mgodi mkubwa sana, lakini kutoka mwaka 1994 hadi Mei mwaka huu (2008) mgodi huu amba ni mkubwa sana Serikali haikuwa na mwakilishi katika mgodi huo. Kwa hiyo, *Debeers* walikuwa wanafanya watakavyo, kwa Serikali sidhani kama ilikuwa inajua uzalishaji wake kikamilifu kwa sababu haikuwa na mwakilishi.

Lakini ripoti ya Menejimenti ya Kampuni ya Mwadui ambayo uwakilishi wa Serikali ni hafifu, katika mwaka huu imeeleza kwamba na miaka mingine iliyopita imeeleza kwamba mgodi huu umekuwa ukipata hasara, umeendeshwa kwa hasara kwa miaka 14 na Serikali haijapata gawio lolote kwa miaka hiyo. Hii ni kutokana na usimamizi hafifu unaotokana na hisa kidogo ambazo Serikali inayo katika mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo linasababisha sekta ya Madini isichangie katika pato la Taifa, vilevile inatokana na uzembe kwa Watendaji wetu. Nitoe mfano wa Mgodi huo wa Kampuni ya Mwadui toka mwaka 2006-2008 Bodi ya Wakurugenzi wa Mgodi huo amba kuna wawakilishi kutoka Serikalini na kuna wawakilishi wa kutoka *Debeers*, Bodi ya Wakurugenzi kutoka mwaka 2006 imekaa karibu zaidi ya mara 10, lakini mwakilishi mmoja ambaye ni muhimu sana kutoka Hazina, ndiye anayesimamia mapato ya Serikali au mali za Serikali, ilikuwa na Mwakilishi wa pale kama Mkurugenzi wa Bodi, amehudhuria mara moja tu.

Mkurugenzi huyu ambaye aliiwakilisha Serikali na anatoka Hazina na anatakiwa aishauri Serikali kuhusu masuala ya ukopaji, uendeshaji kama kampuni ilikuwa inakula hasara, ye ye ndiye alitakiwa awe Mshauri Mkuu kwa Serikali kuhusu suala hilo, lakini katika vikao zaidi ya 10 vya Bodi ya Wakurugenzi ye ye amehudhuria mara moja. Sasa wawekezaji tunawaacha wenyewe wafanye watakavyo. Lakini naomba niseme, kuna Wahenga walisema kwamba, wanyenyekevu wanaweza wakarithi kitu chochote duniani juu ya nchi lakini hawawezi kurithi Madini. Nchi yetu tukifanya hivyo kama waungwana, tunakuwa wa namna hiyo, hatuwezi kupata faida kwenye Madini. Serikali ilikuwa wapi mgodi umekula hasara kwa miaka 14? Watendaji wetu na wawakilishi wetu amba

wanatakiwa watusaidie sana ndiyo wanakuwa hivyo. Naomba sana Serikali iongeze uwekezaji katika hisa na iimarishe usimamizi katika hii sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la pili. Nizungumzie mgogoro uliopo kati ya *Eltilary Minerals* na wananchi ambao wanaishi karibu na mgodi huo, hususani wananchi wa Buchambi na Buganika. Aliyekuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe alitembelea Maganzo mwaka 2006, alilalamikiwa na wananchi wa Buchambi na wengine wanaishi karibu na mgodi huu kwamba wananchi wale wamekuwa wakinyanyasma, wakionewa na mwekezaji huyu ambaye anamiliiki mgodi wa *Eltilary Minerals*. Wananchi wa pale hawawezi kuchukua kuni katika eneo ambalo anamiliiki, hawawezi kulima, hawawezi kuchunga na tarehe 4 Mei, 2008 kulikuwa na kurushiana risasi kati ya walinzi wa Kampuni na wananchi na kulikuwa na ng'ombe zaidi ya 600 vilevile zilikuwa zimekamatwa na mwekezaji huyu kwa sababu zilikuwa zimekwenda kuchunga katika maeneo hayo.

Tume ya Jaji Bomani ilishaelezwa malalamiko hayo vilevile, lakini Serikali iko kimya. Naomba niseme malalamiko ya wananchi kwa maneno yao. Walisema hivi: "Inaonekana Serikali inasikiliza wawekezaji zaidi kuliko wananchi."

Mheshimiwa Spika, ni maneno waliyoyasema wao kwenye kikao nilichofanya tarehe 24 Mei, 2008 kwa sababu wamelalamika kwa Naibu Waziri hawajapata jibu, wamelalamika kwa Jaji Bomani hawajapata majibu na mimi nimefikisha suala hili Serikalini kwa maandishi sijapata jibu. Sikuwakilisha hisia walizokuwa nazo za hasira, lakini nawakilisha maneno waliyoyasema.

Mgogoro huu umekuwepo kwa muda mrefu pamoja na mikutano ya ujirani mwema ambayo imekuwa ikifanyika, lakini baada ya kufanyika matendo yale yanaendelea na siku hiyo alikuwepo mwakilishi wa Kituo cha Polisi cha mahali pale, alithibitisha wananchi kunyanyasma, kuonewa na kufanyiwa matendo ambayo sio ya kibinadamu. Naomba Serikali ichukue hatua endelevu ya kudumu na kukomesha uonevu huo. Lakini kuna suala lingine linalohusu wananchi walilalamika, wanasema: "je, kampuni ya *Eltilary Minerals* iliingiaje katika maeneo hayo bila kushirikiana na wananchi wa vijiji hivyo?" Vilevile Serikali haijatoa jibu, kwa Jaji Bomani walilalamika na kwa Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe na ninafikiri walilalamika katika vikao mbalimbali lakini hawapati jibu.

Nimefuatilia Wizarani tarehe 25 Juni, nimeona yafuatayo nilipokuwa na Kamishna wa Ardhi kuhusu maeneo ambayo wananchi wamekuwa wakiyalalamikia kwa muda mrefu. Cha kwanza, kampuni ya *Eltilary Minerals* ambayo imepewa kumiliki maeneo vitalu namba 95,96,97,98 imemilikishwa sio kihalali kufuatana na maelezo yaliyoelezwa na Kamishna. Hakuna Kamati iliyokaa Kishapu kuzungumzia utoaji wa maeneo hayo, barua ya toleo au *letter of offer* iliyotolewa tarehe 4 Machi, ilisainiwa Kahama kinyume cha taratibu na Kamishna alikubali kwamba *Eltilary Minerals* amemilikishwa sio kihalali na ninaomba Serikali ithibitishe hilo na kuwaeleza wananchi kwamba sasa maeneo hayo, mashamba namba 95,96,97,98 umilikishaji wake usitishwe au utenguliwe mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuzungumzia suala moja tu ambalo limezungumzwa katika *report* ya Jaji Bomani kuhusu utata mkubwa uliojitokeza katika mgodi wa Kiwira kuhusu ubinafsishaji. Nakubaliana na maelezo ya Tume ya Jaji Bomani kwamba kuna utata mkubwa wa jinsi umilikishaji ulivyofanyika na tunaomba Serikali kama mapendekezo yale yalivyozungumza, ifanye uchunguzi wa kina kuhusu suala hilo zima la umilikishwaji wa Mgodi wa Kiwira, lakini na umilikishwaji wa Mgodi wa *MEREMETA* vilevile ufanyike kwa kina. Lakini naomba kupongeza kuhusu Serikali kusitisha mkataba wa *Dorwans*, tunashukuru sana kwa sababu wengine walikuwa wanakejeli kuhusu suala la *Richmond*. Lakini naomba nimalizie kusema hivi, ukweli unapitia hatua tatu. Kwanza ukweli unakejeliwa sana; hatua ya pili, ukweli unapingwa hata kwa nguvu na hata kwa kumwaga damu; lakini tatu, ukweli hukubalika kwa sababu ukweli hujisimamia wenyewe.

Kwa hiyo, masuala tunayouliza humu Bungeni kuna masuala ambayo ni kweli na kwa mfano *Report* ya *Richmond* iliyowasilshwa hapa ilikubalika na Wabunge wote hapa na mapendekezo yake yalikubalika, lakini kuna baadhi wanaokejeli, lakini ukweli ni kwamba ripoti ile ilikuwa ni sahihi, imeungwa mkono na wananchi na Watanzania wengi na kutokana na *report* hiyo, Bunge lako Tukufu limepata heshima kubwa sana. Ni ukweli huo. Unaweza kukejeliwa baadaye, unaweza ukapingwa, lakini utakubalika kwa sababu ukweli unajisimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nisigongewe kengele, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Fred Mpandazoe Tungu. Ni zamu sasa ya mchangiaji ambaye atakuwa wa mwisho asubuhi hii ambaye ni Mheshimiwa Ahmed Ally Salum – Mbunge wa Solwa.

Nimetahadharishwa na Katibu hapa kwamba Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami kumbe alikwishaongea, kwa hiyo, nimemwondoa kwenye orodha, atajiunga na wale waliokwishaongea.

Mheshimiwa Ahmed Ally Salum karibu!

MHE. AHMED ALLY SALUM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye hoja hii ya Bajeti ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa William Ngeleja kwa bajeti yake ambayo siyo mbaya sana wala siyo nzuri sana, lakini kwa sababu nimekuwa naye muda mrefu ofisini kwake kufuatilia umeme Jimbo la Solwa, sikuona chochote Jimbo la Solwa, kwa hiyo, nasema mimi siungi mkono hoja na ikiwezekana nitaondoa shilingi kama sijapata majibu ya kuridhisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu tarehe 9 Januari, nilimwandikia barua Mheshimiwa William Ngeleja, naomba kunukuu kwa kifupi sana. “Napenda

kukujulisha kuwa tarehe 27 Julai, 2006 katika majibu ya swali langu kuhusu mahitaji ya umeme Jimbo la Solwa, nilijibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wakati ule Mheshimiwa Lawrence Kego Masha na aliahidi kwamba Jimbo la Solwa litapata umeme 2009/2010”

Sasa katika barua hii niliweka msisitizo sana kwamba kutokana na mradi wa maji ambao unatoka Ihelele kupitia Jimbo la Solwa lenyewe kwenda Shinyanga wenye thamani ya sasa inafika shilingi bilioni 240, ingependeza zaidi kama Serikali itaongezea tu shilingi bilioni mbili au tatu ili kupeleka *infrastructure* katika kuinua uchumi katika Jimbo la Solwa. Kwanza sikupata majibu mpaka sasa ya barua yangu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali na ninamwomba Mheshimiwa William Ngeleja nipate majibu.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, umtamke Waziri, ndivyo Kanuni zinavyosema.

MHE. AHMED ALLY SALUM: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri nipate majibu ambayo yataniridhisha kwa hakika kuhusu umeme katika Jimbo la Solwa.

Mheshimiwa Spika, umeme sasa hivi kwenye dunia hii tunayokwenda ni muhimu kweli kweli. Huwezi kuongea mambo ya *irrigation scheme* bila kuongea umeme; huwezi kuongea biashara, viwanda bila kuongea umeme; huwezi kuongea sekondari, sasa hivi sekondari tujenga kwa maelfu, maabara, wanafunzi hawasomi vizuri kwa sababu hakuna umeme. Umeme sasa hivi ni kitu cha lazima katika uchumi wa Tanzania. Sasa hivi Dar es Salaam peke yake unachangia asilimia 80, ni kosa kubwa kweli kweli! Mikoa yote *almost* ni asilimia 20 ni *idle, simply* kwa sababu hakuna umeme kule.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Solwa linaongoza kwa kilimo cha dengu. Wanaonunua dengu kutoka nchi za nje wanadhani Solwa ndiyo Makao Makuu ya Tanzania. *Sometimes* kwa jinsi kilimo kilichokuwa kikubwa sana, lakini unakuta viwanda vingi sehemu ambavyo vinatakiwa viwe havikui kwa sababu hakuna umeme.

Mheshimiwa Spika, leo Solwa hakuna hata mashine, *simply* kwa sababu hatuna hata umeme, hakuna hata vivutio vidogo vidogo kwa kuvutia wawekezaji wa ndani hata wafanyabiashara wadogo wadogo wa Jimbo la Solwa, kwa sababu hatuna umeme. Naomba sana Wizara ifikirie kwa undani sana kuhusu umeme. Kinyume na umeme, tutakuwa na kila aina ya *problem*, tuna *DADPS, DASIP, REAR*, yaani hapa tutakuwa tunacheza mpira kwenye maji kama hatupeleki umeme vijijini. Maana sasa hivi umeme umekuwa kama ndiyo kitu cha mjini tu.

Mheshimiwa Spia, *raw material* kwa wakulima wanaolima kule Bariadi peke yake inatoa asilimia 30 ya Pamba ya Tanzania nzima, lakini Shinyanga hakuna kiwanda. Kwa wakati ule tatizo kubwa lilikuwa ni maji, lakini sasa hivi tunashukuru maji yanakuja, maeneo mengi ambayo yanastahili viwanda viwepo, kwenye maeneo yale hakuna umeme, maeneo mengi sana hapa Tanzania. Kwa hiyo, nadhani *first priority*

Serikali au Wizara ingetazama *potential area* ipo kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye maeneo muhimu sana katika kuinua uchumi wa eneo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali sana tena sana katika bajeti ya mwaka 2009/2010 tuone umuhimu wa kuiongezea fedha Wizara hii ili tupeleke umeme kwenye maeneo yote ya Tanzania ili sasa maeneo yote ya Tanzania ambayo hayachangii katika uchumi wa Taifa yawefe kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yote tunaongea hapa, MKUKUTA, MKURABITA, tutatengeneza kila aina ya *slogans* hapa, tutatengeneza kila aina ya *program*, lakini utaona maendeleo ya Tanzania kama yanakwenda kwenye mwendo wa taratibu *simply* tu kwa sababu umeme hakuna kwenye maeneo ambayo yanahitajika hasa yawepo pale. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niombe maombi yangu yafuatayo:-Katika kituo cha Afya cha Samuye, fedha zilishatoka, kila kitu vyombo vyote vilitoka pale kwa ajili ya kurekebisha umeme katika Kituo cha Afya cha Samuye. Nilipokwenda kuongea na Mkurugenzi wa TANESCO wa Mkoa akaniambia tatizo lilikuwa ni nguzo nne tu hazipo, tumekaa zaidi ya miezi minane, nne tu. Lakini sasa hivi nimefanya mawasiliano nimeambiwa kwamba nguzo zimefika, lakini naiomba sasa Serikali isukume kwa nguvu zote ili umeme pale uweze kurekebishwa katika Kituo cha Afya cha Kata ya Samuye.

Mheshimiwa Spika, lingine, kulikuwa kuna wakandarasi wanaitwa *Greeneka* walikuwa wakitengeneza barabara ya lami Shinyanga, Nzega, Tinde na Isaka, walituachia majengo 28 pamoja na kisima kimoja kikubwa sana. Katika kikao cha RCC cha Mkoa wa Shinyanga pamoja na Halmashauri yetu ya Shinyanga vijijini tukawa tumeamua majengo yale yaye majengo ya Wasichana katika elimu ya *secondary school* kuanzia *form one* mpaka *form four* katika Mkoa mzima wa Shinyanga. Kwa bahati mbaya sana *Greeneka* walivyoondoka wakaondoka na *transformer*, wakang'oa na nyaya za umeme. Mimi nilishangaa nikajiuliza kwa sababu gani wamefanya vile? Niliumia, lakini hakuna cha kufanya.

Nilipoongea na Mkurugenzi, akasema ni mikataba hiyo waliyoandikiana kule, sielewi waliandikiana namna gani. Sasa baada ya kufuutilia kwa undani sana, nilikwenda TANESCO kupata gharama mpya gharama zenyewe zilikuwa ni ndogo tu, *almost* Sh. 16,800,000/= kuweka *transformer* na waya ili sasa wanafunzi wasichana tena Wabunge wa Viti Maalum naomba mniunge mkono, hili tumeamua kwa ajili ya wasichana tu wa Mkoa wa Shinyanga asilimia 50 wanatoka Wilaya ya Shinyanga Vijijini na asilimia 50 Wilaya zote za Mkoa wa Shinyanga watakuja kusomea pale. Naomba sana Wizara izingatie hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ombi la pili. Mimi niko kwenye Sekondari tu leo kuhusiana na umeme. Sekondari ya Kituli ni kubwa kwelikweli, ina wanafunzi zaidi ya 200 na zaidi, wengi wao ni wasichana, lakini hakuna umeme. Hivi mazingira ya usiku kwa wasichana wale kila siku wanapatapata mimba haraka haraka wanaondoka tu, nani wa

kulaumiwa? Wa kulaumiwa ni giza? Mtatuzi wa giza ni Mheshimiwa Waziri mwenyewe mwenye dhamana hii husika. Kwa hiyo, naomba sana tena sana Sekondari ya Kituli, narudia, gharama zake tulishazifanya hizi hapa, *almost* shilingi milioni 58, ni ndogo kwelikweli. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana hii Wizara ifikirie sana baada ya kuchangia haya makaratasi yote niliyoyafanya kazi, Mheshimiwa Waziri nakuletea ili uone jinsi gani na nitapenda sana nipate majibu uniambie ndiyo fedha zimepatikana na umeme wa Jimbo la Solwa lini ninapata.

Lingine, mimi sipendi wasichana waondoke ondoke kwa sababu za mamba, ndiyo maana yake. Sekondari ya Samuye yenyewe tathmini yake ilikuwa ni shilingi milioni 26, ni nzuri ukiona, utadhani sekondari ya kimataifa jinsi tulivoyijenga, sasa hivi hakuna umeme. Naomba sana na hii shule ya Sekondari ya Samuye nayo ipate umeme. Shule ya Sekondari ya Kituli ipate umeme, kituo cha Afya cha Samuye Mheshimiwa Waziri naomba aifuatilie warekebishe umeme, Jimbo la Solwa na lenyewe lipate umeme.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, namalizia kwa kusema kwamba kuna wachimbaji wadogo wadogo katika Kata ya Mwakitolyo. Kabla ya wiki moja hivi alikuja hapa mwakilishi wao Peter - Mwenyekiti wa Wachimbaji wadogo wadogo, tukaonana na Mheshimiwa Naibu Waziri tukaeleza matatizo yao. Lile eneo nimepata taarifa kwamba ni *Barricks*, yaani *Barricks* anabeba nchi nzima sasa.

Sasa unajua Sheria na haki ni vitu viwili tofauti, yawezekana kabisa *Barricks* alikuwa amewahi, lakini wachimbaji wadogo wadogo wale kwa sababu ya kutokujua Sheria wakaambwa bwana, ninyi ...Kwa hiyo, mimi naitahadharisha Wizara na mapema kabisa kwamba itakapokuwa tayari, wamekuja wachimbaji wadogo wadogo wasije wakaondolewa hivi hivi, hatuwezi tukakubaliana. Hivi aliyeishi kabisa kuanzia dunia hii imeumbwa ni *Barricks*? Aliwahi kuishi pale au wachimbaji wa pale wadogo wadogo? Kwa hiyo, kikubwa hapa huwezi kusema Sheria sijui nini, waliwahi, wanakuja *Barricks* wachimbaji wadogo wadogo maelewano yanakuwepo, kama ni fidia kwa jinsi wanavyoridhika wao wapewe ili yeye aendelee na uchimbaji salama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nitaunga mkono hoja pale ambapo majibu yangu yatakuwa ni mazuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge ni dhahiri muda uliosalia hautuwezeshi kupokea na kuruhusu mchangiaji mwagine, kwa hiyo, tutaendelea baadaye jioni. Nawatamka tu wale ambao watakaochangia ili wajiandae kuanzia saa 11.00. Tutaanza na Mheshimiwa Anthony Mwandum Diallo, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary halafu Mheshimiwa Prof. Feethan Filipo Banyikwa, Mheshimiwa Balozi Getrude Ibengwe Mongella, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje na Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, kwa mpangilio huo.

Sasa kama nilivyotamka, muda hautoshi, kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge jilirudia*)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Mbili, Kikao cha Kumi na Tisa, *session* ya jioni. Mzungumzaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Anthony Diallo.

MHE. ANTHONY M. DIALLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru sana kwa kuniruhusu niwe mchangiaji wa kwanza katika hoja iliyo mbele yetu. Pili, napenda niishukuru sana Wizara ya Nishati na Madini kwa bajeti nzuri ambayo wameileta. Nina hakika kwamba ndugu yangu Mheshimiwa Ngeleja na mwenzake Mheshimiwa Malima au mtoto wangu Malima, wamefanya kazi nzuri na wanahitaji pongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mambo mengi yameshaanza kuzungumzwa, nitajaribu kwenda haraka haraka kwa maeneo machache, kwanza sekta ya madini. Sekta hii imekuwa ni kero kwa Watanzania. Ukiangalia idadi ya Tume ambazo zimeundwa kuchunguza, zinatoa mapendekezo, lakini mapendekezo yote unakuta hayafuatwi. Sijui kuna tatizo gani! Labda Mheshimiwa Waziri mpya na mwenzake kwa kutuonyesha mfano wa kuvunja mikataba uliokuwepo wa kufua umeme wa *Dowans* labda ni dalili njema. Kwa hiyo, napenda niwape moyo, waendelee hivyo hivyo tutawa-support. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba angalau mapendekezo ya baadhi ya hizi Tume yafanyiwe kazi. Sekta ya madini ilianza kuingiliwa na watu wa nje siku nyingi sana. Nakumbuka nikiwa *back bencher* mwaka 1998 kama sijasahau wakati tumetunga ile sheria iliyokuwa inafuta ile ya mwaka 1966, tuliletewa *advisors* wawili, mmoja alitoka *World Bank*, wakati ule bei ya dhahabu ikiwa karibu dola 283 na ilikuwa bado inateremka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mshauri mzuri sana ni yule tuliyempata kutoka *Commonwealth*. Yeye alitushauri kwamba, mikataba hii mnayoiweka bei ya *troll ounce* moja itakapopita, dola 350 lazima mu-*impose windfall tax* kwa sababu hawa watakuwa wanapata faida zaidi kuliko mlivyo kuwa mnategemea. Lakini mshauri wa *World Bank* alikataa katakata na kwa wakati ule ilikuwa lazima wamsikilize yeye na ametufikisha hapa tulipo. Kwa hiyo, kuna ugumu mkubwa sana ambao nina hakika una chanzo chake na sasa hivi ni wakati muafaka Serikali waanze kulitatua hilo tatizo. Limekuwa ni kero kwa wananchi, uwekezaji sasa umekuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni tatizo la *TANESCO*. Kama walivyoanza, basi waendelee kwenye mikataba mingine. Hii mikataba kwa kweli ukiangalia sana dalili zote za rushwa zilikuwepo. Nitatoa mfano mmoja tu. Ukienda Mwanza, kuna shamba tunaliita la *TANESCO*, limejaa jenereta arobaini, *under normal circumstances* mimi sio mhandisi, ku-power generator za kukupa 40 megawatt na ku-power generator mbili za kukupa *twenty times two*, nadhani ni rahisi ku-operate generator mbili kuliko ku-operate generator 40 kwa sababu *tear and wear consumption* ya mafuta, zile *losses unazozipata*, kwa sababu ya *efficiency* ya *engine* na *generator* huwa haiko *hundred percent*. Utakuta ni matatizo makubwa. Sasa nashindwa kuelewa, *TANESCO* wana tatizo la *planning* au nao tuwaweke kwenye hilo group. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu *you can not believe it*, zile jenereta zilitoka China, zililetwa kwa ndege na zile za *Dowans* sijui za *Richmond* na zenewe zililetwa kwa ndege ambayo iliashiria kwamba tuna matatizo kwenye *planning*, hatuwezi ku-*forecast*. Sasa namna hiyo ni *fire fighting* kila siku na tunapata taabu sana nchi ambazo tulikuwa nazo *level* moja miaka ya 1960, leo ziko mbali sana na ni kwa sababu ya migongano, huyu anavuta kamba huku, huyu anavuta kamba huku, matokeo yake tunastukia wote tunasimama katikati. Kama wasipoangushwa kama jana alivyotueleza Mheshimiwa Spika, Timu ya Bunge ikavuka upande mmoja wakaanguka wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika Mheshimiwa Waziri Mkuu mpya ni mtu mzuri sana, atajaribu ile *function* ya ku-coordinate, maana hapa ni tatizo la ku-coordination tu. Unakuta mmoja anaweka *negative*, mwingine anaweka *positive* ina-cancel. Kwa hiyo, hatuwezi kwenda mbele, nina hakika Waheshimiwa hili watalichukua kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri anifafanulie, kuna miradi yangu ya umeme kwenye Jimbo la Ilemela Wilaya ya Ilemela, anifafanulie. Bahati nzuri nina mkataba wa *MCC* na Tanzania. *Component (c)* kwenye *energy inazungumzia juu ya Mkoa wa Mwanza*, kifungu kidogo cha (2), “*Construction of up to 247 distribution line extensions consisting of new 33KV, 11KV na low voltage lines and customer connections in the six regions*”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba tu anifafanulie, mradi wangu wa umeme kutoka Kisesa kwenda Kayenze na Kayenze kwenda Igombe umo. Kama haumo, nitamuunga mkono nusu, akija kunihakikishia nampa na nusu nyingine. Maana ilikuwa ni ahadi, tumewaaahidi wananchi tukawaamini wakatupa kura na bahati nzuri tumepata fedha za uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, siwezi kuchukua muda wote, ni kuhusu *TANESCO*. Naomba sana ama tatizo tuliwaingiza kama nchi, maana *TANESCO* wanatakiwa ku-compete. Hii mikataba ya *IPTL* na nini mkimaliza kuifuta madeni yanayobaki, basi Hazina iyachukue. Hawa ndiyo wataweza ku-compete na tutaweza ku-measure performance yao, lakini sasa hivi wapo *overburden* na madeni na nadhani hata *EWURA* wanapata taabu sana jinsi ya ku-compute bei wanapoomba kuongeza kwa sababu *burden* ya madeni ni kubwa sana na ililetwa tu basi, bahati mbaya sana wanasiwa

tunawaingilia sana. Lakini kama wanakwenda kwenye ushindani wa kweli, nina hakika kwamba inabidi tufike mahali tuwaache wafanye kazi kibashara na waweze ku-*compete* na wale ambao tuliwakubalia kwamba wanaweza kuja kufanya hiyo biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni *Tanzanite*. Hii sekta ya madini inashangaza sana. *Tanzanite* inachimbwa Tanzania tu. Duniani kote ukikuta *Tanzanite* jua ni ya Mererani, lakini ukiangalia *volume* ya *Tanzania Trade* ukiacha kwenye sekondari, maana baada ya kuwa *processed* imekatwa na kadhalika nina hakika tusingetakiwa kuwa na kipato chini ya dola bilioni mbili na nusu au tatu. Sasa hizi fedha zinakwenda wapi? Maana kama hatuwezi kusimamia vizuri, basi yafukiwe yale mashimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere aliuliza huko nyuma kwamba, kwa nini wanashindwa kuchimba dhahabu? Yalifungwa! Nakumbuka Geita *Goldmine* ilifungwa mara ya kwanza na sio kwamba dhahabu ilikwisha. Ni kwa sababu namna hii mnatureleka vibaya, watakuja kutulilia kwenye makaburi yetu kwamba hawa watu walikuwa wanafanya nini? Nadhani *it is high time* tuangalie kweli baadhi ya uwekezaji unatusaidia au unatudidimiza na kama unatudidimiza afadhali udidimizwe kwa ile *sustainable* kudidimizwa. Hii tunadidimia kabisa na kutu-*perish*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana watupe majibu mazuri. Nina hakika wana nia njema na kwa Serikali hii tunayo matumaini makubwa kwamba watafanya kazi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja kwa nusu mpaka nipate majibu. (*Makofi*)

MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami angalau kidogo nichangie kuhusu bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwa maoni yangu nahisi ina mapungufu kidogo. Ina mapungufu kwa sababu kuna mambo ambayo nahisi ni *National issues* ambazo hakuzzungumza. Hapa ninao muhtasari wa taarifa ya utekelezaji wa makadirio ya mapato na maombi ya fedha ya matumizi katika Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo taarifa hii tuliletewa sisi Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 41, naomba ninukuu. Inasema hivi: “Utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.” Anasema: “Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wameridhia uteuzi wa Mshauri Mwelekezi atakayeshauri kuhusu mgawanyo wa mapato yatokanayo na rasilimali ya mafuta ili mkataba wa kazi hiyo ukamilike kama ilivyopangwa mwezi Septemba, 2008.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijiuliza, ikiwa huyu Mshauri Mwelekezi amechukuliwa kwa masuala ya mafuta tu, nikajiuliza swali moja, Katiba Ibara ya (4) katika nyongeza ya kwanza, kifungu kidogo cha (15) kimefutwa. Lakini kumbukumbu zangu hazionyeshi kwamba ibara hiyo imefutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hiyo inasema kwamba, mafuta na gesi asilia ni masuala ya Muungano. Sasa ikiwa kweli mafuta na gesi asilia ni masuala ya Muungano, mbona huyu Mshauri hakuelekeza kuhusu mgawanyo wa mapato yatokanayo na rasilimali ya gesi. Hilo ni kosa, ni kosa kubwa sana na haya ndiyo yanayofanya siku zote Wazanzibar wakawa wanasema Tanzania Bara inawaonea Wazanzibar, ni kwa mambo kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi, kumbukumbu zangu zinaniambia kwamba ilichimbwa au ilianza kuvunwa kuanzia mwaka 2004 na kuanzia 2004 hadi leo gesi hiyo bado inaendelea kuvunwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bakary, nikukumbushe tu kwamba, hiki unachojaribu kukisoma wewe, tunachojadili hapa ni hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Unachokisema ni kutokana na *presentation* ya hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo kwenye ratiba watakuja, huwezi kuvumilia mpaka wakati huo ili upate majibu muafaka?

MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hii ni Wizara ya Nishati na Madini na gesi inahusika katika Wizara hii na ndiyo maana hata katika Kitabu chake Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala la gesi, kwa hiyo, nimeona ni vizuri na hapa nikalizingumza. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Basi nakuomba urudie tena pale unaposema kwamba Watanzania Bara wanaonea Zanzibar kwa kunukuu Katiba. Sio vizuri sana Waheshimiwa Wabunge kutoa kauli ambazo zinakufanya hata mchango wako..., hebu panyooshe pale unaposema kwamba Watanzania Bara wanawaonea Wazanzibar na kwa kunukuu Katiba. (*Makofi*)

MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichosema ni kwamba Katiba inasema, suala la gesi na suala la mafuta ni masuala ya Muungano. Lakini katika hiki kifungu ambacho nimekisema kwamba huyu Mshauri Mwelekezi haikusemwa kwamba ye ye pia atashauri Serikali kuhusu mgawanyo wa mapato yatokanayo na gesi. Sasa naomba kutoka hapo niendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mshauri huyu ilisemekana kwamba na ye ye amepewa jukumu hili la kushauri kuhusu mgawanyo wa gesi na gesi kama nilivyosema ilichimbwa au ilianza kuvunwa kuanzia mwaka 2004 na kuanzia mwaka 2004 mpaka leo ni fedha nyingi sana ambazo zimepatikana kwa mauzo ya gesi.

Ninachotaka kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba: Je, ni kiasi gani Serikali imepata kutokana na mavuno haya ya gesi? Je, katika mavuno haya au katika

fedha hizi ambazo zimepatikana, ni kiasi gani ambacho baada ya kutoa *production cost* na mambo mengine kama hayo ile faida ni kiasi gani ambayo imepewa Zanzibar kama sehemu moja ya Muungano? Je, gesi nayo ni sehemu ya Muungano na pia ni kiasi gani ambacho Serikali ya Jamhuri ya Muungano upande wa Tanzania Bara wamepata kutokana na mavuno hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la zaidi ni kwamba, ikiwa fedha hizi Zanzibar haijapata kitu ambacho nina hakika mpaka leo Zanzibar haijapata hata senti moja: Je, Serikali itatuambia nini hapa? Wataweka au wanazo kumbukumbu ambazo wanaweza kutulipa wakati wowote kuanzia leo? (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nizungumzie kidogo kuhusu suala hili la *PSA*, yaani *Production Sharing Agreement*. Kwa mujibu wa mikataba, *PSA* ni kitu ambacho kinanufaisha wale ambao wanakuwa *involved* katika masuala hayo. Sasa hapa *PSA* mara nyngi ni *TPDC* ambayo inahusika nayo. *TPDC* ninavyoilewa sio chombo cha Muungano. Sasa hapa kuna kosa kubwa ambalo naomba nilizungumze.

Kwanza, ikiwa *TPDC* sio chombo cha Muungano: Je, kwa nini chombo hiki kikawekwa kwamba ni chombo ambacho kinashughulikia masuala haya ya mafuta na masuala ya gesi ambayo ni ya Muungano? (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kwamba, katika suala hili *TPDC* mara nyngi inapata kitu ambacho, katika sheria mpya ya *EWURA* inatoa fursa ya uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo. Sasa ikiwa *EWURA* inatoa fursa ya uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ambapo Mfuko huu unatumia na *TPDC*, napenda kujua hawa *TPDC* wanaisaidia vipi Zanzibar kutokana na Mfuko huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho napenda kuzungumzia ni kwamba, hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia sana kuhusu *sub-marine cable* ambazo zinataka kuwekwa hasa alipozungumzia *sub-marine cable* ya Unguja ambayo *ita-cost* kiasi cha dola za Kimarekani milioni 63.

Sasa nilikuwa nataka kujua ikiwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano imezungumzia suala la *sub-marine cable* kutoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar. Je, huu mradi ambao tulikuwa tunauzungumzia siku nyngi kuhusu *sub-marine cable* kutoka Tanga kwenda Pemba mbona haukuzungumzwa na utaanza lini? Ikiwa mradi huu upo, ni kwa nini Mheshimiwa Waziri hakuzungumzia suala hilo au ataniambia kwamba mradi huu ni mpaka *sub-marine cable* ya kutoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar umalizike ndiyo ule wa kutoka Tanga kwenda Pemba ndiyo uanze?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la majanga ambayo yanatokea mara kwa mara. Nafikiri janga linapotokea na linapokuwa kubwa ninavyofikiri ni kwamba Serikali inawajibu kwa kuwaarifu au kuwajulisha wananchi wake. Hivi karibuni kulikuwa na janga kubwa ambalo naweza kusema kwa upande wangu la kukosekana kwa umeme Kisiwani Zanzibar. Sasa katika janga hili

tulisikia mambo mengi tu. La kwanza, ni kwamba pengine kosa hilo liliabishwa na *TANESCO* na magazeti yaliandika, watu walisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, *TANESCO* walisema kwamba kosa hili ni la Zanzibar, magazeti yaliandika na watu walisema. Sasa nilikuwa napenda nijue kosa hasa lilikuwa la nani na hatua gani zilichukuliwa ili kurekebisha kosa hili? Kwa sababu ikiwa kweli kuna makosa kwa chombo kimoja chochote kati ya hivyo, nafikiri chombo kingine ambacho kinahusika ni vyema kikaanza kufanya matayarisho ili waweze kudai fidia. Nafikiri kitu kama hiki kingeelezwa na watu wakajua kwamba kutokana na matatizo haya ni kosa la chombo fulani, basi ingekuwa vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la Wizara hii, kuna mkataba unaoitwa *United Nations Convention on the Law of Sea*. Katika mkataba huu, Tanzania ni *member* na katika mkataba huu kuna kifungu ambacho kinasema kwamba pale nchi mwanachama anapokuwa na *potential ya natural resources*, basi nchi hiyo inaweza kuomba *extra two hundred miles* mbali na ile *exclusive economic zone*. Sasa kwa sababu Tanzania ina *potential ya natural resources*: Je, suala hili wameshaanza kulichukua au bado?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kifungu ambacho kinasema kwamba, ikiwa utachelewa, basi mwenzako na hapa Kenya wanawenza kuomba na kuchukua *two hundred miles* hizo au kama wote hawakufanya, basi kitakachofanywa itakuwa chini ya *International Sea Bed*. Sasa je, Tanzania wameshaomba suala hili au bado? Kama bado, ni hatua gani watachukua ili kuzipata hizi *two hundred miles* ambazo ni zaidi ya zile za *exclusive economic zone*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Bakary kwa mchango wako. Nitoe tu maelekezo ya jumla ya kitu, ni vizuri kila mchangiaji kuwa makini kutotoa *sweeping statement* ambazo zinaweza kuleta mtifaruku ambao hauna sababu. Kwa hiyo, tungependa jioni ya leo na hata michango inayofuata kuwa makini kwa nafasi yetu ya Ubunge kuzungumza vitu ambavyo haviwezi kutuletea migawanyiko ambayo haina sababu. (*Makofi*)

MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kuniruhusu niweze kuzungumza mchana wa leo. Kwanza, nianze kwa kumpa pongezi Mheshimiwa Waziri kwa kutoa mada ambayo niliona inaleta matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Wakuu wa Idara, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri kutayarisha hotuba ambayo ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. Naunga mkono hoja kwa sababu kile kilichoandikwa kwenye hotuba kwa kweli kimenipa matumaini, lakini baada ya hapo nianze kuzungumzia matatizo ya umeme katika Wilaya

ya Ngara. Ni kweli kwamba Ngara Wilayani kuna umeme, lakini huu umeme ulikuwa uzalishe *megawatts* mbili, lakini baada ya muda *megawatts* mbili hazikuweza kuzalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya muda mfupi, mashine moja iliharibika na kwa sasa kinachozalishwa ni *megawatt* moja. Sasa *megawatt* moja hii ukiigawa kwa sehemu ambazo zina umeme tayari, umeme hautoshi. Kwa sasa hivi umeme unafika kijiji au mji unaoitwa Muhweza na haujafika Kabanga *Border*, Mabawe, Mugoma, Lusumo *Border* na Rulenge. Tunachokiomba ni kwamba, angalau umeme upelekwe mpaka kwenye vijiji ambavyo tuliahidiwa na Rais Mkapa alipokuwa madarakani. Hili ni tatizo la siku nyingi ambalo naomba lishughulikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ninachotaka kuzungumza ni kwamba, Januari, 2008 Mheshimiwa Rais Kikwete alipotembelea Wilaya ya Ngara akaahidi kwamba itakapofika Desemba, 2008 Kabanga *Border* watakuwa na umeme.

Ninachomwomba Mheshimiwa Waziri ni kwamba afuatilie ahadi hii, ahakikishe kwamba, Kabanga *Border* kuna umeme kabla ya Desemba. Nimeshaandika barua kuhusu hili na nimeshajibiwa na kuahidiwa, lakini inaonekana hajjatekelezeka. Kwa hiyo, nasisitiza kwamba, Waziri mhusika ambaye ni ndugu yangu Mheshimiwa Ngeleja afuatilie na ahakikishe kwamba kabla ya Desemba, 2008 Kabanga *Border* wapate umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimaliza hilo naona nizungumzie *Kabanga Nickel*. *Kabanga Nickel* ni mgodi wa *nickel* ambao utakuwa mkubwa kuliko yote Afrika. Katika gazeti la *African* la tarehe 14 April, imeandikwa kwamba *Ngara billed Africa's biggest nickel mine*. Katika makala hiyo *Barrick Gold Tanzania* wameahidi kwamba watashughulikia uchimbaji wa *nickel* mwaka huu, wataanza 2008 kujenga huo mgodi na by 2009 na 2010 mgodi utakuwa umeshaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba, Mgodi wa *Kabanga Nickel* unahitaji umeme wa MW 45. Kwa sasa hivi Ngara inazalisha umeme wa MW2 na hata tukipewa hiyo *machine* ambayo inatoka Mtwara kuja Ngara hatuwezi kuzalisha umeme wa MW 45 ambao tunauhitaji kwa ajili ya *ku-develop* Mgodi wa *Kabanga Nickel*. Kwa hiyo, nawaomba Mheshimiwa Waziri na Serikali wajipange ili tuweze kupata umeme wa MW 45 ili tuweze kufaidika na mgodi wa *Kabanga Nickel*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie umeme wa *Rusumo Falls* ambao Mheshimiwa Waziri ameizungumzia kwenye ukurasa wa 18 kwenye *Budget Speech*. Amesema hivi, nanukuu: “Mipango ya muda wa kati kulingana na *PSMP* inahusisha miradi kadhaa na Rusumo ikiwemo MW 60.” Mwisho wa kunukuu. Ninachouliza ni kwamba, hizi MW 60, umeme huu utapatikana mwaka 2009, 2019, utapatikana 2011 au 2012.

Tunachokiomba ni kwamba tujue lini hizi MW 60 zitapatikana kabla ya mwaka 2010 na suala zima la matatizo ya umeme katika Wilaya ya Ngara litakuwa limetatuliwa.

Tutaeneza umeme vijiji vyote vya Wilaya ya Ngara ambavyo vinahitaji *MW* ambazo hazizidi 10. Katika *MW* hizo 60 tutapeleka *MW* 45 katika Mgodi wa *Kabanga Nickel*. Kwa hiyo, tutakuwa tumetatua matatizo yote ya mahitaji ya umeme ya Wilaya ya Ngara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoomba, naomba maelezo kutoka Waziri ndugu yangu Mheshimiwa William Ngeleja, hizi *MW* 60 ambazo zitatokana na Rusumo Falls tutazipata lini? Tukiweza kuzipata mwaka kesho au mwaka unaofuata tutakuwa tumetatua matatizo yote ya mahitaji ya umeme katika Wilaya ya Ngara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nzungumzie *Kabanga Nickel*, *Kabanga Nickel* ni mgodi mkubwa katika Afrika. *Nickel* iko kilomita moja na nusu chini ya ardhi kutokana na *data sheet* niliyonayo. *It is 1.5 kilometer under the ground*. Hii siyo dhahabu ambayo unaweza kuchimba tu juu ya ardhi ukapata. Hii ni *heavy investment mine* ambayo inahitaji uwekezaji wa hali ya juu ndiyo sababu tunahitaji umeme wa *MW* 45.

Wakati nazungumzia na aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini wakati huo Mheshimiwa Nazir Karamagi alikuwa amenieleza ya kwamba atachukua umeme kutoka somewhere Shinyanga, akauleta Westwards mpaka *Kabanga Nickel* na utakuwa unaweza kabisa kuwezesha kuchimba hayo madini. Sasa sijui huo umeme au mipango hiyo imeishia wapi. Kama na yenyewe inawezekana, ingawaje najua kwamba *line* ya kutoka Mtera mpaka Shinyanga iko *overloaded by 10%*.

Kwa hiyo, inabidi kuwe na *line* nyiningine ya kuleta umeme mpaka Shinyanga and then uende Magharibi mpaka ufile *Kabanga Nickel*. Which ever come earlier tukipata umeme wa Rusumo mapema sawa. Lakini kama huo utachelewa, basi tupate huo umeme wa kutoka Shinyanga ambao utakuwa umeunganishwa na National Grid ili mradi tuweze kuchimba madini ya *Nickel* mapema iwezekanavyo.

Faida za *Kabanga Nickel*, kwa sababu *Kabanga Nickel* ni mgodi mkubwa, utaajiri watu 1,000 wakati wa ujenzi wa Mgodi. Watu 1,000 mpaka 2,000 imeandikwa kwenye *data sheet* ya *Kabanga Nickel* ambayo nimeshaieleza katika Wilaya yangu ya Ngara. Tutapata unafuu vile vile wa kupata *training opportunities* wakati unajenga mgodi utahitaji mafundi wa aina zote. Utahitaji mafundi wa ujenzi, utahitaji mafundi wa umeme, utahitaji mafundi bomba, utahitaji mafundi wa magari na madereva na utahitaji *information technologies*. Kwa hiyo, itakuwa *nucleus* ya kuendeleza Wilaya ya Ngara. Tunaungoja huo mradi ili Ngara angalau iweze kuibuka na iweze kuendelea kwa kasi kama Ilani ya Uchaguzi inavyosema, Kasi Mpya, Ari Mpya na Nguvu Mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Ngara watapata mahali pa kuuzia vyakula. Kwa mfano, ukiwa na watu 1,000 wanakula kuku, watakula kuku 250 kwa siku, hiyo ni *consumption* kubwa kweli kweli kwa Wilaya ya Ngara. Tutapata mahali pa kuuzia vyakula vyetu, tutapata mahali pa kuuzia mbuzi, ng'ombe na maharage. Kwa hiyo, mgodi uta-stimulate production ya vyakula vya aina mbalimbali. Ndiyo sababu nasisitiza ya kwamba tusaidiane katika kuleta maendeleo katika Wilaya ya Ngara kwa

kujenga Mji mdogo wa *Kabanga Nickel* ili tuweze ku-stimulate maendeleo katika Wilaya ya Ngara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Prof. Feetham Banyikwa, nakushukuru sana. Kama nilivyosema awali, Mheshimiwa Balozi Getrude Ibengwe Mongella atafuatiwa na Mheshimiwa John Momose Cheyo na Mheshimiwa Getrude Mongella - Rais wa Bunge la Afrika.

MHE. BALOZI DR. GETRUDE I.. MONGELLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu. Kwanza kabisa, ni muda mrefu sijakuwepo pamoja nanyi. Naomba niseme tu, *I missed you very much.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo, nasema tu ni kwa sababu tulikuwa na kazi muhimu na ninapenda niseme tangu mwanzo ya kwamba Kikao cha Wakuu wa Nchi za Afrika kilikuwa Kikao kizito na Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alionyesha uhodari wake wa kuendesha Kikao hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Waziri wa Nishati na Madini na Naibu Waziri wake kwa kuwasilisha vizuri hotuba hii na kuiandaa pamoja na wale wote waliowasadidua kuiandaa hotuba hii. Lakini hapo hapo naomba tu pia niwashukuru wale amba wanashughulikia umeme na hasa wale amba wamesaidia kufikisha uamuzi wa mwisho wa Sakata la *Richmond*. Hili suala la watu waliotuletea mikataba feki wasiendelee kuionyonya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nadhani hata ile mitambo tunge-*confiscate*, wangeniuliza mimi ibaki hapa hapa, hakuna sababu tena ya kuiondoa hapa baada ya kutufanya ulangizi wa kutosha, ingebaki hapa hapa, siku tukipata dharura tuitumie vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ningependa pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa kupata mtoto wa kike anaongeza *a gender balance.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa labda hili niliseme mwanzoni kabisa leo walipokuwa wanatambulishwa Wakuu wa Vitengo mbalimbali katika Wizara hii, hakukuwa na mwanamke hata mmoja. Swali, kwa nini katika uongozi wote wa juu wa Wizara ya Nishati na Madini niliousikia hakukuwa na mwanamke hata mmoja. Je, akinamama hawajasoma katika fani hizo au ni matatizo tu ya ubaguzi wa kijinsia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na pongezi nilizompa na kwa sababu amepata mtoto wa kike sasa alitazame sana hili kwa makini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda nichukue nafasi ya pekee kuwashukuru Wizara ya Nishati na Madini na kuishukuru Serikali ya Tanzania ambayo kwa ushirikiano na Nchi ya Spain wameweza kuvusha umeme mpaka kwenye Kisiwa kikubwa cha Ukerewe – Nansio. Wameweza sasa kwa kushirikiana na Sweden, wameanza maandalizi ya kusambaza umeme katika Kisiwa hiki kikubwa tukiwa na matumaini ya kwamba hatua pili ni kuingiza umeme katika Kisiwa cha Ukala na baadaye kwa kutumia njia tofauti kama hivi, *Solar Energy* na upopo waweze kusambaza katika Visiwa vingine zaidi ya Visiwa 28 ambavyo ndivyo vinafanya Wilaya ya Ukerewe. Nawashukuru sana, tumeshirikiana kwa karibu na tumefanya kazi kwa karibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa basi niseme hivi, kila ninaposikiliza Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambaو hawajapata umeme, wanaomba umeme kwa nguvu zote na mimi ninawaunga mkono. Nimekuta kama ndugu yangu pale kutoka Ngara ni giza tupu hajapelekewa umeme. Peramiho kila mara Mwenyekiti wetu anapiga kelele, kwenda kwa Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba kule naye anapiga kelele, ukienda Kigoma, kila mtu anapiga kelele na mkwe wangu hapa naye anasema Namtumbo na Pwani na kila mahali wanapiga kelele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu hata kama Ukerewe peke yake itapata umeme, hatuwezi tukaendelea kama wengine wote hawajapata umeme. Kwa hiyo, ndiyo maana nataka niweke msingi. Tunaposema kumekuwa na ongezeko la mapato kutokana na umeme na tukazungumzia pia kwamba uzalishaji wa umeme umeongezeka, swalí ni kwamba, umeongezeka kwa kiasi gani kama hao wengine wanaotoka katika sehemu nyingine za Tanzania hawajapata umeme.

Mimi nadhani bado tunapaswa kufanya mkakati utakaotuwezesha kujibu kiu ya kila mtu kupata umeme. Bila umeme, hakuna maendeleo. Kwa muda mfupi tulipata umeme, Nansio ukija katika Wilaya ya Ukerewe utaona kulivyokuwa na chachu ya maendeleo na kwa kawaida WakereWE tunapenda maendeleo. Sasa umeme umeongeza kasi hiyo, kumeanza kuwa na mabadiliko ya nyumba, kumbe kunapokuwa hakuna umeme hata nyumba zinakuwa hivyo hivyo za nyasi. Lakini sasa hivi kuna kasi kubwa ya kujenga nyumba zilizo bora kwa sababu kila mtu nataka kuweka umeme katika nyumba yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kumetokea sasa viwanda vidogo vidogo ambavyo vinapaswa kuwasaidia katika kuwaondoa watu katika umaskini. Kwa hiyo, ninaungana na wale ambaو bado wanalia na kiu ya umeme. Ninaomba Wizara hii ikamilishe upesi mradi wa Ukerewe ili waweze kuhamia kwenye maeneo mengine. Naomba kabisa ifikapo mwezi Desemba, 2008 wakati wa Krismas mradi wa Ukerewe uwe umekamilika na wahamie mahali pengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninapenda pia niseme katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Wizara imetueleza kwamba kumekuwa na Mpango Maalum wa Kueneza umeme katika nchi. Ni matumaini yangu kwamba huo Mpango utaletwa, tuufahamu. Tupewe nakala ili tuweze kuona jinsi tunapiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzoefu niliupata katika Mradi huo wa Ukerewe ambao kwa kweli umenufaisha na Jimbo la Mwibara, kwa sababu sisi ni Kisiwa, umeme usingewenza kupita kutoka Bunda bila kupertia eneo lingine. Kwa hiyo, umeme ulipitia Bunda na watu wa Bunda nao wamenufaika na umeme unaokwenda Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu niliokuwa nao ambao nataka niwasifu wananchi wa Wilaya ya Ukerewe ni kwamba mahali pengine walijitolea kutoa nafasi ya umeme kupita. Kwa hiyo, napenda niwashukuru sana wananchi wa Wilaya ya Ukerewe na ninadhani na wananchi wa sehemu nyingine watajitatidi kufanya hivyo. Hiyo inasaidia kupunguza gharama za usambazaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pale ambapo umeme umepita sehemu ambazo wananchi wanastahili kulipwa, ningependa waharakishe kwa sababu mradi huu umeanza muda mrefu na sio kweli kwamba hakukuwa na bajeti ya kuwalipa wale ambao waliwekewa ‘X’ kwenye majengo yao na katika mali zao nyingine. Ningependa hilo suala liishe, walipwe, tuendelee hivyo hivyo na tutaendelea kuwapisha na tutaendelea kushirikiano nao, lakini na wao wanapotoa ahadi kwa mwananchi ya kwamba banda lake hilo watalilipa. Ningemba watekeleze haraka kwa sababu linatuletea utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni suala la mafuta. Mafuta yanapanda bei, kwa hiyo, ni vizuri tukalieleza hili vizuri kwa sababu kupanda kwa bei ya mafuta, nadhani wiki iliyopita ilikuwa ni *dollar* 143 kwa pipa. Lakini *estimation* tulizokuwa tunazungumza na hao wenye mafuta kwa sababu tulikuwa sehemu za watu wenye mafuta, wanasema ya kwamba huenda bei ikafika *dollar* 150 kwa pipa hivi karibuni. Sasa *issue* iko hapo. Sio suala la kukimbizana kununua mafuta ni suala la kuhakikisha tunakuwa na nishati mbadala kama hatuna mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishati mbadala tunayo, gesi. Gesi katika nchi nyingine ndiyo nishati ambayo inatakiwa duniani kote. Kwa hiyo, sisi tunayo Songo songo. Kwa hiyo, ukisoma vitabu, sasa sijui mwaka wa ngapi, ninasoma Songo Songo, *Mnazi-Bay* unayosoma mambo yote haya kwenye vitabu. Huu siyo wakati ambao tungeacha kila kitu tuhakikishe kwamba hiyo gesi inatolewa inatumika ndani ya nchi, lakini pia tunafanya uwezekano wa kuipeleka nchi za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemba kwa kweli Wizara itafiti nchi ambazo zinaweza kutumia *natural gas* katika kutengeneza nishati, lakini wasituletee tena mikataba ile ya ajabu ajabu. Iwe mikataba mizuri na duniani kuna watu wapo tayari kuwekeza katika *natural gas* ili tuweze kushindana na hii hatari ya kupanda kwa bei ya mafuta. Ni hatari kama wale wakubwa kama zile nchi nane kubwa duniani zinahaha juu ya bei ya mafuta, zinahaha juu ya chakula. Kwa sababu kuna mambo mawili sasa duniani yanafanya nchi kama Marekani, Japan, nchi zote za Ulaya zihahesi ni mafuta na chakula, na haya yote yana uhusiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chakula kina uhusiano hata kama unatumia jembe la mkono kama mafuta yanapanda bei utasindikaje mazao hayo? Utayasafirisha namna gani kutoka kwenye mashamba ya watu na kuyafikisha kwenye masoko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu kweli Wizara hii iangalie na mimi ninasema wasiogope kwa sababu ya uzoefu wa mikataba ya ovyo, wasiogope kuwatafuta watu wengine ambao wanaweza kuwekeza ili tuharakishe matumizi ya gesi ya Songo Songo na gesi ambayo imeja katika nchi yetu ambayo Mungu alitujalia kutupa rasilimali nydingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sasa niseme kwamba Wizara hii ni muhimu, sijui kama tumekuwa na mpango mpana wa kuangalia jinsi Wizara hii peke yake kama ingeimarishwa ingeweza kutuondolea hata umaskini. Tunapeleka fedha nydingi katika kupanda miti, lakini ni vizuri tupande miti. Miti anaweza kupanda hata mtu mmoja mmoja. Lakini suala la kuweka nishati ni la muhimu kwani itamwezesha mwananchi asikate miti. Kwa sababu mimi sioni nitawezaje kuacha kupikia kuni kama sina nishati nydingine. Siwezi kufa na njaa eti ninalinda mazingira.

Kwa hiyo, dawa iliyopo ni nishati ambayo inapaswa kuwa katika Wizara hii. Nadhani lazima tutazame Kitaifa namna gani tutaimarisha Wizara hii ili iweze kwenda kwa kasi kubwa zaidi na matokeo yake yaweze kuonekana katika uzalishaji maji, matokeo yake yaweze kuonekana katika kuondoa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni la muhimu kwa wingi ni la madini. Madini jamani Mungu ametupa tu huko ndani ya ardhi, kamwaga na hakuwa amekosea kuyamwaga Tanzania na hasa hakuwa amekosea kuwamwagia Wasukuma dhahabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo unakwenda kwenye maeneo hayo mpaka uambiwe huku ndiko dhahabu inakotoka, hakuna kinachoonekana ambacho kinatofautisha eneo la dhahabu na lisilokuwa la dhahabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sehemu nydingine ukiambiwa huko ndiko kunakotoka kitu fulani angalau unaona dalili hata kama ukienda Ukerewe kwamba huko ndiko wanakovua samaki angalau kuna harufu ya samaki. Kwa hiyo, katika maeneo hayo tunayotegemea kwamba katika maeneo hayo ambayo yanazalisha dhahabu tusioneane haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella nakushukuru sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Ephraim Madeje atafuatia na Mheshimiwa Hasnain Gulamabass Dewji. Kwa sasa Mheshimiwa John Cheyo simwoni humu ndani. Mheshimiwa John Cheyo yupi. Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa Ephraim Madeje ajiandae. (*Makofi*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti najua ni mfupi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nafurahi kwamba umeweza kuniona pamoja na *size* yako. (*Makofi/Kicheko*)

Lakini pili, kabla sijatoa mchango wangu nataka kutumia nafasi hii kuwapa pole sana wakulima wa pamba kwamba bado wanahangaika na bei. Hapa kutoa taarifa kwa Serikali hatutauza pamba kwa bei ya Sh. 400/=. Kwa hiyo, jaribuni kutafuta njia nyingine tufike Sh. 500/= kama vile ilivyokuwa mwaka 2007. Hapo nimemaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nataka kutumia nafasi hii pia ku-*declare interest* kwamba mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Rais ya kudurusu utaratibu wa madini. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kututaja na kuangalia baadhi ya mambo ambayo tumesema katika ripoti hiyo.

Baada ya kusema hilo, nataka kumpongeza Mheshimiwa Rais ambaye ndiyo mwenye ripoti kwa kukubali ripoti hii iweze ikawekwa hadharani. Huu ni ujasiri na jambo hili linapaswa kupongezwa sana, lakini ni hatua njema. Serikali inayofichaficha mambo inaingia katika matatizo. Kwa hiyo, hapa nampongeza Mheshimiwa Rais sana kwa kufanya kitendo hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati huo huo mimi nilisikitishwa sana kama Mjumbe kuona kwamba ripoti yetu ilikuwa tayari katika *Website* ya baadhi ya Wazungu wanaoishi katika nchi hii. Mimi najiuliza hivi nchi hii inatawaliwa na nani na vyombo viko wapi? Huyu mtu anazidi kumwita hata Mheshimiwa Rais wetu tuliyemchagua kwamba “rafiki yangu” na anatoa maneno ya dhihaka. Mimi niliyekuwa zamani nakumbuka enzi za Nyerere kulikuwa na mtu mmoja aliyetoka Mauritius alisema kwamba Serikali ameiweka mfukoni. Rais wakati ule Mwalimu Julius Nyerere alisema ninakutia ndani na kesho saa 24 uwe uko kwenu. Mimi naona Serikali panapokuwa na dharau ya viongozi wa Taifa na Kamati kama hiyo iliyochanguliwa na Rais inadharauliwa na mtu anayepata faida kubwa sana katika nchi yetu, Serikali ipate ujasiri wa kumwambia mtu huyu *out*, ili haki itendeke katika Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, nataka kuchangia mambo yafuatayo:- kwanza kabisa Serikali igeuze Wazungu, wanasema *mindset* na hiyo *mindset* nataka Serikali igeuze ni kwamba kama mama Getrude Mongella alivyo sema na nashukuru nimezungumza baadaye ya Mheshimiwa Rais wa Bunge la Afrika kwamba Mungu hakukosea kutupa dhahabu, Mungu hakukosea kutupa almasi na hii almasi ni mali yetu na ni mali ya Serikali kwa niaba yetu. Kwa hiyo, mtindo wa Serikali kufikiri kwamba wanaoweza kutoa mali hii bila kuwa na hisa ndani, bila washiriki katika migodi mbalimbali mimi nafikiri ni fikra potofu na hatuangalii migodi yetu na hatupati faida.

Kwa hiyo, la kwanza kabisa ambalo nataka kusisitiza *mindset* ambayo igeuke ni kwamba Serikali ijione *deposit* au mashapo au dhahabu tuliyonayo huo ndiyo mtaji wa Watanzania. Mtaji huo wa Watanzania Mheshimiwa Waziri anafahamu ndiyo unatumika katika kukopea fedha na watu ambao wanakuja hapa kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo najua hata kwenye ripoti yetu ipo na ripoti ya Masha, katika ripoti ya Alex Stewart ipo, ukiona uwiano kati ya *equity* na *borrowing* ni kubwa ajabu mpaka mara nyingine laki mia moja na themanini na tano asilimia. Kwa hiyo, ndiyo kusema kwamba mtaji mdogo, lakini ukopaji mkubwa kufuatana na madini ambayo tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusione aibu. Kwa nini tuone aibu sisi kuwa na *share* katika migodi mbalimbali ya dhahabu, almasi? Katika Kamati tulisikitishwa sana kuona kwamba Serikali kwanza katika mgodi wa *Williamson Diamond* mwaka 1994 ilidanganywa na washiriki walioko sasa kwamba waliambiwa kwamba nyinyi mpunguze hisa zenu na mtupe miaka mitano msitutoze kodi mbalimbali na mwisho wa miaka 10 mtapata dola za Kimarekani milioni 12, kama vile *dividends* na nini. Mwisho wa miaka 10 *Willcroft* kuendesha *WDL* mgodi ule umekwenda kwa hasara ya milioni 23 *dollars*, leo tena Serikali inaambiwa mpunguze hisa zenu.

Tunajua mashapo kwanza yaliyo pale kwa *feasibility study* ya *Willcroft*, ni mashapu milioni nane. Tunajua *grade* yake ni *carat* sita kwa kila tani. Ukizidisha kwa hesabu hata za darasa la pili unaona kwamba pale tuna *carat* zaidi milioni 48. Tunaelezwa hata bei ya chini ambayo *Willcroft* inanunua *dollar* 100 kwa kila *carat* tuna 4.8 billion *dollars*.

Leo uniambie Mheshimiwa Waziri nazungumza kama pale ulivyozungumza kwenye *paragraph* 61 ya hotuba yako na *paragraph* 108 unazungumza kwa nia ya kuondoa hizi hisa 25. Utaachiaje bilioni 4.8 ukimkabidhi tu mtu kutoka *De Beers*? Naliomba Bunge hili, kwa hili kama vile Kamati ilivyosema, tuseme hapana kabisa na Watanzania wote wanansikia kwamba *Williamson Diamonds* ibakie angala Serikali ibakie na hisa 25. Iwe *clear* kabisa. (*Makofii*)

Sasa nayajua kwamba *lobbying* ni kubwa sana na viongozi wetu nawaomba utaratibu wa kukubali ukiwa sijui wapi kwa sababu mtu amekuja kuomba tungeacha tutumie utaratibu wa kuamini watalaam wetu waangalie kama ndiyo *proposal* sawa sawa bila shinikizo la viongozi wa aina yoyote, bila shinikizo la aina yoyote kutoka kwa washiriki ndani ya hii kuliko kugawa. Tunagawa bure mali ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu.

Hili Waheshimiwa Wabunge, naomba tuseme hapana kabisa. Sio hivyo tu, tumekimbia hisa zetu tulizokuwa nazo Bulyanhulu, nani asiyejua kwamba hata leo mimi nikipewa leseni ya madini tayari nimeshapata fedha? Angalia Bulyanhulu *Sutton Resources* wamechukua wameuza ile Bulyanhulu kwa shilingi milioni 388, hata chapa moja kwa kuingia Serikalini, Serikali inasema *goodbye* fedha.

Naona kila siku unatafuta fedha, kwa nini Mheshimiwa Waziri tukubali ku-*dilute*? Mimi naona Mheshimiwa Waziri shika hapo kama ni lazima upoteze Uwaziri wako sema

goodbye kuwa Waziri, lakini uwe na msimamo kwamba unaangalia mali zetu tulizopewa na Mwenyezi Mungu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiondoka hapo, nataka nisisitize tu kwamba katika baadhi ya washiriki..!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, uwe makini kwa ushauri wa namna hiyo.

MHE. JOHN M. CHEYO: Nataka kusisitiza, washiriki katika hii migodi isiwe tu Serikali. Nimefurahi katika hotuba yako kwamba, unataka *STAMICO* ifanye kazi na Kamati pia imelizungumzia jambo hilo. Hili ni jambo la kumpongeza Waziri, shika hapo. *STAMICO* ifanye kazi na iweze kushiriki katika migodi mbalimbali. Pawepo pia na Watanzania wa Kati, wachimbaji wadogo, hiyo ndio utasema kwamba mali tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, inakaa kwa Watanzania, sio utaratibu wa sasa ambao wewe mwenyewe unaufahamu.

Watu wanachimba katika *statistics* ulizotupa hapa, mwaka huu peke yake ni milioni 888; dhahabu na madini mengine yatapelekwa nje, fedha zote hizo wala hazirudi Tanzania. Fedha hizo zote kwa mikataba iliyopo zinakaa huko huko, jamani ni lini tutafunga macho tufanye biashara ambayo itawasaidia Watanzania? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Serikali kwa muda mrefu, imetumia kodi kama njia ya kuwavutia wawekezaji, utaratibu huu unatumalizia fedha. Kamati imesema kuwa, tuondokane na utaratibu huu. Ukiangalia utaratibu wa mfano, nafuu ya ziada ambayo Serikali imetoa jumla ya kodi ambayo tungepata kama pasingekuwa na utaratibu huo ni kama Dola za Marekani 265 milioni, ambayo ni sawa sawa na shilingi bilioni 320, ambayo ni sawa sawa kabisa na bajeti yako ya maendeleo ambayo umetuambia hapa. Tumeachana na hizo fedha, utaratibu haufai. Ukiangalia mambo ya *fuel levy*, hata hivyo, mwaka 2006/07 tumeachia bilioni 91, 2007/08 kwa nini sisi watu maskini ndio tutoe ruzuku kwa matajiri? Kwa nini Tanzania ndiyo itoe ruzuku kwa *Barrick* ambayo ni Kampuni tajiri?

Nakuomba uende katika baadhi ya mapendekezo; kuna vitu ambavyo unawenza kuvifanya kesho au mwisho wa Bunge hili, wakati wa Muswada wa Fedha, ukaondoa GN 99, vitu vingi ambavyo vimezungumzwa hapa na ripoti yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine wachimbaji wadogo, *in my opinion* nasema hili ni *time bomb*, tusipoangalia hapa nchi haitakalika. Kuna faida ya wachimbaji wadogo wote wale ambao wanachimba Bulyankulu, fedha yao ilikuwa inabaki hapa. Waliokuwa wanachimba Bulyankulu wale ndio wamejenga Kahama. Wale ndio wameweka mabati katika vijiji mbalimbali na walikuwa wanlisha maelfu kwa maelfu ya watu. Tuangalie hili. Nimefurahishwa kwamba umeangalia kama kuna uwezekano wa kuweka *revolving fund* kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji; ng'ang'ania hapo hapo. Hilo ni jambo zuri sana, lakini kwa usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Wizara hii ni kubwa mno. Kuna Wizara ya Nishati na matatizo lukuki na kuna Wizara ya Madini matatizo lukuki, Serikali ingefikiria kuziachanisha hizi Wizara. Mimi nafikiri kuna fedha nyingi sana ambazo tunawenza tukatoa ili kusaidia maendeleo ya nchi hii kwa upande wa madini. Pia kuna matatizo mengi ambayo lazima yaangaliwe katika upande wa nishati ili kuhakikisha kwamba, angalau nchi hii inaondokana na janga la kupandishwa mafuta na maisha ya wananchi sasa hivi hayawezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo, naomba ripoti hii na vitu vyote ambavyo tunesema vifanyiwe haraka, hii ni *business* ukingojea miezi sita yote ambayo tunesema huku hayatatusaidia. Ukingojea mwaka mmoja ni afadhali uchukue ripoti hii uweke kwenye majivu, basi moto uweze labda kuwasaidia watu wenye baridi. Nataka kusisitiza yaliyowekwa humu yafanyiwe kazi mara moja na tungependa sheria na vipengele ambavyo vinaweza kugeuzwa vigeuzwe.

Bunge hili lisingojee tena sijui tustadi mara ngapi, hakuna cha kustadi tumeshatosha na wananchi wameshatuambia haya mambo ya Kamati yametosha. Mambo ya kuangalia yametosha, fedha tulizotumia kuangalia ni nyingi mno, fanya kazi. Nakutakia kila la kheri mdogo wangu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Momose Cheyo, kwa kuunga mkono hoja. Mheshimiwa Mongella alizungumzia habari ya kuchelewa sana kwa maendeleo Usukuman. Mimi nakubaliana naye kwa sababu bado mauaji ya vikongwe, wenye macho mekundu yanaendelea kule na wanaendelea kuwaua albinos. Sasa anayefuatia hapa ni Mheshimiwa Madeje, baba yao Wasukuma.

MHE. EPHRAIM N. MADEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nitoe mchango wangu. Kwanza, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Ngeleja, kwa kuteuliwa kuwa Waziri na kwa kazi yake nzuri ambayo amekuwa akiifanya, kabla ya kuteuliwa na sasa akiwa Waziri Kamili. Pia nampongeza kwa hotuba nzuri aliyoitoa. (*Makofi*)

Hotuba hii imesheheni kazi waliyofanya katika mwaka uliopita katika kutekeleza yale ambayo yalikuwa yamepangwa, lakini pia imekuwa ni dira kwa kazi ambazo wamezipanga kwa ajili ya mwaka ujao. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nimpongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Malima, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, lakini pia kwa kazi nzuri ambayo anaifanya kwa ushirikiano na Waziri wake. Bila ya kuwasahau Katibu Mkuu, Watendaji Wakuu na Wafanyakazi kwa ujumla wa Wizara hii ambayo ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara hii kwa kukamilisha Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme Nchini, unaoitwa *Power System Master Plan*. Mambo yote ukitaka yaende vizuri, lazima uyafanye mipango (*planning*). Tukiangalia mpango huu, tunapata matumaini kwamba, sasa tunaelekea kule ambako tungependa kwenda. Mpango huu, unatoa matumaini kwamba, tutapata maendeleo ambayo

yatakuwa endelevu katika sekta hii. Pia inawezekana kabisa ukatusaidia tuondokane na ile tabia au yale mazoea ya zimamoto. Ni kama mwaka mmoja au miaka miwili iliyopita, nchi yetu ilikumbwa na ukame ikapata matatizo makubwa sana kwenye suala la umeme. Tulichofanya tuliwaita zimamoto. Matokeo yake nchi yetu imepata hasara kubwa sana. Matatizo ambayo tunajaribu kuyarekebisha sasa hivi lakini ni kama vile tumeshachelewa, hasara tumeshaipata. Kwa hiyo, tuna matumaini kwamba, Mpango huu utatutoa pale tulipokuwa na kutupeleka ambapo ni pazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nirudi hapa nyumbani kwangu; katika Jimbo la Dodoma Mjini au tuseme Manispaa ya Dodoma tuna bahati nzuri, lakini pia tuna bahati mbaya kwenye masuala ya umeme. Bahati nzuri kwa maana ya kwamba, kwa hapa mjini katikati hatuna malalamiko yoyote kuhusu umeme. *TANESCO* umeme wao ni wa uhakika na kazi yao tunaweza tukasema kwa wastani wanaifanya vizuri sana. Bahati mbaya ambayo naisemea ni kwamba, Jimbo la Dodoma Mjini au tuseme Manispaa ya Dodoma imezungukwa na vijiji visivyopungua 40, ambavyo havina umeme. Tumekwishatoa maombi kwenye Wizara na tukaahidiwa kwamba, yanashughulikiwa.

Sasa ningependa kurudia tu kwamba, kuna baadhi ya vijiji ambavyo viro katika orodha yetu na ambavyo kama tulivyokwishakubaliana kiujumla kwamba, vijiji ambavyo vinapitiwa na *National Grid Power Lines* ni vizuri vikapewa umeme. Sasa niliwhali kuuliza hata swalii kwenye Bunge hili na nikajibowi kwamba, mambo yanashughulikiwa kwa ajili ya vijiji vya Nkulabi, Mpunguzi na Matumbulu. Bahati nzuri, vijiji hivi haviko mbali sana na umeme ambao umeshapozwa, ambao uko kwenye Kiwanda cha Kutengeneza Kokoto pale Nyankali. Kwa hiyo, nina imani kabisa kwamba, Wizara inaweza ikalifanya kazi ombi hili ili umeme upatikane katika vijiji hivi. Pia tuliomba umeme kwa ajili ya vijiji vya Mbabala na Kikombo, navyo pia havipo mbali sana na maeneo ambayo umeme unaweza ukaunganishwa kwa bei ambayo sio mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zoezi la kupeleka umeme kwenye Wilaya Mpya ya Bahi na kwa kutumaini kwamba, umeme huo utaanzia Dodoma kuelekea huko; tunaomba vile vijiji ambavyo vitapitiwa na huo umeme, visisahauliwe kwa mantiki kwamba hiyo kazi ikifanyika sasa hivi, gharama bila shaka itakuwa nafuu lakini pia manufaa kwa wananchi yatakuwa ni makubwa. Vijihi hivyo ni Nala, Mbalawala, Chigongwe na Msembeta. Vijihi hivi kama vitapatiwa umeme, manufaa makubwa tutakayopata ni kwenye hizi shule zetu ambazo tumezianzisha. Kuna shule za sekondari takriban tano hivi ambazo zitanufaika na umeme huo. Pia kuna zahanati na vituo vya afya ambavyo umeme ni muhimu kwa shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nije kwenye suala moja ambalo linatukanganya, lakini pia linasikitisha kidogo. Kuna wananchi ambao wanaishi kwenye Kitongoji cha Chinyoyo, Kata ya Kilimani. Wanaishi katika makazi ambayo hayajapimwa lakini walio wengi wana nyumba ambazo ni za kisasa na ambazo kwa kila hali, zinastahili kuunganishwa na umeme. Cha kushangaza ni kwamba, *TANESCO* hapa Dodoma imekataa kuwaunganishia umeme wananchi hawa; tunashindwa kuelewa ni kwa sababu gain? Tukiangalia miji mingine, asilimia kubwa ya makazi ni *squatter areas*; mfano mbaya ni Dar es Salaam lakini watu wana umeme. Sasa kwa kawaida, sipendi

mtafaruku lakini katika hili, kijana wetu Mheshimiwa Ngeleja naomba nitoe tahadhari kwamba, tukishafika kwenye vifungu, kwa kweli tutaibana hiyo shilingi mpaka tupate maelezo ambayo yataturidhisha kwa nini wananchi hawajaruhusiwa kufaidi matunda ya nishati hususan umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, nina suala lingine moja ambalo linahusu mahitaji ya umeme kwenye Shule ya Sekondari ya Makutupora. Makutupora kwa bahati nzuri ina umeme na tuna shule yetu pale ambayo imeshakomaa, maana yake wameshatoa wanafunzi au wameshafanya mitihani ya *Form four* kama miaka mitatu, minne hivi na maendeleo yao kitaaluma sio mabaya. Shule hii inatarajiwa kupandishwa daraja iwe na *form five* na *six* katika mwaka ujao. Sasa kuna mpango wa kuweka umeme katika hii shule; tayari kazi kubwa imeshafanyika ya kufanya *internal wiring*, lakini *application ilipokwenda TANESCO* imeleta bili au tuseme ankara ya shilingi 11,072,000 ili kuunganisha huo umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hiyo ankara ni kwamba, shilingi 10,147,000 ni gharama za *TANESCO* za kuvuta umeme pale ulipo kuufikisha pale ambapo mita itawekwa kwa ajili ya hii shule. Gharama ambazo labda kwa uelewa wangu mdogo, zinatakiwa zibebwe na *TANESCO*. Sasa ukizileta kwenye Mradi kama huu amba ni wa kijamii, mimi naona si sahihi. Kwa hiyo, gharama halisi ambazo wazazi na wananchi wa pale wanatakiwa wabebe ni za *service line* labda na mita, lakini gharama za kuvuta huo umeme au kuweka nguzo kutoka barabarani mpaka ufile pale ni jukumu la *TANESCO*. Kibaya zaidi, katika ile barua imetolewa tahadhari kwamba, hivyo vifaa ina maana hizo nguzo na nyaya, zikishafungwa na *TANESCO* mali yote itakuwa bado ni ya *TANESCO* kwa mujibu wa sheria. Ombi letu kwa Mheshimiwa Waziri na kwa *TANESCO* ni kwamba, wajitahidi watafute hivyo vifaa ili wawapunguzie mzigo hawa Viongozi wa Makutupora Sekondari na vijana wetu, waondoe ile gharama ya milioni kumi ili hiyo milioni moja tuweze kuishughulikia sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja.
(*Makofii*)

MHE HASNAIN G. DEWJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu hapa. Kwanza kabisa, namshukuru Waziri kwa hotuba yake nzuri. Nawashukuru Watendaji wake wote kwa kuileta bajeti hii na kuipanga vizuri, nasema naunga hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nataka niongelee kuhusu Mradi wa Umeme wa Somanga Fungu. Mradi huu bado upo nyuma kwa miaka miwili sasa. Tumewaambiwa Wananchi wa Kilwa kwamba, pamoja na gesi asilia mliyokuwa nayo, mtapata umeme kutokana na *Power Project* ya Somanga Fungu. Huo Mradi wa Gesi kupata umeme bado unaathiri Wilaya za Wilaya ya Kilwa, Rufiji, Kibiti na Mkuranga. Ni aibu kusema Mradi bado unachelewa kwa miaka miwili sasa. Mradi umeanza kwa kasi, mpaka leo mwembe tunao lakini matunda hatufaidi. Gesi ya Songosongo ni mkombozi wa nchi yetu kwenye Gridi ya Taifa. Gridi ya Taifa imepokea megawati 300 kutokana na gesi ya Songosongo, lakini thamani kwa watu wa Kilwa hakuna. Ni jambo

la aibu, tunamwomba Waziri, atujibu ni lini tutapata umeme huo? Mheshimiwa Waziri, wakati unahitimisha naomba kauli yako lini tutauona mwanga, hatutaki kusikia hadithi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, huu Mradi ulikuwa unataka kusaidia vijiji ambavyo nguzo za umeme zimepita. Zilipopita nguzo kulikuwa na suala la fidia kwa wananchi walioathirika kwa kung'olewa mazao yao kama mikorosho na minazi. Namshukuru Waziri kwa kazi nzuri, hao wananchi wote wameshalipwa kuanzia Kilwa, Rufiji, Kibiti mpaka Mkuranga. Nasema Waziri ahsante sana; shilingi milioni 400 tumeziona, sasa ugomvi wetu kuwaka taa. Mwanga tunautaka na tukiupata samaki wetu wataokoka, tutaepukana na jenereta bovu ambalo lipo Kilwa Masoko, linalofanya umeme uwake kwa mgao wa *panadol*. Jenereta bovu tangu wakati wa ukoloni lipo pale, linaharibu bidhaa za wananchi. Wavuvi wanajitahidi kuvua, wakiweka samaki wao, ikifika saa tatu mgao unaanza, kwa hiyo, tunataka tutokane na mgao wa *panadol* kutwa mara tatu, hatuutaki tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona tutaokoka safari hii Waziri atanijibu hilo, lakini nina tatizo lingine la bei ya kuunganisha mita mpaka mteja kupata umeme. Bei ya kuunganisha umeme majumbani imekuwa kubwa mno, leo mteja shilingi analipa laki sita; mwanakijji anaipata wapi fedha hiyo? Itakuwa hadithi, mwanga upo lakini majumbani haupo, upo kwenye nguzo tu na waya. Kuna vijiji nikivitaja hapa, hata nyumba moja haina umeme ukianza Kisangi, Mtanga, Mpara, Singino, Nangulukuru, Miteja, hakuna umeme kabisa watu wanashindwa kuunganisha. Nguzo zitapita lakini watu watashindwa kuunganisha. Namwomba Waziri kwa kuwa sisi ni wakombozi, watu wa Kilwa kutokana na gesi ya Songosongo, kuwe na punguzo maalum kwa Wananchi wa Kilwa, Rufiji mpaka Mkuranga; ndio tunaanza kuifaidi hiyo gesi.

Mheshimiwa Waziri, nakuomba sana hilo, wananchi wangu wanakusikia, tupate punguzo maalum la kuunganisha umeme huo jamani ili tuweze kuunganisha uingie majumbani usibakie kwenye nyaya tu. Mheshimiwa Waziri, kwa jicho la huruma nataka unijibu ili wananchi wangu wasikie punguzo hilo lipo kwa Songosongo, kwa Wilaya yetu ya Kilwa na Rufiji, pamoja na Mkuranga jamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee kuhusu Songas, jamani ule Mkataba urudiwe tena ni bomu, Serikali inapata hasara na *TANESCO* inapata hasara kubwa. *Capacity charges* ni milioni 270 kwa siku, unatuumiza ule Mradi jamani, naiomba Serikali iuangalie upya ule Mkataba. Tukiangalia Songas hautusaidii sana kimaendeleo. Kuna Kamati ilikwenda pale, kisiwa kile hakioti kitu, ule ni mwamba lakini hakuna ajira hata ile ajira ya korokoroni (walinzi wale wa mageti) inatoka Moshi, Arusha na Mbeya. Kufyekafyeka pale kwenye *yard* nayo wanatoka nje ya Kilwa. Jamani hatulimi Songosongo, tuna mwamba pale na hata samaki wamekuwa wajanja hawapatikani hivi sasa. Kipato cha kisiwa kile ni kidogo mno na hasa wananchi wa pale, wakiona kuna Mradi mkubwa wa Serikali, lakini wao hali zao taabani, inauma sana hasa ninapokwenda kuomba kura pale. Serikali iuangalie vizuri kwenye Mikataba ya Songas ili nchi ifaidike na Wananchi wa Kilwa wafaidike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee machache kuhusu mfumko wa bei ya mafuta. Sote tunafahamu, Tanzania hatuna visima nya mafuta, bei inapanda kila siku lakini kuna neno nimelipata nimeona niliweke ili *Hansard* irekodi na Mheshimiwa Waziri alipate aweze kulifanyia kazi. Kutokana na gesi tunaweza kupata mafuta. *Gas to liquid projects, the project will be converting in 300 million cubic feet of natural gas per day to DTL diesel.* Huu ni Mradi unaogharimu karibu bilioni 500,000,000, dola nusu bilioni. Utatukomboa kutumia fedha zetu za kigeni, utaifanya gesi iwe *liquid* itakayotengenezwa mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizitaje hizo nchi; *Natal Petroleum* wameshaanza mwaka jana; *South Africa* wameshaanza; Nigeria wapo ubia pamoja na Wamarekani; *Evron Nigerian Petroleum* wanafanya Mradi huu *gas to liquid projects*. Utatusaidia hivi sasa gesi haipo Kilwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna gesi Mtwara - Mnazibay, Mkuranga kwa rafiki yangu pale Mheshimiwa Adam Malima, ananinyooshea mkono pale. Naomba makabrasha haya nikukabidhi ili wataalamu wafuatilie jambo hili la gesi kuwa *liquid* ambayo ni mafuta. Utatukomboa sana hususan katika kutumia fedha zetu na mfumko wa bei. Leo Dar es Salaam dizeli inauzwa shilingi 2,040. Itazidi kupanda, uchumi wetu sasa hivi umekuwa wa kujikimu kutokana na mafuta. Hata hiyo hela ya kujikimu hakuna, tusiongelee maendeleo tuongelee kujikimu. Hatuwezi kuchukua mzigo mzito sana ili mradi tubuni jambo lingine tuweze kukomboka kwenye uchumi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naongelea kuhusu *gypsum* ambayo inapatikana Kilwa kwa wingi na ina ubora mzuri tu. Cha kushangaza, viwanda havitumii *gypsum* yetu ya ndani, walituahidi watanunua *gypsum* za Kilwa na sehemu nyingine wameanza ku-*import*. Hii ni hatari, tunaanza kuzitumia fedha zetu za kigeni na ubora wa *gypsum* ya Kilwa nimepata *datas* kutoka *STAMICO* ninazo. Ina *contents* ya *protein* zaidi ya asilimia 90, lakini naona hawataki kuitumia tena sijui kuna nini? Wanapata mshiko huko nje, hawataki kununua mazao yetu! Nataka Waziri wakati anajumuisha aniambie kwa nini *gypsum* ya Kilwa ina ubora lakini hainunuliwi na viwanda vyetu nya saruji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Deweji, kabla hajafuata mchangiaji mwingine, nimkumbushe kaka yangu Mheshimiwa Ephraim Madeje, alisita kidogo kuunga mkono hoja kwamba, katika Bajeti hii Vijiji nya Mpunguzi, Mbabala (a) na (b), Hombolo Makulu vyote viro kwenye *MCC*. Kwa hiyo, mtu ye yeyote atashtuka kwa upande wake. Sasa nimwite Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro.

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Nishati na Madini. Nawapongeza sana Waziri, Mheshimiwa Ngeleja, Naibu wake, Mheshimiwa Malima na Watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini, kwa kazi nzuri ya kuandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Kamati ya Mheshimiwa Jaji Boman, kwa kazi yake nzuri ambayo tumeipata hapa leo. Mimi naamini hawa walifanya kazi ya kizalendo kweli kweli na ya kitaifa. Naipongeza Serikali, kwa kuamua walichokifanya kiletwe hapa Bungeni ili Wabunge wote wajadili na uwe ni mjadala wa Kitaifa. Kwa hilo naipongeza Serikali na naamini yote yaliyoandikwa sasa, Serikali itayatekeleza kwa wakati unaofaa bila kuchelewa, kwa kuwa Watanzania wengi wanangojea mabadiliko ya Sera ya Nishati na Madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye nishati; naamini *percent* 80 ya Watanzania wanatumia nishati ya mkaa na kuni, kwa mahitaji ya kupikia kila siku. Sijaona Wizara inatoa Sera ya Kusimamia Nishati hii ambayo inatumiwa na Watanzania wengi; *percent* 80. Pamoja na kwamba suala hili ni mtambuka, linaingia pia kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini ni vyema ikawekwa Sera ili Nishati hii kama itatumika na itaendelea kutumika, iwe na bei nafuu na pia isiharibu mazingira. Kwa sababu tupende tusipende, Watanzania wengi (asilimia 80), wanatumia kuni na mkaa, kidogo mafuta ya taa na kidogo sana umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye Jimbo langu, maeneo mengi ya Jimbo la Vunjo yaliyo na umeme, umeme huo umekuwa ni kidogo sana ambaao hauwashii hata *bulb*. Hakuna sababu ya kuwa na umeme ambaao hauwezi kuutumia. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Nishati na Madini, itupie macho suala hilo. Transfoma ziongezwe maeneo yale ambayo tayari yana umeme kwenye Jimbo langu ili umeme ule utumike kikamilifu na watu walipe. Pesa ikipatikana iendeleze umeme maeneo mengine. Kwa hiyo, naomba pale ambapo palishapatikana lazima papatikane kitu ambacho ni bora. Namwomba Mheshimiwa Waziri, asimamie hilo transfoma ziongezwe kwenye Jimbo la Vunjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna maeneo ambayo hayana umeme kabisa kwenye Jimbo la Vunjo. Kuna vijiji vya Kata ya Kahe Mashariki, ambapo walishachimba mashimo wakaambiwa umeme unakuja chimbeni mashimo nguzo zitaletwa. Wamechimba mashimo sasa ni mwaka wa pili, umeme haujafika. Namwomba Mheshimiwa Waziri, Vijiji hivyo ni Kilottoni, Kiterini, Kiomu, Soko na Wona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri aangalie pia gharama ya kuvuta umeme. Sasa hivi *single phase* ni shilingi 600,000 kuvuta tu. Katika hali ya sasa, gharama zilivyo juu, bei ya vyakula ilivyo juu na mfumko wa bei ulivyo juu, shilingi laki sita si Watanzania wengi wanaoweza kuvuta umeme kwenye nyumba zao. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri aangalie, ashirikiane na *TANESCO* kuona jinsi ya kupunguza hizi gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye madini. Suala la madini, lazima iundiwe Sera mpya ambayo itawawezesha wananchi waliotoka maeneo ya madini, waweze kufaidika na madini yale. Pili, Halmashauri zenyne maeneo hayo ziweze kufaidika na madini hayo na Serikali Kuu vilevile iweze kufaidika, kwa sababu sote ni Watanzania. Serikali Kuu inasimamia Watanzania wote, Halmashauri inasimamia Watanzania waliopo kwenye Halmashauri zao na Serikali za Vijiji zinasimamia vijiji

vilivyoko kwenye maeneo yao. Kwa hiyo, haiwezekani aje mtu kutoka Canada, anakuta kwenye kijiji madini yapo, Serikali inasema wanavijiji ondokeni tunachimba madini.

Mtakachopata, mtajengewa nyumba tu mbali na pale. Baadae wale wachimbaji wakubwa, wanajenga ukuta hakuna kuingia kule ni mali yao, ninyi Watanzania ambao mliishi na yale madini, hampati kitu mnabaki kulia kila leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naiomba Serikali ijaribu kurejea hizi Sera za Madini ili kila mtu aweze kufaidika. Yale maisha bora kwa kila Mtanzania yatapatikana kama tutagawana hizi rasilimali vizuri. Madini yanayozalishwa Tanzania ni pamoja na dhahabu, almasi, tanzanite, vito kama *ruby*, *green garnet* na vingine vingi. Tanzania haifaidiki kabisa na madini hayo. Ukiangalia kama dhahabu, Tanzania ni nchi ya tatu Kusini mwa Afrika kwa kuzalisha dhahabu na ni nchi ya 12 Duniani, lakini haijawahi kuleta faida. Tanzania ni nchi ya 15 kwa kuzalisha almasi Duniani lakini vilevile almasi yetu kwa miaka yote, hakuna faida ambayo tumepata. Tutakachokuja kubaki nacho ni mashimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wanapokuja tunawasamehe kodi *whole sale*, lakini hawa si maskini. Wakati wa Mkutano wa *Sullivan*; Andrew Young alisema ye ye ndiyo aliyefanya bidii Barrick wakaja Tanzania, lakini hahusiki na Mikataba. Mikataba ni yenu, mmefanya mikataba mibovu, kwa hiyo, irejeeni hiyo Mikataba. Waziri Mkuu wa Canada alipokuja Tanzania alisema, rejeeni hiyo Mikataba. Mimi naamini, kwa kutumia taarifa hii ya Jaji Bomani; Mikataba hii tutairejea ili Watanzania tuweze kufaidi. Nitoe tu mfano wa hasara tunazopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Geita Gold Mine* inatumia lita milioni 58 za mafuta kwa mwaka, lakini wamesamehewa kodi za ushuru wa forodha na wamesamehewa *fuel levy*. Watanzania tunawakata *fuel levy* ili tukajenge barabara kwenye Halmashauri, hao matajri tunawasamehe wanalipa dola 200,000 *flat rate* kwa mwaka! Tena na wao wanashangaa, hivi ninyi mbona hamtudai kitu! Tunabaki tunalialia hapa. Tunapolia hapa wale wapo Canada hawasikii, hawasomi haya magazeti hapa. Mimi nawashauri sasa wanaharakati na sisi tunaopenda maendeleo ya Tanzania, twende tukapige kelele kwenye *Stock Exchange* ya London, NASDAQ New York, tuwaseme kule ili wawaulize kwamba ninyi wenzetu kumbe ndiyo mnakwenda kuiba kule Tanzania mnajifanya matajiri hapa? Kwa namna hiyo watasikia, lakini tukisema huku wapi, wapo Canada wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka, naomba nizungumzie suala la Kiwira. Ilisemekana hapa Bungeni kwamba, taarifa itakuja na nategemea itakuja. Naomba nilizungumzie kidogo, naishukuru Wizara ya Nishati na Madini, kwa kuwapiga chini Dowans, pia wanaendelea na *IPTL* na watakaofuata nadhani ni Songas. Sasa lazima tuangalie hili suala la *capacity charge*, kwa kipindi hiki hatuhitaji umeme wa dharura, inakuwaje *IPTL capacity charge* dola milioni 2.85 kwa mwezi, *Songas* milioni 6.09, Kiwira dola 3.65 milioni kwa mwezi, bahati nzuri Dowans tumeipiga chini. Sasa haya ndiyo mambo ambayo tunatakiwa tuyaangalie na kuyarekebisha. Kwa sababu tumeshakubali kwamba, kama kuna kitu ambacho kimekosewa na kinasemwa, inabidi

tubadilike na tumalize tuendelee na shughuli nyingine za kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya kuleta maendeleo ya Watanzania. Hakuna sababu ya kuendelea kurudia kitu hicho hicho, mara tunakwepa kama kipo kisemwe kishe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye *Tanzanite*. *Tanzanite* inapatikana Tanzania tu, lakini ukienda India Jaipur wanaajiri watu 280,000 kuchambua *Tanzanite*. Inakuwaje *Tanzanite* inaenda kuchambuliwa India, hii ni njia mojawapo ya kukwepa ushuru? La pili, Kamati ya Jaji Bomani imependeleza madini yote ya vito yachimbwe na Watanzania. Kwa hiyo, naunga mkono naomba *Tanzanite* ambayo inapatikana Tanzania tu ichimbwe na Watanzania pekee. Hata wale wawekezaji walioko kule, wana uhusiano mbaya sana na wachimbaji wadogo. Kwanza, kila wakiingia kwenye mgodi wanapotoka wanapigwa *X-Ray* mwili mzima kila siku. Sidhani kama hiyo ni nzuri kwa afya. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri twende tukaangalie wale vijana wetu wanafanya kazi kwenye mazingira mabaya kabisa. Ni kweli wanapigwa *X-Ray* mwili mzima kwa kila siku wanapotoka migodini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala hilo, naomba Serikali iliangularie ili vijana wetu waweze kufanya kazi vizuri, wapate afya na waweze kuiendeleza Tanzania vizuri. Kabla sijamalizia, naomba tuangularie faida inayopatikana na madini. Kwenye taarifa ya Waziri imesema, kwa mwaka 2006 madini yalichangia 2.6 percent kwenye Uchumi wa Taifa na 2007 madini yalichangia asilimia 2.7. Huko nyuma hakusema, lakini kuanzia 1990 wakati wachimbaji wadogo wakiwepo, madini yalikuwa yanachangia asilimia 3.5 kwenye Pato ya Taifa. Sasa baada ya wachimbaji wakubwa kuja, hiyo imeshuka maana yake kuna hila hapo. Haya makampuni makubwa, yanatumia pesa nyingi kuliko wanavyozalisha. Sasa kama hatupati tunaachiwa mashimo; kuna sababu gani ya kuendelea kuchimba? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali hawa wachimbaji wakubwa wasimamishwe, tufukie hayo mashimo mpaka tutakapokuwa na uwezo wa kuchimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, nikushukuru sana na kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ili nisisahau. Naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa William Ngeleja na Naibu wake, Mheshimiwa Adam Malima, pamoja na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri. Mmeonyesha kwamba sasa Watanzania mnawenza. Naomba nichukue nafasi hii, kuwapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusitisha Mkataba wa Dowans, Watanzania wengi wamefurahi sana tena sana. Waziri Mkuu na Waziri wetu, mmeonyesha moyo kwa kuwasikiliza Watanzania jinsi walivyokuwa wanalamika katika kuhakikisha kwamba,

mikataba mibovu ambayo ilikuwa inawakwaza sasa inaonyesha njia; tarehe 1 Agosti, 2008 Mkataba huu umesitishwa. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Nishati na Madini, ndiyo Wizara pekee ambayo mimi naiona ya kukuza uchumi katika nchi hii. Wizara hii ina Shirika la Mafuta, *STAMICO*, *TANESCO*, Chuo cha Madini, Wakala wa Jiolojia; ambavyo ni utaalam kamili kabisa wa Watanzania kuhakikisha kwamba, wanalinda mali zao wenyewe. Cha kusikitisha, mashirika haya niliyoyataja ambayo yapo chini ya Wizara ya Nishati na Madini, yaliachwaachwa tu. Sasa inatufariji sana Watanzania, kama Kamati yetu ilivyozungumza, tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri, *TPDC* sasa ihakikishe inawezeshwa kikamilifu, maana yake ni wataalam pekee.

Inafurahisha ukiangalia Kitabu cha Waziri; nilipokuwa Kamati ya Fedha na Uchumi, sikujua kama Tanzania tuna madini ya aina hii, pamoja na mafuta. Ramani iliyoko nyuma ya kitabu hiki, inaonyesha kabisa maeneo mengi ambayo yatapatikana mafuta, gesi pamoja na madini. Kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali yetu ya Awamu ya Nne izingatie sasa kuiangalia Wizara hii. Pamoja tumeamua kuweka vipaumbele katika Miundombinu, lakini lazima sasa tuangalie na Miundombinu katika Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Mheshimiwa Mongella, asubuhi ulipokuwa unatambulisha watendaji wa asasi ambazo zipo chini ya Wizara hii walikuwa wanaume watupu. Kuna Dr. Joyce Singano pale *TPDC* ni akina Joyce Singano wangapi ambaao ni *Doctors* lakini tunawaacha acha kwa sababu ni wanawake, tunashindwa hata kuwaleta na kuwatambulisha ndani ya Bunge hili, kwa kweli inasikitisha! Nawaomba sasa kwa Wizara nyingine zinazokuja, tuhakikishe wanawake walio na ngazi sawa sawa na wanaume kwenye Wizara hizo na wao waletwe ndani ya Bunge hili tuwaone. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi humu Bungeni tumearifiwa kwamba, watu wa *TPDC* wanatakuwa na maonyesho yao. Naomba sana Waziri wa Fedha na Uchumi, apitie kwenye banda lile akaone vizuri. Ni uchumi ambaao wa uhakika, ambaao unawenza ukapatikana hapa nchini. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala la *STAMICO*. *STAMICO* kama nilivyoanza kuzungumza pale mwanzoni, iliachwa tu, lakini ni shirika ambalo litasimamia wachimbaji wadogo wadogo, ambaao kila siku wamekuwa na mgogoro kati ya wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo. *STAMICO* tukaamua kuiacha ambapo ingetusaidia sana wachimbaji wadogo wakapata elimu ya kutosha, wakaelekezwa jinsi ya uchimbaji wa madini huko waliko na migogoro kama hii tusingewenza kuipata tena.

Nitashukuru sana kama alivyotuambia Mheshimiwa Waziri, *STAMICO* imetolewa kwenye mashirika ambayo yalikuwa yabinafsishwe. Niombe sasa *STAMICO* itumike katika kuhakikisha Wachimbaji Wadogo wa Mugusu, Nyarugusu Geita na

Wangasamo Magu na maeneo mengi yenyenye madini nchini, sasa waelimishwe na *STAMICO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende *TANESCO*. Tunapozungumzia kupunguza umaskini ni katika kuwawezesha wananchi kuwapa bei nafuu ya kuhakikisha kwamba, wanajiimarisha katika maeneo yao; kama ni wajasiliamali wanavuta umeme ili waweze kuzalisha. Kabla ya kusomwa Bajeti ya Wizara hii, kuna Mjasiliamali mmoja amekuja kwangu akasema kama mnataka sisi wajasiliamali tujiendeshe, tuvute umeme, tuuze *ice cream* na barafu kwa nini gharama ya uvutaji wa umeme ni ghali? Amekuja na risiti zake ambazo ni halali kutoka *TANESCO*, naomba nizisome.

Nguzo tu peke yake ni Sh. 729,582.72; anapolipia hiyo nguzo anapigwa VAT ya shilingi 182,395.68. *Service line* anaambiwa alipe Sh. 383,682 na hiyo *service line* inapigwa VAT shilingi 77,136. Huyu mjasiriamali mdogo amelipa na risiti anazo jumla ni shilingi 1,377,796.80. Mjasiriamali wa kiasi hiki; hata hiyo biashara ataianzisha? Naomba *TANESCO* mkae chini, pamoja na gharama ambazo mlikuwa kweli mnabebeshwa kutoka huko nyuma, lakini lazima hili tuliangalie. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, amezungumza kwamba *EWURA* wanatafakari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wakati wanaendelea kutafakari, hebu tujaribu kuangalia basi angalau mpange hata hizo gharama huyo mjasiliamali alipe awamu kwa awamu labda itamsaidia. Unapomwambia Sh. 1,377,000, wakati hajaanza biashara yake, hajaenda *TRA* na hajakata leseni; hivi kweli tutawafikisha Watanzania katika hali hii ya kuondokana na umaskini? Naomba hili la *EWURA*, mkae pamoja na *TANESCO* muwasaidie wajasiriamali wadogo ambao wanataka wajiedeleze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba basi nishauri upande wa *TPDC* kwamba, hawa wachimbaji wakubwa wanapokuja hapa nchini kutafuta mafuta na gesi, ningombwa sana tuwatumie wataalam ambao wapo *TPDC* waongozane na hao watafiti. Maana inafikia hao watafiti wanaomba muda mrefu wa kutafuta mafuta au kutafuta madini, huo muda wanatumia katika kuchimba madini na kuuza na kuondoka zao, baadae wanasema hawakupata chochote. Kama tutawatumia *TPDC* upande wa mafuta na gesi, tutahakikisha kwamba, mafuta yetu yatapatikana vizuri. Pamoja na hawa wa upande wa madini, *STAMICO*, ikitumika vizuri kwa kuwawezesha ili waweze kusimamia madini yetu vizuri, maana hawa ndiyo wataalam ambao wanahakikisha kwamba, miamba fulani ipo mahali fulani ndiyo ina madini. Ni Watanzania ambao watakuwa na moyo kuhakikisha kwamba, udanganyifu sasa ambao tulikuwa tunapewa wa kuambiwa kwamba, hapa madini hayajapatikana kumbe yapo, lakini kama Mtanzania yupo pale ataweza kusimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amediriki kutuambia kwamba, hata nguzo zinaagizwa Afrika Kusini. Nafikiri hata na hii nayo inaongeza bei ya nguzo hizi. Tunajua Iringa kuna miti, Mbeya kuna miti mingi na hapa Tanzania tunahamasishana sana kupanda miti, hivi sisi tunashindwa kuweka hata mashamba maalumu ya kuhakikisha kwamba, tunapanda miti na kupata

nguzo ili tuweze kuwasaidia Watanzania. Naomba sasa suala la kuagiza nguzo tuliangalie upya, tujaribu kutumia miti tuliyonayo na tulikuwa tunaona malori mengi kutoka Iringa na Nyanda za Juu Kusini; hivi ndiyo yamekwisha mpaka tuagize Afrika Kusini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru sana, Mheshimiwa Waziri amekuja na Mkakati mzuri sana wa kuanzisha ule Mfuko ambao unawawezesha wachimbaji wadogo wadogo. Mfuko huu uwalenge wachimbaji wadogo wadogo, isije sasa ikafikia mahali Mfuko umetoka kama Mfuko wa JK, watu wakubwa wakubwa wamepeana, wahusika hawakupata. Sasa naomba wachimbaji wadogo wadogo, Mfuko huu uwalenge na naomba sana ututumie Wabunge, maana sisi ndiyo tunaowafahamu huko waliko. Mambo ya kuja tena kutuambia hapa kwamba, fedha zilikuja kidogo na wamepewa watu wachache, kwa kweli Mheshimiwa Ngeleja tutatofautiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kama nilivyochangia kwenye Bajeti ya Serikali; wakati wanapokuja wawekezaji nchini, kwa nini basi wasikae na wananchi wanaozunguka maeneo kama ya migodi ya dhahabu na gesi, kujadili ni kitu gani cha kipaumbele cha kuweka maendeleo katika eneo lile? Nitaomba sana mtakapoanza kubadilisha mikataba ile ambayo tulikuwa tumejikwaa kidogo, tujaribu kuwashirikisha wananchi wa maeneo yale ili na wao waweze kufaidika na mali walizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasikitika sana Chuo kama cha Madini Dodoma tunakiachia na ni kimoja tu Tanzania nzima, ambacho kinatoa wataalam wa uchimbaji wa madini. Nitaomba Bajeti ijayo, Waziri ahakikishe anakuja na Bajeti kubwa ambayo itayawezesha mashirika na taasisi ambazo zipo chini yake, ambapo kila taasisi ina kipaumbele chake cha kuhakikisha kwamba, wanawezeshwa kwa wanapewa miundombinu mizuri ili tuweze kupata wataalam. Lingine ambalo ninaliomba katika *TPDC*, watalaam ambao tunawategemea ni wachache sana katika utafutaji wa gesi pamoa na mafuta. Naomba sana tutenge fedha kuhakikisha kwamba, hawa waliopo wachache akina Dr. Joyce wavezeshwe ili wapatikane akina Joyce wengine, ambao wataweza kuhakikisha kwamba, mafuta na gesi tuliyonayo wanaweza kuisimamia vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nifahamu vijiji ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, atavipa umeme; je, vitapata lini umeme huo? Amevorodhesha ukurasa wa 77 ni vingi, lakini nina uhakika kwa sababu ninajua mipango imewekwa vizuri, tutahakikisha kwamba, wamepeleka umeme. Mheshimiwa Waziri atuhakikishie ni lini watapelekewa umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa; ni lini Serikali itaona wachimbaji wadogo wadogo wa madini kwamba na wao wanahuksika katika nchi hii na wakatengewa maeneo yao ya kudumu? Isifike wakati wakaja wawekezaji kutoka mbali, wakaanza kuambiwa tokeni. Ninaomba Mheshimiwa Waziri uje na mikakati ya kuhakisha kwamba, wachimbaji wadogo wa Nyarugusu, Kasamo na wa maeneo mengine, wanapewa maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.
(Makofi)

MWENYEKITU: Nakushukuru sana Mheshimiwa Esther Nyawazwa. Waheshimiwa Wabunge, mpaka sasa hivi uchangiaji wa jioni ya leo, wamechangia Wabunge wanaume saba na Wabunge akina mama wawili tu. Kwa kuwa Mheshimiwa Mongella na Mheshimiwa Nyawazwa wamesema kipekee kuhusu haja ya kuhakikisha uwiano unakuwepo, basi sasa narekebisha kidogo ratiba yangu hapa. Naomba nimwite Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Umbulla. Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, kama ulikuwa hujajiandaa, shauri yako.

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa utaratibu, kama mwanasiasa huna haja ya kujiandaa. Kwa hiyo, sina wasi wasi.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupewa nafasi ya kuchangia hoja ilio mbele yetu. Kwa kushangaza kabisa, naomba niseme bila kuficha, siungi mkono hoja hii mpaka nihakikishe nimeambiwa umeme wa Bukene na wa Ndala ukoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Bajeti ya 2006/2007, wakati Waziri akiwa Mheshimiwa Dr. Msabaha, alipitisha hapa bajeti na tukapata shilingi milioni 900 kwa ajili ya umeme wa Bukene na Ndala. Tulipitisha, lakini cha kushangaza, pesa zile hatukuweza kuzipata kwa ajili ya manufaa ya taifa. Sisi tuliondoka na Mheshimiwa Selelii, tukaenda kuwaambia wananchi wapiga kura Ahadi ya Rais Mkapa, ambayo alichukua kijiti Rais Kikwete kwamba, tumeacha kupata safari hii, lakini mwaka unaofuata umeme unafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007/2008, bajeti yake ambayo tumeimaliza juzi, tukapitisha, tukapewa shilingi milioni 50, wakati Waziri aliyepo sasa hivi, Mheshimiwa Ngeleja akiwa Naibu Waziri. Sisi tukasema milioni 50 tunafanyaje nazo hizi kazi, mbona ni ndogo mno! Akaniambia hizo ni kuonyesha kwamba, Mradi huu upo, haukuondolewa kwenye bajeti na haujaondolewa kwenye mipango ya Serikali. Nikafuutilia mpaka kiatu kikaenda upande, kupanda pale TANESCO kufuata umeme wa vijijini na nikaambiwa pesa hizo haziwezi kufanywa kitu chochote zipo. Mpaka mwisho kabisa, kwa kifupi wakanambia hawawezi kuzifanyia kitu chochote kwa sababu ni hela ndogo sana. Nikawaambia pelekeni hizi pesa, msizirudishe kwenye Serikali, lazima zianze angalau nguzo moja au mbili kutoka Nzega kuelekea Bukene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati ya Nishati na Madini nikaenda kufuutilia, nikakuta tena nimepewa milioni 50 ya mwaka huu ambao tunauzungumza. Halafu imeandikwa kwamba, kazi imeanza. Naomba kusema wazi kabisa, nilikuwa Bukene juzi na nimeondoka jana, hakuna kazi yoyote iliyofanyika kwa shilingi milioni 50. Ninayo makabrasha hapa kutoka kwenye Kamati yanayosema kazi imefanyika, huo ni uongo na ni wizi! Hakuna kazi iliyofanyika, hakuna mtu, hakuna waya, wala hakuna kitu chochote cha kuonyesha kuwa kazi imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndio maana nasema, ndugu yangu Ngeleja sawa, nimekufta sana umeniahidi utanipa umeme, lakini kwenye hotuba yako ya leo hakuna Bukene, kwenye hotuba ya Mwenyekiti, Bukene ipo; Sasa njue lipi? Umeme wa Bukene upo au haupo? Pesa zipo, hazipo zile za mwaka jana maana kazi haijafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mambo ya kusikitisha na kuanza kuelezana kwamba, tupelekane Bukene, tubebane sijui tufanyeje. Nimechoka kusema hadithi hiyo, lazima tujue umuhimu, sisi sote ni Viongozi, tumechaguliwa na tunajua ahadi maana yake nini, hasa ahadi ikitolewa na Viongozi wetu Wakuu. Ndugu zangu, mimi nafikiri nimeeleweka, naomba kuelezwu hilo na sitaunga mkono, tutakutana kule, nafikiri tunaelewana, mpaka kieleweke, hiyo shilingi milioni 50 lazima ionyeshe inaanza kazi, siyo tunaambiwa kila siku 50, hamna kitu, 50 hamna kitu. Sisi tunaweza kufanya kazi na maendeleo yanaeleweka. Tumefufua Igembe Sabo; Igembe Sabo inanunua mchele. Tumenunua mashine ya kukobia mchele. Hatuwezi kuweka mashine yetu Bukene kwa sababu hakuna umeme. Tumepeleka Ziba, tunawanyima Wananchi wa Bukene ajira na biashara kwa sababu ya umeme. *Priorities* za umeme zinakwendaje? Bukene ni *centre* kubwa kuliko sehemu nyingine ambazo sitaki kusema, zinazopangiwa kupewa umeme. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Sema! Sema!

MWENYEKITI: Ongea na Mwenyekiti, Mheshimiwa.

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU: Mimi naongea na Mwenyekiti. Mwenyekiti, nafikiri umenielewa, hata Waziri na Naibu Waziri wamenielewa. Lazima tuangalie kama tunapopeleka umeme unaleta manufaa. Kwa mfano, ukipelekwa Bukene unaweza kutuletea manufaa kama hivyo ninavyosema; tuna mashine sisi ya kukobia mchele, tumeipeleka Ziba. Tumewapa watu wa Ziba ajira badala ya kuwapa vijana wetu wa Bukene. Sasa hiki ni kitu gani?

Siyo kwamba sisi hatuwezi kulipa umeme au kuendesha gharama za umeme; tunaweza ila basi tu, sijui ni kitu gani. Tuna kitu gani? Tunaonewa au tuna balaa la kuzaliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri nimeeleweka. Uchungu huo unakwenda maana Mradi wa Bukene ndio Mradi wa Ndala. Unapotunyima umeme Bukene, maana yake unachelewesa umeme wa Ndala, maana ndio unaoendelea. Ndala kuna hospitali kubwa sana; ni *historical*, kuna vyuo na vitu vingine ambavyo vyote vinahitaji umeme, *secondary school* ndio usiulize kila kona, tutafanyaje bila umeme? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ndugu yangu Ngeleja kaelewa na mtani wangu kaipatapata na watanifikiria kunirudishia hela zangu na kuniongeza siyo kunirudishia tu hizo chache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye suala la madini. Madini ni kitu ambacho kinatakiwa kutusaidia tutokane na umaskini na kuna nchi nyingi sana zinazoishi kwa Madini tu. Madini siyo kama mahindi. Mahindi unalima unavuna, unalima tena, hakuna hasara, lakini Madini ukichimba ukayaondoa yameshaondoka yale, unabaki na shimo. Nafurahi kwamba, walionitangulia wamezungumza hivyo hivyo. Sasa, sisi tunaotoka kwenye Madini, tunahitaji kufananafanana angalau kimadini madini. Matatizo na migogoro inayotoka kwenye migodi mingine, inatakiwa kuzuiwa, hizo ndizo kero na mara nyingi tunazungumza, *we learn through mistakes*. vYale ni makosa yaliyotangulia, hatutakiwi kuyarudia tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sisi tunaanza sasa kufufua kuonekana tuna Madini kama kwenye Jimbo langu; Mwanzwilo, Mahene na Itanana kuna Almasi, basi tusiingizwe tena kwenye matatizo ambayo siyo ya lazima. Watu wanaondolewa bila kulipwa chochote, wanakuwa kama wanafukuzwa. Wanapewa pesa barabarani, shilingi 60 chukua hizi, kama hutaki basi, ardhi ni mali ya umma. Hivi ni kweli ndivyo tunavyofanya. Mtu na bustani yake anapata chakula, anapata ada ya watoto wake kutoka kwenye bustani hiyo, halafu unampa barabarani shilingi 60, akikataa, unampa baba yake au mke wake, nenda umpelekee. Kweli ndiyo hivyo, hela ya baba yake na ya mtoto wake! Ndiyo tunavyofanya hivyo katika utaratibu wa fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri nilikuwepo katika kupitisha Sheria ya Madini. Sheria ya Madini inasema lazima tukubaliane pamoja na kwamba ardhi ni mali ya umma, lakini tukubaliane ardhi ina thamani, pale umenikuta mimi nina shamba, lazima *uli-value* shamba langu. Nalima bustani nauza.

Nina bwawa la kumwagilia, nina nyumba, *ui-value* ile nyumba, ujue unachukua sehemu hii kwa miezi 18 maana unanizua mimi kufanya kazi ya kuzalisha. Kwa hiyo, unipe pesa ya kutosha kunisaidia na mimi nifanye kazi zangu, nisomeshe watoto wangu, nilishe familia yangu, nisiaibike na vile vile niondokane na umaskini, niwe na maisha bora, ndiyo tunazungumza hivyo. Unaponitoa au kunifukuza kienyeji, maana yake nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuisiangalie sana wanaokuja kutoka nje, tuangalie wananchi wenyewe, Kinyamwezi wanasema “wenye matongo yao, wenyе mashamba yao, wenyе nyumba zao”, tuzungumze nao, tukubaliane nao, watupe fidia. Tukubaliane mikataba inayoleweka kwamba, unafanya mikataba miezi 12 basi miezi 12, mwaka wa kwanza utalipa shilingi hizi, mwaka wa pili utalipa shilingi hizi. Hata kama unafanya utafiti ukimaliza, tutazungumza hadithi nyingine. Kurashiarashia, unatishwa eti ondoka, utafanya nini ardhi ya umma. Tunatishana katika nchi hii? Ndio uhuru wenyewe huu au ndio demokrasia yenyewe hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba twende kwa utaratibu, tuheshimiane na kila mkubwa amheshimu mdogo na mdogo anamheshimu mkubwa na Sheria zifuatwe. Haki mtu apewe! Narudia tena, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, nakushukuru sana kwa kuunga mkono hoja. Mheshimiwa Mama Mongella, unaweza ukaona jinsi ambavyo imekuwa hatari kubwa. Hali hiyo hajajiandaa, angejiandaa ingekuwa shughuli kubwa.

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa sijaunga!

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Kasella-Bantu.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia nakushukuru sana kwa nafasi hii ya upendeleo. Tatizo ninalopata ni kwamba, unapomfuatilia msemaji ambaye amezungumza kwa umahiri sana, wewe unaweza ukaonekana hujajitayarisha. Nakushukuru sana na mimi japokuwa mchango wangu utakuwa pungufu, lakini nitajitahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na wenzangu kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Ngeleja, Naibu wake, Mheshimiwa Adam Malima na Watendaji Wakuu wa Wizara ya Nishati na Madini, kwa kazi nzuri ambayo wengi imetupa matumaini na nadhani itakuwa imekidhi matarajio ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni nzuri kwa sababu mimi nimeona imeweka bayana mikakati mbalimbali na malengo ya baadaye. Imeweza kuweka bayana matatizo na changamoto mbalimbali na mikakati ya kutatua. Kwa hiyo, nawapongeza kwa moyo wa dhati. Tunaona mahitaji yetu ya Nishati ni makubwa sana kuliko tulichonacho, lakini nadhani tutafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuomba kuchangia Wizara hii, naomba nitumie fursa hii kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Manyara na Wananchi wa Wilaya ya Mbulu, kuishukuru Serikali na Chama cha Mapinduzi, kwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kutupatia umeme Kijiji cha Dongobesh, Mbulu. Nadhani mtakumbuka kwamba, tumeuliza maswali mengi hapa, Mheshimiwa Mbunge wetu amefuatilia kwa miaka mingi sana umeme wa Dongobesh, Daudi na maeneo mengine. Tunashukuru Serikali hata kwa hicho kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni sehemu ndogo kabisa ya Makao Makuu ya Tarafa. Vijiji vingi vilivyo pembezoni viro kwenye giza, basi na kwa hicho kidogo tunatarajia kwamba, Serikali itaendelea kutusaidia ili vijiji vyetu viweze kupata umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi sana nchini mwetu, hawana umeme na tunajua kwamba hili ni tatizo kubwa la nchi nzima, kama wengi ambavyo wameweza kuainisha hapa, tatizo la umeme linarudisha nyuma maendeleo ya wananchi, linachangia sana kupunguza ubora wa maisha ya wananchi. Kukosekana kwa Nishati ya umeme kunachangia elimu duni, tukizingatia kwamba Mkoa wetu wa Manyara upo pembezoni,

vijiji vyake vina hali duni sana na hivyo Walimu wanaopangwa kwenda kwenye vijiji hivyo, wanakwepa kwenda kule kwa sababu ya kukosa umeme na hali ni mbaya kule. Kwa ajili hiyo pia, katika maeneo haya kuna umaskini uliokithiri kutokana na sababu wananchi ni vigumu sana hata kuendesha biashara ndogo ndogo, masuala ya ujasiriamali inakuwa nyuma sana kwa ajili ya kukosa Nishati ya Umeme. Tatizo hili ndio kubwa linalochangia hata kupunguza Pato la Taifa, kwa sababu Wanawake kwa ujumla wao ndio wanaochangia sana Pato la Taifa kwa uzalishaji wa kijijini.

Sasa wanakosa nafasi ya kufanya shughuli ya uzalishaji, kuacha ile shughuli nyingine ya wanawake ya kutumikia familia zao. Kazi za ndani ambazo huwa hazipimwi na wala haziwekewi thamani, lakini zile za uzalishaji ambazo wanachangia Pato la Taifa na wao wanashindwa kufanya kwa sababu hakuna Nishati ya Umeme. Wanahangaika kutafuta maji, kuni na kutafuta namna nyingine mbadala ambayo wanaweza kuendesha maisha ya familia zao. Kwa hiyo, nadhani utakapopelekwa umeme kwa wingi vijijini, tutawapa Wanawake fursa ili waweze nao kuchangia katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwaletea wananchi umeme vijijini ni jambo moja, lakini wananchi kumudu gharama za kuunganisha umeme ni jambo lingine. Kama nilivyosema, tumepata umeme katika kijiji chetu cha Dongobesh, lakini cha kusikitisha ni kwamba, wananchi walio wengi wameshindwa kabisa kumudu gharama za kuunganisha umeme katika nyumba zao. Gharama hizo ni kubwa sana, zaidi ya shilingi milioni moja kwa mtu wa kijijini ni gharama ambayo si rahisi kuimudu. Pamoja na kwamba, katika hotuba hii ukurasa wa 24 ameainisha sababu ya gharama hii kuwa juu, pengine ninukuu kidogo ili hata na wananchi wasikie; Ukurasa wa 24; gharama za ujenzi wa njia za umeme zimepanda kutokana na kupanda kwa bei ya chuma na shaba kwenye Soko la Dunia. Gharama ya ujenzi wa njia ya KV33 zimepanda kutoka shilingi milioni 18 kwa kilomita mwaka 2006 hadi shilingi milioni 35 kuanzia Januari mwaka huu. Bei za nguzo zimepanda kutoka shilingi 96,000 hadi shilingi 153,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ni sahihi na ni ya kweli, lakini pia *TANESCO* ni yetu na ni Shirika la Serikali yetu na wananchi wetu ni maskini hawawezi kumudu. Sasa tunaiomba Serikali basi iweze kuangalia namna ambavyo inaweza ikachangia, ikawasadidua wananchi wakamudu hizo gharama hasa tukizingatia umuhimu wa Nishati hii ya Umeme vijijini. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Wananchi wetu wa Mkoa wa Manyara, wana tatizo kubwa kwa sababu Mkoa wetu ni mpya; tumegawanyika kutoka Mkoa wa Arusha na upya una matatizo mengi sana. Kama Serikali imeona ni vizuri Mkoa huu ukaanzishwa kama Mkoa mpya, tunaomba upya huo uende sambamba na kutekeleza yale yaliyo muhimu ili na sisi tujikongoje tuwafikie wenzetu wa Mkoa wa Arusha na Mikoa mingine. Hivi sasa baadhi ya Makao Makuu ya Wilaya kama Simanjiro na kwingineko, hakuna umeme na hata Barabara hazififikasi.

Sisi Wabunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Manyara, tunapata tatizo kubwa sana, ukitoka Basotu kule Hanang ukaenda Mbulu ukiteremka kuja Babati ili kwenda Kiteto, inabidi uje Kondoa ndio utafute njia ya kwenda Kiteto. Mimi nadhani hili ni

tatizo ambalo hata kutimiza zile ahadi zetu tulizoahidi kuwatumikia wanawake wa Mkoa wa Manyara, itakuwa ni tatizo kuzikamilisha. Tunaomba Serikali walau iangalie Makao Makuu ya Wilaya na maeneo yale muhimu ambayo wananchi wetu wanawenza wakaanzisha hata biashara za kufanya hasa za ujasiriamali, wakapewa Nishati ya Umme mapema iwezekanavyo. Tunaomba Serikali itoe kipaumbele katika eneo hilo la Mkoa kama ambavyo nimeweza kuielezea kwa msisitizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika eneo la madini kwa kifupi sana. Kama ambavyo wenzangu wameshatamka, Mwenyezi Mungu, ametupa zawadi ya madini katika nchi yetu. Cha kusikitisha ni kwamba, Watanzania tumefaidika kidogo sana zawadi hii na kwa miaka mmingi, nadhani hatujapata hata manufaa kidogo yanayotokana na Madini. Kwa ajili hiyo, tungefikia matarajio ya kuwa na maisha bora. Sisi Watanzania tusingekuwa na tatizo nayo kwa ajili ya madini tuliyonayo. Tuna dhahabu, almasi, *Tanzanite* na mengineyo ambayo yametajwa. Nadhani sisi Watanzania tulibarikiwa lakini hatukuweza kutumia fursa hii ambayo tumepewaa bure na Mwenyezi Mungu. Tukiangalia Tanzania ni ya tatu katika Afrika kwa kuuza Madini nje na nusu ya mauzo ya nchi yetu yanatokana na madini. Sasa nashindwa kuelewa kwamba ni kwa nini kwa miaka mmingi sana Tanzania hatukuweza kunufaika na mauzo ya madini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotia moyo ni kwamba, tatizo hili limeweza kujulikana na kupigiwa kelele sana. Nadhani kuna matumaini ya masuala ambayo yanarekebishiha kutokana na tatizo la kutowajibika vizuri na kutotoa taarifa ambazo ni za uwazi. Kwa hiyo, nadhani ni wakati muafaka kulirekebisha ili Watanzania tulio wengi tuweze sasa kunufaika na Sekta hii ya Madini. Matatizo yamejulikana na kupigiwa kelele, lakini kuna tatizo ambalo nashindwa kuelewa hapo; mchangiaji mmoja alitamka kwamba, tatizo hili limechukua miaka. Bajeti iliyopita kulikuwa na matatizo ya Mikataba ya Madini, hadi leo hii tunapozungumza, bado linazungumziwa tatizo hilo hilo la matatizo ya mikataba mibovu ya Madini na kwamba, madini hayachangii katika Pato la Taifa.

Sasa ni kwa nini inachukua mwaka mzima kulitatta tatizo? Nadhani tunapoamua kwamba, tumeona tatizo basi ichukue muda mfupi sana kulitatta ili tuendelee kutatua mengine ambayo yanakuja mbele yetu, badala ya kuendelea kulizungumzia hili kila wakati kwamba. Najua ni masuala ya kisheria, lakini kama alivyosema mchangiaji mwingine kwamba, basi hayo mashimo yetu tuyafukie, turekebishe mambo yetu halafu tuje tufukue baadaye, tutakapokuwa tumerekebisha mikataba yetu na sheria zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na machache haya ya kuchangia. Ninaomba tu lizingatiwe, tuletewe umeme katika vijiji vyetu vya Mkoa wa Manyara ili tuweze kufanya kazi vizuri na Mkoa wetu uweze sasa kukimbia wakati wenzetu wanatembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nashukuru. (*Makofi*)

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nichangie hoja iliyio mbele yetu. Awali ya yote na mimi nawapongeza sana watoa mada; Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Viongozi wote kwenye Wizara hii, kwanza, kwa kuhakikisha kwamba bajeti hii imeandikwa vizuri, kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba, tutekeleze yale masuala ambayo yatatusaidia huko mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi kwangu naishukuru kwa sababu vitu vingi vilivyozungumzwa kwenye bajeti hii kwa upande wa Wilaya ya Rudewa, ambayo kwa miaka mingi imekuwa ikiachwa nyuma, sasa kunaonyesha dalili ya maendeleo ya kasi mpya kwa kupitia Wizara hii. Mategemeo yangu ni kwamba, sasa tutaanza kwenda *speed* na kutushika itakuwa kazi kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuhusiana na umeme wa jenereta ambayo tuliahidiwa kupewa na kwamba ifikapo 2006 umeme ungekuwa umewashwa Rudewa Mjini, kwa kutumia jenereta ambalo tulipewa na wahisani. Umeme ule hatukupata 2006 kama ilivyoahidiwa mpaka juzi ndio nimeambiwa ule umeme umewaka lakini lile jenereta linafanya kazi kwa shida kidogo, umeme upo.

Ninachoshukuru sana kwa Wizara hii ni kutimiza ahadi ya kuleta zile *generators* mbili ambazo nimeambiwa zipo kwenye utaratibu wa kuzipeleka Ludewa na bila shaka zikifungwa sasa kwa Mji wa Ludewa na viunga vyake, hatutakuwa na malalamiko tena na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuleta *generators* hizo, nawashukuru tena *TANESCO* kwa kutujengea Ofisi za *TANESCO* pale Ludewa Mjini, ahadi ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Msabaha alipokuwa Waziri na imetekelozwa. Kwa hiyo, napenda kuwashukuru sana kwa sababu ofisi tunayo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zote hizo, lakini kuna tatizo moja ambalo wenzangu waliotangulia wamesema pamoja na Mheshimiwa Dewji; la gharama za kuingiza umeme majumbani. Tatizo hili nililizungumza na Mheshimiwa Karamagi, niliongea pia na wewe Mheshimiwa Ngeleja na tulikubaliana kwamba, mtalifanyia kazi ili kupunguza gharama kwa wananchi maskini kama wa Ludewa, ambao hawana uwezo wa kulipa shilingi milioni moja kwa ajili ya kuingiza umeme majumbani kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mategemeo yangu ni kwamba, *EWURA* walishatangaza bei za umeme na kwamba, mmelifanyia kazi. Bila shaka, utakapokuwa unajumuisha utatutolea maelezo kwamba, mmeamuaje kuhusu kuwasaidia wananchi ambao hawana uwezo kuingiza umeme majumbani kwao wakati umeme upo, la sivyo miradi hii yote ya kupeleka umeme vijiji kama Ludewa, haina maana kwa sababu wananchi hawataitumia, inakuwa ni *white elephants*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninashukuru vilevile kwa umeme *grid*. Nimepiga kelele kidogo hapa tangu mwaka jana, nashukuru umeme ule utakapotoka Makambako

kwenda Songea, kutokea Madaba, utakwenda vilevile Ludewa. Kwa hiyo, wananchi wangu wa Vijiji vya Mavanga, Mondindi, Shaurimoyo, Rugarawa, Mlangali, Mkongobaki, Milo, Ludende, Muholo na kuelekea Mjini Ludewa, watapata umeme wa uhakika wa *grid*, amba ni wa muda mrefu kulinganisha na wa *generator* amba ni wa muda mfupi, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze vilevile wenzetu wa *REA*, Wakala wa Kupeleka Umeme Vijiji, kwa kukubali ombi langu la kuchangia umeme wa maporomoko madogo katika Kata za Lupanga na Mlangali, kwa kushirikiana na wenzetu wa *UNDP*. Nawashukuru sana ni changamoto nzuri na mchango mzuri pia kwamba, tunakuwa na umeme licha ya huo wa *grid*, tutakuwa na mwagine ambao utasaidia Kata angalau mbili, kwa wenzetu waliopo sehemu za pembezoni mwa vijiji vikubwa vikubwa karibu na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mchuchuma, mimi ninavyoja, taarifa zote zinazotakiwa kwa ajili ya uwekezaji kuhusu Mchuchuma zipo zinajulikana, *unlike zilivyo Liganga*. Liganga najua taarifa nyingi bado, lakini nimeambiwa kwenye hotuba hii kwamba, kuna utafiti maalumu utatakiwa kufanywa. Nitapenda Mheshimiwa Waziri anieleze; utafiti maalumu ni upi huo na je, kwa vile uchimbaji na uzalishaji wa umeme tulisema ifikapo 2010 Mradi ule uwe umeanza *according to the Ilani* ya CCM; sasa je, katika vipindi hivi tunavyokwenda mwakani hata mwaka kesho kutwa ni kazi zipi ambazo zinaendelea za maandalizi ya kuhakikisha kwamba ifikapo 2010 Mradi wa Mchuchuma utaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa madini, naipongeza tena Serikali kwa kukubali na kuweka mpango wa kasi mpya wa kuzalisha chuma ghafi pale Liganga, hasa kwa upande wa Wizara hii kutenga *square km.* 14.7 za Milima ya Maganga Matitu, kwa ajili ya kiwanda hicho cha kuzalisha chuma ghafi. Lengo tuanze na hiki kidogo angalau wakati tunangojea Mradi mkubwa. *After all*, kuna shida kubwa sana hapa nchini ya chuma chakavu, tunaweza kuzalisha *sponge iron* ambayo ni mbadala wa chuma chakavu na tukaondokana na matatizo yote ambayo tunayapata ya kuharibu mataluma na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza vilevile kwa juhudi zinazoendelea kuandaa utafiti wa ziada, upembaji kwenye chuma cha Liganga ili kupata taarifa za uhakika kuhusu viwango vya *titanium* na chuma chenyewe. Ninaona hela zimetengwa safari hii kwa ajili ya shughuli hiyo, lakini nina wasiwasi na kiasi cha hela zilizotengwa kwa ajili ya *NDC* kama zitatosha kwa kufanya kazi hiyo inayotarajiwa. Nitapenda kuthibitishiwa kama kweli zimetengwa hela za kutosha kwa ajili ya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yote hayo mazuri kwa Liganga na Mchuchuma wasiwasi wangu ni kwenye miundombinu, niliuliza swali hapa Bungeni nadhani kama siku mbili, tatu zilizopita, nikaambiwa kazi ya miundombinu. Barabara ni kazi ya mwekezaji atakayepewa kazi hiyo, tunawategemea waje waanze kwanza kuweka miundombinu ya mitambo na mashine kubwa za kupeleka Liganga; *it will take ages*, hatutafika 2010 tuwe tunazalisha *sponge iron*, *it is impossible*. Mategemo yangu ni

kwamba, bado Serikali itabeba mzigo wa kuchangia kwenye miundombinu ya kwenda kwenye Migodi ya Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo masuala ya ujumla, napenda nipate maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kuhusu sheria, mchakato na taratibu, zinazofuatwa na watafiti wanaotafuta madini. Tunaona wanatoka Wizarani au Mkoani moja kwa moja kwenye *site* ya uchimbaji wa madini. Hii inaleta ugomvi kati ya Halmashauri, watafutaji madini hawa na wananchi vijijini, kwa sababu hawajui hawa watu wamekuja kwa utaratibu upi. Hivi Sheria inasemaje, hawa jamaa hawawezi hata kubisha hodi kwenye Halmashauri wanaenda moja kwa moja vijijini; je, vijiji wanavijuaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda nipate maelezo, sheria inasemaje kama ina walakini iletwe tuikebishe, lakini kuna wawekezaji wadogo wadogo, watafutaji madini au wachimbaji wadogo wadogo ambao wanaunganisha vitalu vyao; sheria inasema hawa wanatakiwa kufanya *Environmental Impact Assessment (EIA)*, wengi hawafanyi hata Ludewa kule ninao hawafanyi. Sheria tumeiweka sisi kwa nini Wizara hii haifuatilii na kuhakikisha kwamba *EIA* zinafanyika? Ninapenda nipate majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye hili kuna suala zima za sampuli za kwenda kupeleka kwenye maabara. Kwangu kule kuna matatizo hata leo ananipigia simu, malori ya mawe yanabebwa, mchanga udongo wanasema wanapeleka kwenye maabara, hivi zinatakiwa tani ngapi na sheria inasemaje? Kinarhusiwa kiasi gani kwa ajili ya kufanya utafiti wa maabara, kwa nini inakuwa ni fujo hatuelezwi? Nitaomba Waziri anieleze kinatakiwa kiasi gani na kwa madini yapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho kabla sijagongewa kengele ni suala zima la Nishati Mbadala. Wabunge wenzangu, siyo kwa kujigamba lakini nchi hii iliyonisomesha nikawa mwanamazingira bingwa hapa nchini, vitu vingine ninapozungumza ninavielewa kwa sababu ya utalaamu wangu ninavijua. Tunaambiwa hapa kwamba, unatayarishwa mwongozo kusudi hawa wanaoendelea waendele, wakati huo huo unaandaa Sheria, Sera na Mkakati. Utaratibu wa kulima *jetrofa*, hivi kwa nini tusingoje mpaka Sheria na Sera ziwe tayari tunakimbilia wapi? Ninajua nimesoma *EIA* nyingi zinazolima nishati mbadala hii hapa nchini, *EIA* zile ni za ovyo kweli kweli, yaani wanatulalia vibaya sana, kuna maeneo yamechaguliwa yanafaa kwa kilimo cha chakula; wale wameshaanza wanalima jetrofa na vinginevyo, tutawaondoaje kama tumewaruhusu sasa hivi na baadaye ikaonekana kwamba, kule hakufai kulima mazao haya? Napenda nipate maelezo kutoka kwa Waziri; kwa nini tusisimamishe hizi Sera na Taratibu ili tusijilettee matatizo huko mbele kwamba ni aina ya mikataba mibovu? Tulifanya maamuzi vibaya, halafu yanakuja kutoka hayo na Mheshimiwa Profesa Mwalyosi alikuwepo kwa nini hakushauri? Mimi nashauri tusimame kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namshukuru sana Waziri wa Wizara hii kwa kukubali baada ya muda mrefu, kutujengea Ofisi ya Madini kwa ajili ya Afisa wa Madini pale Ludewa. Agizo ambalo alilitoa Mheshimiwa Dr. Msabaha, limekubaliwa na safari hii nategemea kuna hela ambazo tutajengewa pale. Wialaya ile ina madini ya kila aina;

Uranium, Diamonds, Gold kila kitu kipo, tunategemea tukishajenga ile Ofisi pale, kutakuwa na *survey* na *mapping* ya *mineral resources* katika Wilaya ile ili mambo yasiende ovyo ovyo na kukwepa makosa na matatizo yaliyojitokeza kwenye maeneo mengine hapa nchini. Tunataka Ludewa twende kwa utaratibu na tuonyeshe mfano wa *good mining practices* katika nchi hii. Kwa hiyo, tutashukuru sana kama mtatujengea ile ofisi pale na naomba hilo lianz mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kusema, kwa ujumla ninashukuru na nimefurahishwa sana na hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri; ni nzuri kwa upande wa Wananchi wa Ludewa, najua wanapiga makofi mambo yamekuwa safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, kwa kuunga mkono hoja na kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, dakika zilizobaki hazitoshi kwa mchangiaji yejote yule, lakini ninawaarifu tu kwamba, bado uchangiaji utakaoendelea kesho utakuwa wa uchangamfu mkubwa; atayeanza atakuwa ni Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Bujiku Sakila na kadhalika.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile shughuli zilizopangwa katika *Order Paper* ya leo zimekamilika zote, naomba kuchukua fursa hii kuahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 01.43 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,
Tarehe 09 Julai, 2008 Saa Tatu Asubuhi*)